**Condensed Great Controversy in Swahili**

# VITA KUU

Baina ya Kristo na Shetani
Ellen G. White

## *VALIYOMO*

Sura Ukurasa


Dibaji 7
1. Uasi Mkuu 9
2. Siri ya Kuasi 16
3. Watengenezaji wa Kanisa la Zamani 29
4. Jinsi Luther Alivyoleta Matengenezo Makubwa 53
5. Maendeleo ya Matengenezo ya Dini 42
6. Kushindsva Kuendelea 50
7. Ujumbe wa Malaika wa Kwanza 53
8. Ujumbe wa Malaika wa Pili 63
9. Kilio cha Usiku wa Manane 69
10. Patakatifu 76
11. Ujumbe wa Malaika wa Tatu 81
12. Jukwaa Lililo Imara 88
13. Madanganyifu ya Shetani 92
14. Imani Iuu va Kuone-ca na Mizimu 98
15. Sauti Kuu 106
16. Mwisho wa Rehema 109
17. Wakati wa Taabu ya Yakobo 114
18. Kuokolewa kwa Watakatifu 117
19. Ujira wa Watakatifu 121
20. Miaka Elfu 123
21. Ufufuo wa Pili 126
22. Kumtawaza Kristo 129
23. Sauti ya Pili 136
24. Ulimwengu Mpya 140


## *Ujumbe wa Mwandishi kwa Wasomaji wa Kitabu Hiki*

KWA njia ya mwangaza wa Roho Mtakatifu, mambo ya shindano baina ya wema na uovu, ambalo limeendelea tangu zamani, yamefunuliwa kwa mwandishi wa kitabu hiki. Mara kwa mara niliruhusiwa kuona yaliyofanywa nyakati nyingine maalum katika shindano kuu baina ya Kristo, aliye Mkuu wa Uzima, na Sababu ya wokovu wetu, na Shetani aliye mkuu wa uovu, na sababu ya dhambi, mwasi wa kwanza wa amri takatifu za Mungu. Uadui wa Shetani juu ya Kristo umeonyeshwa juu ya wafuasi wake. Chuki ile aliyokuwa nayo juu ya sheria ya Mungu, shauri lue fake la udanganyifu, ambalo kwalo hufanya uongo kuonekana kana kwamba ni kweli, tena kwalo wanadamu huongozwa wakakisujudia kiumbe badala ya Muumba: mambo haya yameonekana tangu awali. Jitihada ya Shetani katika kueleza vibaya tabia za Mungu, na katika kuongoza wanadamu wamdhanie Mungu kwa namna isiyo ya haki, hata wamwogope n kumehukia badala

ya kumpenda; jinsi ambavyo amejaribu kubatili amri ya Mungu, na lcuongoza wanadamu ili wafikiri kwamba wamekuwa huru, tena ya kama haiwalazimu kufuata matakwa ya sheria yake; jinsi ambavyo anawadhulumu wale wanaothubutu kuyapinga madanganyifu yake, haya ndiyo mashauxi ambayo ameyafuata katika vizazi vyote... .

Katika vita kuu ya mwisho, Shetani atafanya namna ile ile, atakuwa n nia ile ile, tena atakuwa n kusudi sawa na file alilokuwa nlo tangu zamani zote za kale. Mambo yaliyofanywa zamani yatafanywa tena, isipokuwa mashindano yajayo yatakuwa niakali mno jinsi isivyokuwa duniani tangu awali. Madanganyifu va Shetani yatakuwa werevu zaidi, mashambulio yake yatakuwa magumu zaidi, kama yamkini, atawapoteza hata wateule wa Mungu. (Soma Marko 13:22, na Mathayo 24:24). . . .

Kusudi la kitabu hiki siyc kuonyesha mambo mapya hasa juu ya siku za kale, ila kueleza mambo ya hakika yanayohusika na mambo yajayo. Walakini, yakitazamiwa na kufikiriwa jinrsi yalivyo sehemu ya shindano baina ya nguvu za nuru na za giza, mambo haya ya zamani huonekana kuwa na maana mpya; kwa ajili yake nuru inaangaza siku zijazo, ikimulika njia yao ambao, kama watengezaji wa zamani wa dini, wataitwa, hata kwa kujihatarisha maisha, wawe mashahidi kwa ajili ya "Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu." Ufunuo 1:1.

Makusudi ya kitabu hiki ndiyo kufunua mambo ya shindano kuu baina ya kweli na uongo; kudhihirisha hila za Shetani, tena namna anavyoweza kushindwa; kueleza habari za uovu jinsi ulivyo, kuonyesha chanzo cha dhambi na jinsi itakavyomalizwa, na kueleza mambo haya kwa namna ya kufaa kwa kudhihirisha haki na wema wa Mungu katika yote awatendeavyo wanadamu; na kuonyesha sheria yake jinsi ilivyo takatifu na isivyobadilika; haya ndiyo makusudi ya kitabu hiki. Tena ombi la mwandishi ndilo hili: ili, kwa mvuto wa maneno yake, watu wapate -kuokolewa katika nguvu za giza, wapate kustahilishwa "kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru," kwa sifa yake aliyetupenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yetu. (Kol. 1:12; Gal. 2:20.)

Ellen G. White



# UASI MKUU

YESU alipowafunulia wanafunzi wake ajali itakayoujia Yerusalemu, na mambo yatakayoonekana katika marejeo yake, aliwaambia pia juu ya hali ya maisha ya watu wake tangu wakati atakapochukuliwa kwao, mpaka kurudi kwake pamoja na uwezo na utukufu apate kuwaokoa. Pale katika mlima wa Mizeituni, Mwokozi aliiona mbele dhoruba ya mateso ambayo yalitaka kuja kulipata kanisa la mitume; na alipotazama sana mambo yajayo, macho yake yalitambua taabu na zama za giza na mateso makali yatakayokuja kuwataabisha wafuasi wake. Kwa maneno machache, yenye maana sana, ya kutisha, alitabiri juu ya mambo ambayo watawala wa dunia hii wangeyafanya juu ya kanisa katika njia ya udhilifu, mashutumu na mateso ambayo Bwana wao aliyapitia. Uadui ambao watu wa dunia walikuwa nao juu ya Mwokozi wa dunia, ungeonyeshwa vivyo hivyo kwa watu wanaoliamini jina lake.

Habari za kanisa la zamani zilionyesha utimizo wa maneno ya Mwokozi. Mamlaka za dunia na za ahera zilishindana na Kristo kwa njia ya kuwatesa wafuasi wake. Mamlaka za kishenzi kwenye kuabudu miungu ya uongo waliona mbele ya kwamba Injili ikipata kusitawi, hekalu na madhabahu yao yatatokomelea mbali: kwa hivyo mamlaka

yale yakatumia uwezo wake wote kwa kuiharibu dini ya Kikristo. Mateso makali sana yakaanzishwa. Wakristo walinyang'anywa mali zao na kufukuzwa katika nyumba zao. "Wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani." Ebr. 11:36. Watu wengi sana walitimiza ushuhuda wao kwa damu yao. Watu mashuhuri na watumwa, matajiri na maskini, walioelimika na wasio na elimu, waliuawa wote bila rehema.

Lakini Shetani alishindwa kuliharibu kanisa la Kristo kwa jeuri, ingawa alijaribu sana. Shindano lile kuu ambalo kwalo wanafunzi wa Yesu walitoa maisha yao halikukoma wakati wale mitume waaminifu walipouawa. Ushindi ulikuwa wao. Watenda kazi wa Mungu waliuawa, lakini kazi yake iliendelea kusitawi. Injili iliendelea kuenea, na idadi ya wafuasi wa Injili iliongezeka. Injili ilipenya katika sehemu za nchi zisizoingiliwa hata mahali pa mamlaka ya Rumi. Mkristo fulani alisema maneno haya alipokuwa akiwagombeza watawala washenzi waliokuwa wakichochea sana yale mateso: "Mnaweza kutuua, kututesa, kutuhukumu. . . . Dhulumu lenu ndilo linaloshuhudia ya kwamba hatuna hatia. . . . Wala jeuri yenu haiwafaidieni kitu." Lakini mateso haya yalikuwa kama mwito wa kuwavuta wengine washirikiane nao katika imani yao. Wakristo walisema hivi, "Kwa kadiri mnavyotufyeka kama majani, ndivyo tunavyozidi kusitawi: damu ya Wakristo ni kama mbegu."

Watu maelfu walifungwa gerezani na kuuawa: lakini wengine walitokea na kujaza mahali pao. Na wale waliouawa kwa ajili ya imani yao, waliyakinishwa kuwa wa Kristo, wakahesabiwa naye kuwa washindi. Walikuwa wamepiga vita vilivyo vizuri, na walitazamia kuipata taji ya

haki siku Kristo atakaporudi. Maumivu ambayo Wakristo waliyavumilia yaliwaleta karibu na wenzao zaidi, na pia karibu na Mwokozi wao. Mfano wao wakati walipokuwa wazima, na ushuhuda wa kufa kwao, ulishuhudia daima juu ya ukweli wa Mungu; na mahali pasipotazamiwa kamwe, raia za Shetani walikuwa wakiacha kumtumikia na wakajitia chini ya bendera ya Kristo.

*Mapatano Yaliyofanywa na Ushenzi*

Kwa hivyo Shetani aliazimia kupigana vita vikali zaidi na mamlaka ya Mungu, kwa kutia bendera yake katika kanisa la Kikristo. Kama wafuasi wa Kristo wangeweza kudanganywa na kuongozwa kumwasi Mungu, ndipo nguvu yao na uthabiti wao ungepungua, na wangeshindwa kwa urahisi.

Adui mkuu sasa alijitahidi kufanya kwa hila jambo lile aliloshindwa kufanya kwa nguvu. Mateso yalikoma, na badala yake yalikuja mashawishi ya kimwili yenye hatari ya kutamanisha watu kama fanaka na heshima ya kidunia. Watu waliokuwa wakiabudu sanamu walivutwa kupokea sehemu ya imani ya Kikristo, na huku walikana mambo mengine yaliyokuwa ya muhimu sana. Walijidai ya kwamba walimkubali Yesu kama Mwana wa Mungu, na kuamini juu ya kufa na kufufuka kwake lakini hawakuchomwa mioyoni na kujua ya kwamba ni wenye dhambi, kwa hivyo hawakuona ya kwamba wana haja ya kutubu na kugeuka mioyoni. Wakristo kwa mambo mengine, waliwashauri Wakristo ili wao pia wapate kuwaridhisha kwa mambo yao mengine, kusudi wote waungane katika kumwamini Kristo.

Sasa kanisa liliingia katika hatari kubwa zaidi. Kufu-

ngwa gerezani, kuteswa, kuunguzwa kwa moto na kuuawa kwa panga kulikuwa kama mibaraka zikilinganishwa na hatari hii ya baadaye. Wakristo wengine walisimama imara, wakisema ya kwamba hawawezi kufanya upatanisho na dini ya kishenzi. Wengine walisema ya kwamba wakijitoa au kubadili kidogo mambo makubwa ya imani yao, na kuungana na wale waliopokea sehemu tu ya Ukristo, labda kwa njia hiyo wangewavuta hata waongoke mioyo kabisa. Ulikuwa wakati wa maumivu makuu ya rohoni kwa wafuasi waaminifu wa Kristo. Kwa njia ya watu waliojifanya kuwa ni Wakristo, Shetani alijiingiza pole pole katika kanisa, kusudi kuipotosha imani yao na kugeuza fikara zao kutoka kwa ukweli.

Hatimaye wingi wa Wakristo walishusha kipeo chao cha kanuni za dini, na wakafanya umoja fulani kati ya Ukristo na Ushenzi. Ingawa waabuduo sanamu walijidai kuwa wamegeuka, na kuungamana na kanisa, lakini waliendelea kuishikilia ibada ya sanamu, ila tu walibadilisha vitu walivyoabudu, vikawa sanamu michoro ya Yesu, hata na ya Mariamu na wafu walioheshimiwa. Chachu hii mbaya ya ibada ya sanamu, baada ya kuingizwa hivi kanisani, iliendelea na kazi yake ya uharibifu. Mafundisho yasiyo ya kweli, urembo wa ibada kama ya mambo ya ushirikina, na kawaida na ibada za sanamu ziliingizwa katika mafundisho na ibada za dini. Wafuasi wa Kristo walipoungamana hivi na waabuduo sanamu, dini ya Kikristo ilichafuliwa na kanisa lilipoteza utakatifu na uwezo wake. Walakini, kulikuwa na wengine ambao hawakupotoshwa na madanganyifu haya. Walishikilia uthabiti wao kwa Yeye mwenye kweli, wakamwabudu Mungu peke yake.

Tangu awali, wale wanaojiita kuwa ni wafuasi wa

Kristo wamekuwa wakigawanyika makundi mawili. Kundi moja la watu wakijifunza juu ya maisha ya Mwokozi kwa moyo, na kijibidisha sana kusahihisha maisha yao na kumfuasa Kristo, mfano wao; kundi la pili la watu huyadharau mafundisho yaliyo dhahiri na ya kweli kwa kuwa huyafunua makosa yao. Hata katika siku za usitawi, si kwamba watu wote waliokuwako kanisani walikuwa wenye haki, wenye mioyo safi, waaminifu. Mwokozi wetu alitoa fundisho ya kwamba wale ambao hufanya dhambi kwa kusudi wasikubaliwe kuingia kanisani; walakini, Yeye mwenyewe aliungamana na watu waliokuwa wapotovu kwa tabia zao, wapate kusaidiwa na mafundisho yake na kwa mfano wa maisha yake, kusudi wapate nafasi ya kusahihisha maisha yao.

Lakini hakuna umoja kati ya Mkuu wa nuru na mkuu wa giza, wala wafuasi wa wakuu hawa wawili hawawezi kupatana. Wakristo walipokubali kuungana na watu waliokuwa wamegeuka nusu tu kutoka kwa ushenzi waliingia katika njia iliyowatenga mbali na haki ya Mungu na mbali zaidi. Shetani alisimanga kwa vile alivyopata kuwadanganya wafuasi wengi wa Kristo. Ndipo Shetani aliendelea kuwaongoza zaidi, hata aliwatilia nia ya kuwatesa wale waliodumu kuwa wenye haki kwa Mungu. Hakuna ajuaye namna ya kushindana na imani ya kweli ya Kikristo kama wale waliokuwa wakiipigania mara ya kwanza; na hawa Wakristo waliomwasi Mungu, kwa kuungana na wenzao waliokuwa nusu washenzi, walianza kufanya vita na mafundisho ya Kristo yaliyo ya muhimu zaidi.

Wale ambao walitaka kuwa waaminifu, iliwapasa kushindana vikali sana, wakisimama imara na kujihadhari na madanganyifu na machukio yaliyofunikwa na mavazi ya

kikasisi na kuletwa katika kanisa. Biblia haikukubaliwa kuwa upeo wa imani. Mafundisho ya uhuru wa kuwa mfuasi wa dini yo yote bila kuzuiwa na sheria yaliitwa uzushi, na wale walioyafuata walichukiwa na kugombezwa.

*Kujiondoa kwa Waaminifu*

Baada ya mashindano makali yaliyoendelea kwa muda mrefu, watu wachache waaminifu waliazimia kuutangua ushirika wote uliokuwa kati yao na kanisa lililoasi ikiwa litaendelea kukataa kuondoa madanganyifu na ibada ya sanamu. Waliona ya kwamba utengano ulikuwa ni lazima kama wakitaka kulitii Neno la Mungu. Waliona ya kwamba wakitaka kulitii Neno la Mungu hawana budi kujitenga. Hawakuweza kamwe kukubaliana na mambo ya uongo yaliyohatarisha roho zao wenyewe, na kuweka mfano ambao ungehatarisha imani ya watoto wao hata wajukuu wao. Makusudi wawe na amani na umoja walikuwa tayari kukubali jambo lo lote lililohusiana na uaminifu kwa Mungu; lakini waliona ya kwamba kupata amani kwa njia ya kutupa mambo ya asili ya dini ingekuwa vigumu kwao. Kama umoja usingekuwako, ila kwa njia ya kuyatupa mambo ya kweli na ya haki basi, na uwepo utengano, hata na mashindano. Ingekuwa vyema kwa kanisa na kwa dunia kama mafundisho yale yaliyowaongoza wale waliosimama imara yangehuishwa katika mioyo ya wale wanaojidai kuwa ni watu wa Mungu.

Mtume Paulo asema ya kwamba "na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa." 2 Tim. 3:12. Kwa nini basi, mateso yanaonekana ya kwamba yamefifia? Sababu yake tu ni kwamba kanisa limejifananisha na dunia, na kwa hivyo kanisa halishikilii mambo

ya adili yawezayo kuleta ushindani. Hali ya dini katika siku zetu haifanani kwa usafi na utakatifu na hali ya imani ya Wakristo walioishi katika siku za Kristo na mitume. Sababu yake tu ni kwamba kanisa lina hali ya kupatana na dhambi, na kwa kuwa mafundisho makuu na Neno la Mungu hayajaliwi sawa, na kwa kuwa hali ya utauwa imekuwa kidogo kanisani, ndiyo maana ya dini ya Ukristo kupendelewa na watu wa dunia. Hebu kuwepo na huisho la imani na uwezo ule uliokuwako katika kanisa la zamani, ndipo na moyo wa kuwatesa Wakristo utakapoamshwa, na mateso makali yataanzishwa mara ya pili.



# SIRI YA KUASI

MTUME Paulo, katika barua yake ya pili kwa Wathesalonike, aliuagua uasi mkuu ambao mwishowe ungetokea utawala wa Kanisa la Kirumi. Alisema dhahiri ya kwamba siku ya Kristo haitakuja "usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe huketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu." Zaidi ya haya, mtume awaonya ndugu zake ya kwamba ile"siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi." 2 The. 2:3, 4, 7. Hata zamani zile aliona makosa yakiingia polepole kanisani, ambayo yangetengeneza njia ya kukuza utawala wa Kanisa la Kirumi.

Polepole, kwa hila na kwa siri mwanzoni, ile siri ya kuasi iliendeleza kazi yake ya udanganyifu na kumtukana Mungu; lakini kwa kadiri ilivyozidisha nguvu na kuzitawala nia za watu, hivyo ndivyo alivyozidi kufanya kazi yake kwa wazi.

Punde kwa punde, kwa kadiri isiyoonekana, madhehebu ya makafiri yaliingizwa katika kanisa la Kikristo. Kwa muda fulani ile nia ya kufanya mapatano na kuyaingiza madhehebu ya makafiri ndani ya kanisa ilizuiliwa kwa sababu ya mateso makali ambayo kanisa lilipata chini ya

utawala wa ushenzi. Lakini mateso yalipokoma, tena dini ya Kikristo ilipokaribishwa hata kwa majumba ya wafalme, kanisa lilianza kupunguza hali yake ya kufafana na Kristo na mitume kwa unyenyekevu na unyofu, wakaanza kufanya fahari na kiburi sawa na mahaini na watawala wa dini ya kishenzi; na badala ya matakwa ya Mungu, kanisa liliweka mafundisho na maelezo ya kibinadamu. Kulikuwa na shangwe kuu Konstantine alipoongoka mnamo mwanzo wa karne ya nne baada ya Kristo; lakini kuongoka kwake kulikuwa kwa jina tu; ndipo mambo na matendo ya kidunia yakaingia kanisani, yakawa kama yakifunikwa na kuhalalishwa na haki ya kanisa. Halafu kazi ya uhalifu ikaendelea upesi. Dini ya ushenzi, ijapokuwa ilionekana kana kwamba imeshindwa, ilikuwa ikishinda. Roho yake ndiyo iliyotawala kanisani. Madhehebu yake, kawaida zake na matendo yake ya sherehe, hata na mambo kama ya ushirikina yalichanganywa pamoja na imani na ibada ya wale wanaojidai kuwa ni wafuasi wa Kristo.

Kwa ajili ya mapatano haya kati ya Ushenzi na Ukristo, aliadhimishwa yule mtu wa dhambi aliyetabiriwa kuwa ni mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya Mungu. Maungo makubwa haya ya dini ya uongo ndiyo kazi kubwa ya ajabu inayofanywa kwa nguvu ya Shetani,—inaonyesha kujitahidi kwake katika kujiweka katika kiti cha enzi, na kuitawala dunia jinsi apendavyo.

Kwa vile kanisa lilivyotamani kupata faida na heshima ya kidunia, liliongozwa kutaka fadhili na msaada kutoka kwa wakuu wa dunia; na kwa vile lilivyomkana Kristo, lilivutwa kujitia chini ya uongozi wa yule mwovu.

Fundisho moja kuu la Kanisa la Kirumi ni ya kwamba papa (pope) ndiye kichwa kionekanacho cha Kanisa la

Kristo katika mahali pote, ambaye amepewa utawala kabisa juu ya maaskofu na wahubiri wote duniani pote. Zaidi ya hayo, papa amejitwalia majina yale yanayokuwa ya Mungu hasa.

Shetani alijua dhahiri ya kwamba kwa kusoma Maandiko Matakatifu wanadamu wangeweza kufahamu madanganyifu yake na kuzuia nguvu zake. Hata Mwokozi wa ulimwengu alimpinga na Neno Takatifu. Kristo alimshinda kila mara akimpiga na ngao ya ukweli wa Mungu, kwa kusema, "Imeandikwa." Alilipinga kila shauri la adui kwa hekima na uwezo wa Neno. Basi kama Shetani alitaka kudumu katika kuwatawala wanadamu na kuthibitisha mamlaka ya Kanisa la Kirumi, ambalo lilijitwalia nguvu isiyo yake, ilimpasa Shetani kuweka watu katika kutofahamu Maandiko Matakatifu. Biblia ingemtukuza Mungu na kuwafahamisha wanadamu hali yao ya kweli; na kwa hiyo ilikuwa ni lazima kuyafunga na kuyasetiri mafundisho matakatifu ya Biblia. Tena Kanisa la Kirumi likatumia njia hii. Kwa karne nyingi kuvieneza vitabu vya Biblia kulikuwa haramu. Watu walikatazwa wasiisome Biblia wala kuwa nayo nyumbani; tena mapadre na maaskofu wapotovu wakaeleza mafundisho ya Biblia kwa namna ilivyoweza kuthibitisha uongo wao. Kwa njia hii papa alipata kukubaliwa karibu duniani pote ya kwamba yu kaimu wa Mungu duniani, ambaye amepewa mamlaka makuu juu ya kanisa na serikali pia.

### *Wakati na Sheria Zabadilishwa*

Kama kimekwisha kuondolewa kitu kilichoweza kuvumbua mambo ya uongo, basi Shetani aliweza kufanya




*Amri ya Konstantine ya kuweka Jumapili kuwa siku ya mapumziko badala ya Sabato, jinsi ilivyoandikwa kwa Kilatini. (Tazama ukurasa* 28 *jinsi amri hii ilivyofasiriwa kwa Kiswahili).*

apendavyo. Maneno ya unabii yalisema dhahiri ya kwamba Kanisa la Kirumi litatumaini "kubadili majira na sheria." Danieli 7:25. Tena halikukawia kujaribu kufanya hivyo. Makusudi kuwavuta watu kutoka dini ya kishenzi, na kuwawezesha waongoke kwa urahisi katika dini ya Kikristo, badala ya kuabudu sanamu za kishenzi likaingizwa kanisani tendo la kusujudu picha au sanamu zilizowekwa wakfu, pamoja na makumbusho ya watakatifu wa kale. Na mwishowe amri iliyotolewa na baraza kuu (iitwayo "General Council") ilithibitisha kawaida hii ya ibada ya sanamu katika Kanisa la Kirumi. Na kwao kutimiliza jambo hili la kukufuru na kumchukiza Mungu, Kanisa la Kirumi likathubutu kuondolea amri ya pili katika sheria ya Mungu, yaani amri ile inayokataza tendo la kuziabudu sanamu, tena wakagawa amri ya kumi kuwa sehemu mbili, ili waidumishe hesabu yake ya zamani.

Lakini nia hii ya kutoa idhini kwa matendo kama ya kishenzi ili yafanywe kanisani, ilitengeneza njia ili mamlaka ya Mungu ipate kudharauliwa zaidi. Shetani aligeuza amri ya nne pia, akijaribu kuondoa Sabato ya zamani, yaani siku ile ambayo Mungu aliibariki na kuitakasa; na mahali pake alitukuza siku ile iliyoshikwa na washenzi kuwa kama "siku kuu ya jua." Mwanzoni badilisho hili halikufanywa dhahiri. Katika karne chache baada ya Yesu, Wakristo wote wakaishika Sabato ile iliyo ya kweli. Wakawa na uangalifu sana juu ya heshima iliyomhusu Mungu, wakaamini ya kwamba sheria yake haibadiliki, wakafanya bidii katika kuutunza utakatifu wa maagizo yake. Lakini Shetani alitumia hila sana kwa mawakili wake ili wapate kulitimiliza kusudi lake. Makusudi akawatazamisha watu siku kuu ile ya jua (yaani Sunday), siku ile ilifanywa

kuwa siku kuu ya kukumbuka ufufuo wa Kristo. Ikafanywa thubutu kuondoa amri ya pili katika sheria ya Mungu, mikutano ya dini siku ile; hata hivyo ikahesabiwa kuwa siku ya mchezo na furaha, tena Sabato ikashikwa kuwa siku takatifu.

Konstantine alipokuwa angali mshenzi, alitoa amri akiamuru ili "Sunday" iwe siku kuu kwa watu wote na mahali pote katika Ufalme wa Kirumi. Baada ya kuongoka kwake aliendelea kuishika siku ya "Sunday," tena amri ile aliyoitoa alipokuwa mshenzi, ilitiliwa nguvu kwa ajili dini yake mpya. Lakini kadiri siku ile ilivyotukuzwa haikutosha kuwazuia Wakristo wasiishike Sabato ya kweli kuwa siku takatifu ya Bwana. Basi ilikuwa ni lazima jambo jingine lifanywe; sabato ile ya uongo lazima ipate kutukuzwa sawa na Sabato ile ya kweli. Miaka michache baada ya Konstantine kutoa amri yake, Askofu wa Rumi alitoa neno kwa kuiita "Sunday" kuwa ni siku ya Bwana. Kidogo kidogo hivi, watu waliongozwa mpaka kuihesabu hiyo kuwa ni siku takatifu. Lakini watu wakaendelea kuishika Sabato ya zamani.

Lakini yule mdanganyifu mkuu alikuwa hajamaliza kazi yake. Aliazimia kukusanya jamii ya Wakristo wote chini ya uongozi wake, na kutumia nguvu zake kwa njia ya Askofu wa Rumi mwenye kujivuna na kujidai kuwa ni kaimu wa Kristo. Kwa njia ya watu waliojidai kuwa ni Wakristo lakini ni kama nusu washenzi, na kwa maaskofu waliotaka makuu, na kwa washiriki wa kanisa waliopenda anasa za kidunia, basi Shetani alifikiliza kusudi lake. Mara kwa mara zikakusanywa baraza zilizo kubwa, ambamo wakaitwa wakuu wa kanisa kutoka duniani pote. Na katika baraza karibu zote, Sabato ile iliyowekwa na Mungu ili-

kuwa ikizidi kuondolewa heshima na kutwezwa, na "Sunday" ikazidi kutukuzwa. Kwa namna hiyo siku kuu ya kishenzi ikapata kutukuzwa kuwa kama jambo lililowekwa na Mungu, na huku Sabato ya Biblia ikatangazwa kuwa ni msazo wa dini ya Kiyahudi, tena wale waliotukuza siku ile wakanenwa kuwa wamelaaniwa.

Sasa yule mwasi mkuu alikuwa amefaulu katika kujiinua nafsi "juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa." 2 The. 2:4. Alikuwa amethubutu kugeuza amri katika sheria ya Mungu iliyo amri ya pekee ambayo kwa dhahiri huwaonyesha wanadamu Mungu wa kweli aliye hai. Katika amri ya nne Mungu hudhihirishwa kuwa ni Muumbaji wa mbingu na nchi, na kwa hiyo ametofautishwa na miungu mingine yote ya uongo. Siku ya Saba ilitakaswa kuwa pumziko kwa wanadamu ili iwe kama ukumbusho wa kazi za kuumba. Ilikusudiwa kuwa kitu cha kuwakumbusha wanadamu daima ya kwamba Mungu aliye hai ndiye asili ya kuwako kwetu, tena yeye ndiye ahusuye kuheshimiwa na kusujudiwa. Shetani hujitahidi katika kuwavuta watu wasimche Mungu wala kuitii sheria yake; kwa hiyo hujitia katika kushindana na amri ile hasa ambayo huwaonyesha watu jinsi Mungu alivyo Muumba.

Sasa Waprotestanti (yaani Wakristo wasiokubali baadhi ya mafundisho ya Kanisa la Kirumi) walio wengi husema sana ya kwamba "Sunday" ndiyo Sabato ya Wakristo kwa ajili ya ufufuo wake Kristo. Lakini Biblia haishuhudii neno hilo. Wala Kristo mwenyewe wala mitume wake hawakutukuza siku hiyo. Jambo la kuishika "Sunday" kuwa kama siku kuu ya Kikristo lilianzishwa na ile "siri

ya kuasi" ambayo ilikuwa imeanza kutenda kazi yake hata zamani zile katika siku alipoishi Paulo. Basi siku gani, tena mahali gani ambapo Bwana alikubali jambo hili ambalo ni mzaliwa wa Kanisa la Kirumi? Tena inaweza kutolewa sababu gani yenye nguvu kwa kuthibitisha badilisho hili ambalo haliwezi kamwe kuthibitishwa na Maandiko Matakatifu?

Katika karne ya sita, mamlaka ya Papa yalikuwa yameimarishwa zaidi. Kiti cha enzi yake kiliwekwa katika mji mkuu wa kifalme, naye Papa akatangazwa kuwa ni kichwa cha makanisa yote. Mamlaka ya zamani ya Ushenzi iliiondokea ile mamlaka ya Papa. Joka alikuwa amempa nyama "nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi." Ufunuo 13:2. Miaka 1260 ya mateso ya Kanisa la Kirumi ambayo yalitabiriwa na Danieli na Yohana yalikuwa yakianzishwa. (Danieli 7:25; Ufu. 13:5-7). Wakristo walishurutishwa kuchagua, ili watupe uaminifu wao na kukubali urembo wa dini na ibada za Kanisa la Kirumi, ama kumaliza maisha yao gerezani, kuunguzwa kwa moto, kushtushwa viungo katika mtambo, au kukatwa vichwa. Ndipo maneno haya ya Yesu yakatimia, "Nanyi mtasalitiwa na wazazi wenu, na ndugu zenu, na jamaa zenu, na rafiki zenu, nao watawafisha baadhi yenu. Nanyi mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu." Luka 21:16,17. Mateso yaliwapata waaminifu kwa ukali usivyoonekana tangu awali, na dunia yote ikawa kama uwanja wa vita. Kwa miaka mia nyingi watu wa kanisa la Kristo walikuwa wakijificha. Hivyo ndivyo asemavyo nabii: "Yule mwanamke akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengenezwa na Mungu, ili wamlishe huko muda wa siku elfu na mia mbili na sitini." Ufunuo 12:6.

### *Zama za Giza*

Mwanzo wa utawala wa Kanisa la Rumi ulikuwa mwanzo wa Zama za Giza. Kwa kadiri uwezo wa kanisa lile ulivyoongezeka, ndivyo na giza ilivyozidi kuwa nene. Imani ya watu ikatolewa kutoka kwa Kristo aliye msingi wa kanisa wa haki, wakamwadhimisha papa. Badala ya kumtegemea Mwana wa Mungu kwa kuzisamehe dhambi na kwa wokovu wa milele, watu wakamtazamia papa na maaskofu na makasisi ambao papa aliwapa mamlaka. Walifundishwa ya kwamba papa ndiye aliyekuwa mpatanishi wao mbele za Mungu, na ya kwamba hakuna awezaye kumkaribia Mungu isipokuwa kwa papa, tena ya kwamba papa alikuwa mahali pa Mungu kwao, na kwa hiyo alistahili kuheshimiwa na kusikiwa kabisa. Kukosa kumtii na kuyafanya mapenzi yake papa kulikuwa sababu ya mkosaji kupata adhabu kali ajabu mwilini na rohoni.

Hivi fikara za watu zikageuzwa toka kwa Mungu, ili wawaadhimishe wanadamu wakosaji na wakatili—naam, wakamheshimu mfalme wa giza mwenyewe, ambaye aliwaongoza na kuwatumia kwa kazi yake. Dhambi ilifunikwa na vazi la utakatifu. Maandiko Matakatifu yanapokataliwa, na mwanadamu anapoanza kujidhania kwamba yeye ndiye mkuu, hapo twaweza kutazamia ulagai, udanganyifu, na ufisadi. Kwa kuzikuza sana sheria na desturi za kibinadamu, ndipo ubaya wa kila namna ukatokea kwa ajili ya kuacha kuzifuata amri za Mungu.

### *Siku za Taabu*

Siku zile zilikuwa siku za taabu kwa kanisa la Kristo. Watu waliokuwa thabiti kweli kweli walikuwa wachache sana. Ingawa mashahidi wengine walibaki ili kuutunza

ukweli, lakini mara zingine ilionekana ya kwamba dhambi na ibada ya namna ya ushirikina ilikaribia kushinda, na dini ya kweli ilikuwa karibu kutoweka kabisa duniani. Injili ilisahauliwa, lakini mifano mitupu ya dini ilizidishwa, na watu walilemewa kwa kutozwa fedha nyingi isiyo ya haki.

Si kwamba walifundishwa tu kumtazamia papa kuwa mpatanishi wao, lakini pia walifundishwa wapate kuzitegemea kazi zao wenyewe kusudi waupate upatanisho wa dhambi. Safari ndefu, adhabu za makosa, kuyaabudu makumbusho ya watakatifu wa kale, kuyajenga makanisa, mahali pa sanamu, na madhabahu, na kulipa pesa nyingi kwa kanisa—haya yote na matendo mengine ya namna hayo yalishurutishwa kwa nguvu makusudi kuituliza ghadhabu ya Mungu, au wapate kufadhiliwa na Mungu; kana kwamba Mungu, hufanana na wanadamu, tena hasira yake huwaka kwa mambo ya upuzi, au anaweza kutulizwa na sadaka au vitubio!

Karne nyingi zilipoongezeka, ikaonekana ya kwamba makosa ya mafundisho yaliyotolewa na Rumi yalikuwa yakiongezeka sana. Hata kabla ya kuimarishwa kwa mamlaka ya Papa, mafundisho ya washenzi wenye elimu yalikuwa yameingia kanisani. Wengi ambao walijidai ya kwamba wameongoka moyo, walikuwa wakiyashikilia madhehebu ya elimu ya kishenzi, tena hawakuendelea kujifunza mambo yao peke yao tu, bali waliwashurutisha wengine kuyapokea mafundisho yale, ili kwa njia ile wapate kuwa na nguvu na mvuto miongoni mwa washenzi. Hivi mafundisho makubwa ya uongo yalianza kuingia katika dini ya Kikristo. Mojawapo lililo kuu zaidi kati ya haya lilikuwa fundisho lililosema ya kwamba wanadamu wana hali ya kuishi milele, na ya kwamba wafu huwa na ufahamu wa

nafsini. Fundisho hili la uongo ndilo lililokuwa asili ya kawaida ya Kirumi ya kuwaabudu watakatifu wa zamani na kumsujudu Mariamu. Tokea fundisho hili, uzushi mwingine ukatokea ya kwamba wale wasiogeuka mwishoni, watateketezwa milele; fundisho hili lilipokewa na kuwa kanuni ya dini ya Kirumi wakati uasi ulipokuwa umeanzishwa karibuni.

Ndipo njia ikatengenezwa tena kwa uvumbuzi wa namna nyingine ya ushenzi, ambao Warumi waliuita "Purgatory", (yaani mahali pa kuwatakasa watu waliokufa); na njia hiyo ikatumiwa kwa kuwaogofisha watu wengi waliokuwa wajinga na washirikina. Uzushi huu ndio unaosema ya kwamba pana mahali pa ahera pa maumivu makali, ambapo watu wasiostahili kuhukumiwa milele wataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao, na baadaye wakisha kutakaswa na unajisi wao, ndipo watakapokubaliwa kuingia mbinguni.

Lakini fundisho jingine lilikuwa lazima kubuniwa, kusudi kuiwezesha Rumi kujifaidia na hofu na makosa ya wafuasi wake. Likabuniwa fundisho juu ya jambo liitwalo "*Indulgence,*" yaani ahadi ya kuachiliwa dhambi, kwa ajili ya kufanya jambo fulani. Maondoleo kabisa ya dhambi, yaani dhambi zilizopita, za sasa na zitakazofanywa baadaye, na kuondolewa maumivu yote na adhabu zote zipasazo, mambo hayo yote yaliahidiwa kwa wale waliokubali kujitoa kwa kupiga vita vya papa kwa kuieneza milki yake ya dunia hii, kuwatesa adui zake, au kuwaharibu wale waliothubutu kuukanusha ukuu wake. Watu walifundishwa pia ya kwamba kwa kulipa pesa kwa kanisa, waliweza kuondolewa dhambi, na pia kuwaweka huru rafiki zao waliokuwa wakiadhibika katika ndimi za moto. Hii ndiyo njia

ambayo kwayo Rumi ilijaza masanduku yake ya pesa, na kuufululiza utajiri, fahari, na ufisadi wa wale waliojidai kuwa wajumbe wa Yule asiyekuwa na mahali pa kulaza kichwa chake.

Agizo la Biblia juu ya meza ya Bwana lilikuwa limeondolewa, na badala yake iliwekwa ibada ya Misa, ambayo ni kama ibada ya sanamu. Kwa njia ya kufanya mambo yasiyo na maana, makasisi wa Kanisa la Kirumi walijidai ya kwamba walikuwa na uwezo wa kugeuza mkate na mvinyo kuwa mwili na damu ya Kristo kweli. Kwa ufidhuli na makufuru walijidai ya kwamba wana uwezo wa "Kumwumba Muumba wao." Wakristo wote walishurutishwa kukiri kwamba waliamini uzushi huu ambao kweli ulikuwa ukimtukana Mungu ama wapate adhabu ya kufa. Wale waliokataa kuufuata uzushi huo waliteketezwa kwa moto.

Mamlaka ya Rumi yalipozidi kuenea, ndipo uovu wao ukaongezeka duniani. Maandiko Matakatifu yalikaribia kupotea kabisa, si kwa watu peke yao, bali na kwa makasisi pia. Kama Mafarisayo wa zamani, watangulizi wa Kirumi waliuchukia mwanga, usije ukazifunua dhambi zao. Baada ya kuiondoa sheria ya Mungu, ambayo ilikuwa kipeo cha ukamilifu, wakaanza kutumia nguvu bila kiasi, wakatenda mabaya bila kizuizi. Ulaghai, tamaa ya mali; na uasherati ukazidi. Watu hawakuepukana na tendo lo lote la uhalifu lililoweza kuwaletea mali au cheo. Majumba ya mapapa na maaskofu yalijaa zinaa na ulevi. Mapapa wengine wakuu walifanya mambo ya uhalifu na kuchukiza mno, hata watawala wa serikali ya nchi walijaribu kuwauzulisha wale wakuu wa kanisa, wakiwaona kuwa ni watu wabaya kabisa wasiostahili kuyashika madaraka ya heshima. Kwa karne nyingi hayakuwa na maendeleo yo yote kwa kueli-

misha watu, kwa kazi ya ustadi, wala kwa ustaaarabu. Mambo ya kiroho na ya elimu yalizimishwa kabisa katika nchi zote za Kikristo.

---

* Maana ya maneno yaliyoandikwa katika Kilatini katika ukurasa 19: Constantino, mfalme August, kwa Helpidius: Katika siku kuu ya jua (Jumapili) madiwani wote na watu wote wakaao katika miji na wapumzike, tena viwanda vyote vya kazi vifungwe. Lakini katika vijiji, watu wanaofanya kazi ya ukulima, sheria inawaruhusu kuendelea kufanya kazi zao: kwani pengine inaonekana ya kwamba siku hiyo inafaa sana kwa kupanda mbegu za miche ya mizabibu kuliko siku nyingine: kwani wasipofanya hivyo, labda siku zinaweza kuwapitia ambazo zinafaa sana kwa kazi hizo kuliko siku zingine, tena wakikosa kupanda, mibaraka ya mbinguni inaweza kuwapitia. (Maneno haya yametolewa katika: *Schaff's History of the Christian Church,* Vol. III, section 75, paragraph 5. Note 1).



# WATENGENEZAJI WA KANISA LA ZAMANI

KATI ya giza iliyoipata dunia kwa muda ule mrefu wa utawala wa Kanisa la Kirumi, mwanga wa ukweli haukuweza kuzimishwa kabisa. Katika kila kizazi kulikuwa na mashahidi wa Mungu—watu waliohifadhi imani katika Kristo kama mpatanishi wa pekee kati ya Mungu na mwanadamu, watu walioheshimu Biblia kama kipeo cha pekee cha maisha, na walioitunza Sabato ya kweli. Watu wa vizazi vinavyowafuata watu hawa hawatafahamu kamwe ukuu wa mema wanaourithi kwa ajili ya matendo yao. Waliitwa wazushi, makusudi yao yalikanwa, tabia zao zilisengenywa, maandiko yao yalikatazwa, yalielezwa vibaya, au kuondolea sehemu fulani yenye maana sana. Walakini, walisimama imara, na katika kila kizazi waliihifadhi imani yao halisi, kama urithi mtakatifu kwa vizazi vya nyuma.

Vita vilipigwa vikali mno juu ya Biblia hata mara zingine nakili zilizobaki zilikuwa chache sana; lakini Mungu hakuliacha Neno lake liharibiwe kabisa. Mafundisho ya kweli yaliyomo hayakuweza kufichwa milele. Mungu aliweza kuyafunua maneno ya uzima kwa urahisi, jinsi alivyofungua milango ya gereza na kuviondoa vyuma vya milango kwa kuweka watenda kazi wake huru. Katika nchi mbali mbali za Ulaya, watu walivutwa na Roho ya Mungu

wapate kuitafuta kweli kama watu waitafutavyo mali iliyofichwa. Roho ya Mungu akiwaongoza kuchunguza Maandiko Matakatifu, waliyasoma maneno ya Biblia kwa furaha kuu ajabu. Walikuwa tayari kujipatia nuru hata kwa njia ya shida. Ingawa hawakuona mambo yote dhahiri sana, waliwezeshwa kufahamu mambo ya kweli yaliyokuwa yakifichwa tangu miaka mingi. Waliendelea mbele kama wajumbe waliotumwa na Mungu, wakiivunja minyororo ya upotovu na kuamini mambo kama ushirikina, uchawi, mizimu na kadha wa kadha, na kuwaita wale waliokuwa utumwani hivi kwa muda mrefu wapate kuondoka na kudai uhuru wao.

Wakati ulikuwa umewadia kwa Biblia kutafsiriwa ili watu wa nchi mbali mbali waipate katika lugha zao wenyewe. Wakati wa giza nene ya dunia ulikuwa umepita. Saa za giza zilitaka kumalizika, tena katika nchi nyingi ilikuwa kana kwamba zinaonekana dalili za pambazuko.

## *Nyota ya Asubuhi ya Matengenezo*

Katika karne ya kumi na nne, huko Uingereza kulitokea mtu fulani aliyeitwa John Wycliffe, aliyestahili, kuitwa "nyota ya asubuhi ya Matengenezo." Yeye ndiye aliyekuwa mtangulizi wa matengenezo ya kanisa, si kwa Uingereza peke yake, bali katika nchi zote za Kikristo. Alikuwa kama mzazi wa watu ambao baadaye waliitwa *"Puritans."* Wakati wake ulikuwa kama maji jangwani, kama taa siku zile za giza.

Bwana Mungu aliona ya kwamba kazi hii ya matengenezo ilifaa kuwekwa mkononi mwa mtu mwenye akili na uwezo, ambaye angeonyesha tabia njema na uaminifu katika kazi yake aliyopewa. Hali hii iliwanyamazisha wale

wenye kuidharau dini, na iliwazuia adui za ukweli wasiidhihaki kazi ya Mungu kwa kuuchekelea ujinga wa wakili wake. Wycliffe alipohitimu katika mafundisho ya skuli, alianza kujifunza mambo yaliyomo ndani ya Biblia. Katika Biblia alipata mafundisho ambayo alikuwa ameyatafuta muda mrefu asiyapate. Humo katika Biblia aliona ya kwamba azimio la wokovu lilifunuliwa, na Kristo alionyeshwa kuwa mpatanishi wa pekee wa wanadamu. Aliona kwamba Kanisa la Kirumi lilikuwa limeacha njia za Biblia na kuyafuata mapokeo ya kibinadamu.

Kazi kubwa zaidi aliyoifanya katika maisha yake ilikuwa kuifasiri Biblia katika lugha ya Kiingereza. Tafsiri lake la Biblia ndilo lililokuwa la kwanza la Kiingereza lililokamilika tangu awali. Kwa jinsi ambavyo kazi ya kupiga chapa ilikuwa haijajulikana, ilichukua muda mrefu na kazi ngumu kuandika vitabu vingi; walakini, kazi hii ikafanywa, na watu wa Uingereza waliipata Biblia katika lugha yao wenyewe. Hivyo ndivyo nuru ya Neno la Mungu ilivyoanza kuangaza giza nene. Mkono wa Mungu ulikuwa ukitayarisha njia kwa Matengenezo Makubwa.

Kuwavuta watu kutumia akili zao juu ya mambo ya dini kuliwaamsha wasikubali bila kufikiri wenyewe masharti yaliyotolewa na askofu mkuu wa Kirumi. Biblia ilipokewa kwa furaha na watu wenye cheo, ambao tu ndio waliokuwa wenye elimu katika zamani zile. Wycliffe alianza kufundisha mafundisho halisi ya Uprotestanti—yaani wokovu upatikanao kwa kumwamini Kristo tu, na ya kwamba Maandiko Matakatifu ndiyo maandiko peke yake yasiyoweza kukosa. Makasisi wengi waliungana naye katika kuzieneza Biblia, na kuihubiri injili; na mafundisho haya, pamoja na maandiko ya Wycliffe yalikuwa na nguvu sana, hata

karibu nusu ya watu wa Uingereza waliikubali imani mpya hii. Ufalme wa giza ulitetemeka.

Jitihadi zote zilizofanywa na adui za Wycliffe ili kuikomesha kazi yake na kuharibu maisha yake, yote hazikufaulu, na alipokuwa na umri wa miaka sitini na moja, akafariki kwa amani katika kazi ya Mungu.

### *Kuenea kwa Matengenezo*

Kwa ajili ya maandiko ya Wycliffe, John Huss, mwenyeji wa Bohemia, alikata shauri kuyakataa mafundisho ya Kirumi, yasiyo ya kweli akajiunga katika kazi ya matengenezo. Huss pia alikuwa Mkristo mashuhuri kama Wycliffe, tena alikuwa mtu aliyeelimika sana, na mwenye nia ya kujitoa kwa ukweli wa Mungu bila kurudi nyuma. Watu wengi waliamshwa moyo na mafundisho yake yaliyoshikamana na Biblia, na kwa jinsi alivyowashitaki makasisi juu ya maisha yao ya kuchukiza na ya ufisadi, na watu maelfu wakafurahi kuyafuata yale mafundisho mapya yaliyokuwa safi na yenye haki. Jambo hili liliwaghadhabisha sana Papa na maaskofu, makasisi na watauwa (monks), tena Huss aliitwa mbele ya Baraza Kuu ya Constance (*Council of Constance*) apate kuhukumiwa kwa ajili ya uzushi. Alipewa hati ya kusafiri salama na mfalme wa Ugermani, na alipofika katika mji wa Constance aliahidiwa na Papa mwenyewe ya kwamba hatadhulumiwa katika hukumu.

Baada ya kesi yake kusikizwa kwa siku nyingi, naye akishikilia ukweli, Huss aliambiwa achague kuyakana mafundisho yake au kuuawa. Alichagua kufa kama shahidi wa Mungu, na alipokwisha kuona vitabu vyake vikiteketezwa katika moto, yeye naye akaunguzwa pale pale. Mbele ya

wakuu wa kanisa na serikali, mtumishi wa Mungu alikanusha kabisa machafuko ya utawala wa makasisi. Kuuawa kwake kinyume cha ahadi kuu iliyotolewa kwake kwa wazi mbele ya watu wote, ya kama atalindwa salama, kuliwadhihirishia walimwengu wote ukatili na uhaini wa Rumi. Wale adui za ukweli, ingawa hawakujua hivyo, kwa kweli walikuwa wakiendesha mbele kazi ya Mungu ambayo walijaribu kuiharibu wasifaulu.

Ijapokuwa mateso yaliendelea vikali, walikuwako watu ambao kwa upole, kwa bidii, na kwa ustahimilivu waliendelea kuudakuliza uovu na upotovu wa mafundisho ya dini, hata baada ya kufa kwa Wycliffe. Watu wengi walitoa mali zao za kidunia kwa kuiendesha kazi ya Kristo kama ilivyokuwa katika siku za mitume.

Jitahidi nyingi sana zilifanywa ili kuongeza nguvu na kuieneza mamlaka ya Kanisa la Kirumi, lakini ingawa maaskofu wakuu waliendelea kujidai ya kwamba ni wajumbe wa Kristo, maisha yao yalikuwa mabaya hata kuwachukiza watu. Kwa ajili ya uvumbuzi wa mtambo wa kupiga chapa, Maandiko Matakatifu yalizidi kuenea mahali pengi, na watu wengi walianza kuona ya kwamba mafundisho ya Kanisa la Kirumi hayakutegemezwa na Neno la Mungu.

Shahidi mmoja alipozimishwa ndipo mwingine aliposimama na kwa ushujaa mkuu akaitangaza kweli. Vita vilianzishwa ambavyo matokeo yake yalikuwa uhuru, si wa watu mmoja mmoja, au kwa makanisa tu, bali uhuru wa mataifa. Ilikuwa kama watu walinyosha mikono yao kuishika ile kweli ya wale waaminifu wa siku za Wycliffe zamani ya miaka mia moja. Martin Luther alianzisha Matengenezo ya Kanisa katika Ugermani: Calvin alikuwa akiihubiri

injili katika Ufransa, na Zwingle alikuwa akihubiri katika Switzerland. Dunia iliamshwa kutoka katika usingizi wa kiroho uliokuwa ukiishika tangu karne nyingi, na katika kila nchi maneno haya yalisikika, "Uhuru wa kila mtu kuabudu apendavyo."





# JINSI LUTHER ALIVYOLETA MATENGENEZO MAKUBWA

KATI ya wale walioitwa kuliongoza kanisa kutoka katika giza ya mafundisho ya Kanisa la Kirumi wapate kuingia katika nuru na imani ya kweli, yule wa kwanza alikuwa Martin Luther. Alikuwa mwenye bidii na nguvu, mwenye kushika kazi kwa moyo, asiyemwogopa mtu ye yote ila Mungu tu, na asiyekubali msingi wo wote wa dini, isipokuwa Maandiko Matakatifu tu, Luther alikuwa mtu aliyefaa kabisa kuishi katika siku zile: Mungu alimtumia kwa kazi kubwa zaidi, yaani kazi ya kufanya matengenezo ya kanisa na kuleta mwanga katika dunia nzima.

Siku moja, alikuwa akitazama vitabu katika chuo kikuu, Luther alipata Biblia ya Kilatini. Mpaka hapo alikuwa amesikia sehemu za Injili na Nyaraka zikisomwa katika mikutano ya ibada, akafikiri ya kwamba Neno la Mungu ndilo vitabu vile tu. Sasa alipata kuona Biblia nzima mara ya kwanza. Aliyafungua makaratasi ya Biblia kwa kicho, akastaajabu sana, alijisomea mwenyewe maneno ya uzima kwa haraka na moyo unaopigapiga, akitulia kidogo pengine, akisema, "Laiti Mungu anipe kitabu cha namna hiki kiwe changu mwenyewe!" Malaika za mbinguni walikuwa karibu naye, na nuru itokayo katika kiti cha enzi cha Mungu ilimfunulia mambo ya ajabu katika Biblia. Tangu zamani alikuwa akiogopa kumkosea Mungu, lakini wakati huo

aliguswa zaidi moyoni akafahamu hali yake ya kuwa mwenye dhambi kwa namna asivyofahamu zamani. Alikuwa na hamu ya kuwekwa huru na dhambi na kufanya upatanisho na Mungu, na hali hiyo ilimwongoza hata akaingia katika nyumba ya watauwa akajitoa kuishi maisha ya utauwa pamoja na "monks" (ambao ni watu wajitengao na mambo ya dunia, ili wajifunge kwa mambo ya dini).

Kila siku alipopata nafasi kidogo ya kupumzika, alitumia nafasi ile kwa kusoma, akijinyima usingizi, na pengine saa zake za chakula. Zaidi ya mambo yote alipenda kujifunza Neno la Mungu. Alipata Biblia ikifungwa na minyororo juu ya ukuta katika nyumba ile, na alijitahidi kuisoma mara kwa mara.

Luther alitiliwa mikono kuwa kasisi, na akaitwa aondoke katika nyumba ile ya utauwa aishike kazi ya ualimu katika Chuo Kikuu cha Wittenbeg (yaani University). Hapo alianza kujifunza Maandiko Matakatifu katika lugha zilizoandikwa mwanzoni. Alianza kuwahutubia wanafunzi juu ya Biblia; na kitabu cha Zaburi, vitabu vya Injili, na Nyaraka zilifunuliwa na kuelezwa mbele ya makutano ya wasikilizaji waliopendezwa. Alikuwa hodari katika Maandiko Matakatifu, na neema ya Mungu ilimkalia. Ufasaha wa maneno yake uliwavuta sana wasikilizaji wake, akili timamu na uwezo wake wa kuuhubiri ukweli uliwasadikisha kabisa, na nguvu ya usemi wake iliwagusa mioyo.

### *Alikuwa Mtangulizi Katika Matengenezo*

Kwa maongozi ya Mungu, Luther alikusudia kuzuru Rumi. Kuachiwa kosa (*indulgence*) kulikuwa kumeahidiwa na Papa kwa wote ambao wangepanda kwa magoti ngazi ile iliyoitwa *"Pilate's Staircase."* Siku moja, Luther alipo-

kuwa akitimiza tendo hilo la kutembea kwa magoti, mara akasikia sauti kama sauti ya ngurumo ikimwambia hivi, "Mwenye haki ataishi kwa imani!" Kwa aibu na woga, akasimama mara, akatoka hima pale alipofanya tendo lile la upuzi. Hakuyasahau kamwe maneno ya fungu lile. Tangu wakati ule alifahamu zaidi udanganyifu wa kuamini kazi za kibinadamu kwa kuleta wokovu, na haja ya kuamini daima juu ya wema wa Kristo. Macho yake yalikuwa yamefumbuliwa, na hayakuweza kufumbwa tena asiyafahamu madanganyifu mabaya ya mafundisho ya Kanisa la Kirumi. Alipogeuza uso wake kutoka kwa mji wa Rumi arudi Ugermani, moyo wake pia ulikuwa umeanza kugeuka kutoka kwa kanisa la Rumi. Tangu wakati ule utengano ule ulizidi kuongezeka, mpaka akatengana kabisa na kanisa la Kirumi.

Baada ya kurudi kwake kutoka Rumi, Luther alipata daraja ya kuwa Mtaalam wa Biblia (*Doctor of Divinity*) katika kile Chuo Kikuu cha Wittenberg. Sasa alikuwa na nafasi ya kujitoa kabisa, zaidi ya zamani, kwa Maandiko Mtakatifu aliyoyapenda. Alikuwa ameweka nadhiri kusoma kwa uangalifu, na kulihubiri Neno la Mungu hasa, lisilochanganywa na maneno ya mapapa, kwa juhudi katika siku zote za maisha yake. Hakuwa tena kama "monk" wa kawaida, au mwalimu mkuu wa kawaida, bali akawa mwalimu mkuu wa Biblia. Alikuwa ameitwa kuwa mchunga kwa kuwalisha watu wa kundi la Mungu ambao walikuwa na njaa ya kusikia Neno la kweli. Alitangaza kwa uthabiti ya kwamba haiwapasi Wakristo kuyapokea mafundisho mengine zaidi ya yale yaliyoandikwa katika Maandiko Matakatifu. Maneno haya yalishambulia kabisa mafundisho ya utawala wa mapapa. Yalikuwa maneno yaliyoonekana kuwa asili kabisa ya Matengenezo ya dini.

Luther alianza kwa ujasiri kujionyesha ya kwamba yeye ni mtetezi wa ukweli. Aliposimama kwenye mimbara, sauti yake ilisikika ikitoa maonyo makuu na ya ajabu. Aliwaambia watu jinsi dhambi inavyomchukiza Mungu, na akawafundisha ya kwamba haiwezekani kwa mwanadamu, kwa matendo yake mwenyewe, kupunguza makosa wala kuepukana na adhabu ya dhambi. Hakuna kitu cho chote kinachoweza kumwokoa mwenye dhambi isipokuwa kutubu na kumwamini Kristo. Neema ya Kristo haiwezi kununuliwa; hutolewa bure pasipo gharama. Luther aliwashauri watu wasinunue vyeti vya kuachiliwa dhambi (*indulgence*), lakini kwa imani wamtazamie Mwokozi aliyesulibiwa. Alisimulia jinsi alivyopata uchungu na maumivu maishani mwake, alipojidhilisha na kufanya mambo yaliyokuwa kama adhabu ya makosa yake, mambo ambayo yalikuwa bure kwa kujipasisha wokovu; tena aliwahakikishia wasikilizaji wake ya kwamba alipata amani na furaha kwa vile alivyoacha kujitegemea mwenyewe na kumwamini Kristo peke yake.

Mafundisho ya Luther yaliwavuta wengi walioelimika katika nchi yote ya Ugermani. Mafundisho na mahubiri yake yalileta mwanga uliowaamsha na kumulika roho za watu maelfu. Imani kuu ilianza kuingia badala ya urafiki uliokuwa umeenea kanisani kwa miaka mingi. Kila mara watu walikuwa wakipoteza tumaini lao juu ya mambo ya ushirikina ya Kirumi. Nia ya kuchukia mambo yo yote yasiyotoka kwa papa, ilianza kupungua. Neno la Mungu, ambalo kwalo Luther alitegemeza mafundisho yake yote na madai yake yote, lilikuwa upanga ukatao kuwili, likiikata mioyo ya watu. Kila mahali kulikuwa na hamu ya maendeleo katika mambo ya kiroho. Po pote palikuwa na

njaa na kiu ya haki kwa namna isivyokuwa katika vizazi vingi tangu zamani. Watu, ambao kwa miaka mingi walikuwa wakiongozwa kutumaini ibada na kawaida za kibinadamu na wapatanishi wa kibinadamu, wakaanza kugeuka na kutubu na kumwamini Kristo aliyesulibiwa.

Maandiko na mafundisho ya yule Mtengenezaji yalikuwa yakienea katika mataifa yote walio Wakristo. Kazi yake ikaenea mpaka nchi za Switzerland na Holland. Katika Uingereza mafundisho yake yalipokewa na kukubaliwa kuwa ni maneno ya uhai. Ukweli ukaenea pia hata nchi za Belgium na Italia. Watu maelfu walikuwa kama watu walioamka kutoka hali ya kuzimia na kupata furaha na tumaini kwa kuishi maisha ya imani kwa Mungu.

*Luther Ajitenga na Rumi*

Kanisa la Kirumi lilifikiri kumwua Luther, lakini Mungu alimlinda. Mafundisho yake yalienea pote—katika nyumba za watauwa, katika nyumba za watu, katika ngome za watu mashuhuri, katika vyuo vikuu, katika majumba ya kifalme; na watu mashuhuri waliondoka kila upande ili wamsaidie.

Katika barua yake aliyomwandikia mtawala na wakuu wa Ugermani juu ya Matengenezo ya Ukristo, Luther aliandika hivi juu ya Papa: "Ni jambo la kuchukiza sana kumwona mtu anayejiita mjumbe atawalaye mahali pake Kristo, akifanya fahari ambayo hakuna mtawala anayeweza kufanya kufanana nayo. Je, hii maana yake ni kuwa kama maskini Yesu, au mnyenyekevu Petro? Wanadai wakisema ya kwamba yeye ni bwana-wa dunia! Lakini Kristo, ambaye Papa anajidai kwamba yeye ni mjumbe wake, alisema hivi, 'Ufalme wangu si wa dunia hii.' Je, mamlaka

ya mjumbe inaweza kunena zaidi ya mkubwa wake?"

Aliandika hivi juu ya vyuo vikuu: "Ninaogopa sana ya kwamba vyuo vikuu vitakuwa milango mikubwa ya jehanum, visipofanya juhudi sana katika kueleza Maandiko Matakatifu, na kuyaimarisha mioyoni mwa vijana. Natoa shauri ya kwamba mtu ye yote asimpeleke mtoto wake katika skuli ambapo Biblia haifundishwi kama somo kuu. Kila skuli ambapo watu hawashughuliki kila mara na Neno la Mungu haina budi kupotoka kabisa."

Maneno haya yalienezwa pote katika Ugermani, na yakawa na nguvu sana kwa kuvuta mioyo ya watu. Taifa lile lote liliamshwa na kushindania lile jambo la matengenezo. Adui za Luther, walikuwa na hamu kuu ya kulipa kisasi, tena walimshurutisha Papa amfanyie mashauri makali. Amri ilitolewa ili mafundisho yake yakatazwe kabisa. Luther na wafuasi wake walipewa siku sitini wapate kugeuka, na wakikataa, basi wao wote wataharimishwa kanisani.

Tangazo la Papa lilipomfikia Luther, alisema hivi: "Ninaidharau sana amri hiyo, tena nitaishambulia, kwani haimstahi Mungu, ni ya uongo . . . Kristo mwenyewe amehukumiwa katika amri hiyo. . . . Nafurahi kuyachukua mabaya ya namna hii kwa ajili ya kazi iliyo bora, yaani ya Mungu. Naona uhuru mkuu sana moyoni mwangu; kuwa sasa nimetambua ya kwamba Papa ni yule mwongo aliyempinga Kristo; na ya kwamba kiti chake cha enzi ni kiti cha Shetani mwenyewe."

Lakini neno la askofu mkubwa wa Rumi bado lilikuwa na nguvu. Alitumia gereza, ukatili, na upanga kama silaha zilizotumiwa kwa kuwatiisha watu. Kila jambo lililotendeka lilikuwa kana kwamba kazi ya Luther ilikaribia kukome-

shwa. Wadhaifu na wenye hofu walitetemeka mbele ya amri ya Papa, na ingawa katika mahali pengi watu walishiriki katika maono ya Luther, watu wengi waliona ya kwamba haifai kujihatarisha maisha kwa ajili ya kutengeneza kwa upya mambo ya kanisa.



SURA YA TANO

# MAENDELEO YA MATENGENEZO YA DINI

MFALME mwingine, aitwaye Charles wa Tano, alifanywa mfalme wa Ugermani, na wajumbe wa Rumi walienda upesi kumpelekea barua za sifa, wakitaka kumshawishi yule mfalme atumie uwezo wake kwa kushindana na wale waongozi wa Matengenezo ya dini. Lakini liwali mmoja, Elector wa Saxony, ambaye alimsaidia Charles kuwekwa kuwa mfalme, alishauri asifanye jambo lo lote la kumdhuru Luther mpaka atakapomwita katika baraza.

Jamia za watu wa Udachi walitazamia baraza kuu la majimbo yote iliyokuwa karibu kukutanika katika mji wa Worms muda kitambo baada ya kutawazwa kwa Charles kuwa mfalme. Kulikuwa na mambo makuu yaliyohusika na utawala wa nchi, ambayo yalipaswa kufikiriwa na baraza hii kuu ya nchi; lakini mambo haya yote yalionekana kwamba hayana maana sana yakilinganishwa na kazi ya yule mtauwa shujaa wa Wittenberg.

Mara ya kwanza Charles alikuwa amemwambia yule elector wa Saxony amlete Luther katika ile Baraza kuu, akimhakikishia ya kwamba Luther atalindwa na matendo yote ya jeuri, na ya kwamba atakubaliwa kupewa mtaalamu fulani awezaye kujadiliana naye juu ya mambo makuu

hasa yaliyoleta mabishano. Luther mwenyewe alikuwa na hamu ya kuonekana mbele ya mfalme.

Rafiki za Luther waliogopa na kushangaa. Kwa jinsi walivyojua chuki na uadui wa watu wale juu yake Luther, waliogopa ya kwamba isingeheshimiwa ile hati ya kusafiri salama, na walimshauri ili asijihatarishe maisha yake. Alijibu hivi: "Wajumbe wa Papa hawataki nifike Worms, lakini wanataka nihukumiwe na kuuawa. Lakini haidhuru. Msiniombee mimi, bali liombeeni Neno la Mungu."

*Luther Mbele ya Baraza*

Hatimaye Luther alisimama mbele ya baraza. Mfalme aliketi juu ya kiti cha enzi. Alizungukwa na watu mashuhuri sana katika ufalme wake. Hakuna mtu ye yote aliyekuwa amesimama mbele ya baraza kuu ya kushangaza kama ile ambayo Luther alisimama mbele yake ili kuitetea imani yake.

Kuonekana kwake hivi mbele ya baraza kulikuwa dalili ya ushindi wa ukweli wa Mungu. Mtu ambaye alikuwa amehukumiwa tayari na Papa, tena kuanza kuhukumiwa na baraza nyingine, jambo hilo lilionekana kana kwamba utawala wa juu wa Papa unaanza kupunguka. Mtengenezaji Luther, baada ya kulaaniwa, na kuharamishwa kanisani na Papa, aliahidiwa ya kwamba atalindwa, na kusikizwa mbele ya baraza ya wakuu wa taifa. Amri ilikuwa imetoka Rumi kumkataza asinene tena, lakini sasa alikuwa amepewa nafasi ya kuhutubu mbele ya maelfu ya watu waliotoka katika nchi zote za Kikristo. Kwa utulivu na upole, lakini kwa ushujaa na usharifu, alisimama kama shahidi wa Mungu mbele ya wakuu wa dunia. Luther ali-

yajibu maswali yao kwa sauti ya upole na unyenyekevu, pasipo hasira wala haraka. Hali yake ilikuwa ya heshima, na hakuegemea nguvu zake mwenyewe; walakini alionyesha matumaini na furaha iliyowashangaza watu waliohudhuria katika baraza ile.

Wale waliokataa kuipokea nuru kwa ajili ya ukaidi tu, na kukaza nia zao wasiikubali kweli, walikasirishwa na nguvu ya maneno ya Luther. Alipomaliza maneno yake, mwenye kiti katika baraza akamjibu kwa hasira akisema, "Hukujibu swali maalum uliloulizwa. . . Inatakiwa utoe jibu lililo fupi na lenye maana. . . Je, utakubali, au hutakubali kuikanusha imani yako?"

Mtengenezaji akajibu akisema: "Kwa jinsi wewe mfalme mtukufu na ninyi wakuu wa milki mnavyotaka kwangu jibu lililo safi, fupi, na lenye maana, nitawapeni jibu moja, nalo ni hili: Siwezi kuacha imani yangu kwa ajili ya Papa wala baraza, kwa kuwa imeonekana dhahiri ya kwamba mara nyingi wamekosa, na mafundisho yao hayapatani. Kwa hivyo basi, nisiposadikishwa na Maandiko Matakatifu ama na majadiliano yaliyo dhahiri kabisa, nisiposhurutishwa na mafungu ambayo nimeyatoa, na yasiponionyesha moyoni ya kwamba nimefarakana na Neno la Mungu. *sitaikana imani yangu kamwe, wala siwezi kufanya hivyo*, kwa kuwa Mkristo anajihatarisha kama akiyakiri mambo yafarakanayo na dhamiri yake. Hapa nimesimama, siwezi kugeuka; Mungu na anisaidie. Amina."

Hivyo ndivyo alivyosimama huyu mtu wa haki, akisimama imara kabisa juu ya msingi imara wa Neno la Mungu. Nuru ya mbinguni iliangaza usoni pake. Ukuu wake na tabia iliyo safi, amani na furaha aliyokuwa nayo moyoni mwake, zilionekana mbele ya wote alipokanusha mamlaka

ya uongo na kushuhudia ukuu wa imani ile ishindayo ulimwengu.

Alisimama imara kama mwamba, wakati mawimbi makali ya uwezo wa dunia yalipompiga huko na huko yasimdhuru. Nguvu iliyokuwa katika maneno yake, jinsi alivyosimama bila hofu, macho yake yaliyong'aa na kuonyesha amani yake, na uthabiti wake usiogeuka ulioonekana katika kila neno na tendo lake, ziliwashangaza sana wakuu wa baraza. Ilionekana dhahiri ya kwamba hakuweza kushawishwa kwa ahadi wala vitisho, ili ainame mbele ya mamlaka ya Rumi.

Kristo ndiye aliyenena katika ushuhuda wa Luther kwa nguvu na ufasaha, hata maneno yake yakawachoma moyo na kuwashangaza rafiki zake pamoja na adui zake pia. Roho wa Mungu alikuwako katika baraza ile, akigusa mioyo ya wakuu wa dola. Wengine kati ya wale wakuu walikiri dhahiri ya kwamba jambo la Luther lilikuwa jambo la haki kabisa. Wengi walisadikishwa na ukweli wa maneno yake, lakini kwa wengine maono yao hayakudumu sana Kulikuwako na watu wengine pia ambao wakati ule hawakuonyesha ya kwamba waliyasadiki mambo yale; lakini baada ya kujisomea wenyewe Maandiko Matakatifu, katika siku za baadaye kwa ushujaa walitetea Matengenezo ya dini.

Yule elector Frederick wa Saxony alitazamia mambo ya baraza ile kwa wasiwasi naye alisikiliza hotuba yake Luther kwa kushtuka sana moyoni. Alifurahia ushujaa, uthabiti na ukavu wa macho wa yule mtauwa maarufu, naye alifurahia kuwa mtetezi na mlinzi wake. Elector Frederick alipolinganisha wale waliotetana, aliona ya kwamba utetezi wa Luther ulikuwa na nguvu zaidi, na aliona ya kwamba

akili ya Papa, ya wafalme na ya maaskofu ilishindwa kabisa na ukweli alioshuhudia Luther. Ilikuwa ya kwamba utawala wa Kanisa la Kirumi umeshindwa kwa namna ambavyo matokeo yake yangeenea kwa mataifa yote na kwa vizazi vyote vya baadaye.

Kama Luther angalishindwa katika jambo moja tu, Shetani na malaika zake wangalipata ushindi. Lakini uthabiti wake na jinsi alivyosimama imara bila kusitasita, ulikuwa njia ya kuleta uhuru kanisani, na huo ndio mwanzo wa wakati mpya wa amani. Mvuto wa mtu huyu mmoja, ambaye alithubutu kusimama peke yake kwa maoni yake juu ya mambo yanayohusu dini, ulikuwa na nguvu ya kugeuza hali ya kanisa na dunia pia, wala si katika siku za maisha yake tu, bali katika vizazi vya baadaye pia. Uthabiti wake na uaminifu wake ungewatia watu nguvu mpaka mwisho wa dunia, yaani wote watakaopata mateso kama yale. Uwezo na utukufu wa Mungu ulidhihirika ya kwamba unashinda mashauri ya wanadamu, hata na uwezo mkuu wa Shetani pia.

Naliona ya kwamba Luther alikuwa shujaa, mwenye juhudi, mwenye macho makavu, mtu asiye na woga kwa kuikaripia dhambi na kuitetea haki. Hakuwaogopa waovu wala mashetani: alijua ya kwamba pamoja naye alikuwa Mmoja aliye na nguvu zaidi ya wote. Luther alikuwa na juhudi, ushujaa, na uthabiti, na mara zingine alikuwa katika hatari ya kufanya ujasiri kupita kiasi. Lakini Mungu alimwinulia Melancthon, ambaye alikuwa na tabia iliyo mbali na ile ya Luther, apate kumsaidia katika kuiendesha kazi ya Matengenezo ya kanisa. Melancthon alikuwa mwoga, mwenye kuwa na hadhari, mwangalifu na mvumilivu. Alikuwa mpendwa sana wa Mungu. Alikuwa na ujuzi sana

kwa Maandiko Matakatifu, tena alikuwa mwenye busara sana kwa kukata mashauri. Upendo wake kwa kazi ya Mungu ulikuwa sawa na ule wa Luther. Bwana Mungu aliiunganisha pamoja mioyo ya watu hawa; walikuwa rafiki wasiotengana. Luther alimsaidia sana Melancthon alipokuwa katika hatari ya kuonyesha woga na upole zaidi na kwa upande wake Melancthon alimsaidia sana Luther alipokuwa katika hatari ya kuharakisha mambo kupita kiasi.

Busara na uangalifu wa Melancthon uliwawezesha kuepuka matata ambayo yangalitokea juu ya kazi ya Mungu kama kazi ingalikuwa mkononi mwa Luther peke yake; na mara nyingi kazi isingaliendelezwa vizuri kama ingaliachwa kwa Melancthon peke yake. Nalionyeshwa hekima ya Mungu katika kuwachagua watu hawa wawili kuiendesha kazi hii ya Matengenezo.

### *Uingereza na Scotland Zapata Nuru*

Siku zile Luther alipokuwa akiwafungulia watu wa Ugermani Biblia ambayo ilikuwa imefungwa, Tyndale alivutwa na Roho wa Mungu kufanya vile kwa Uingereza. Alikuwa mwanafunzi wa Biblia mwenye bidii sana, na kwa ushujaa sana aliyahubiri mambo yote aliyosadikishwa kwamba ni ya kweli, akisema ya kwamba mafundisho yote yapate kuthibitika kwanza na Neno la Mungu. Juhudi yake haikuwa na budi kuleta ushindani kati yake na wafuasi wa Papa Mtaalamu fulani Mkatoliki aliyekuwa akishandana naye alisema hivi: "Laiti kama tungeishi bila sheria ya Mungu zaidi ya kukosa kuwa na amri za Papa." Tyndale alimjibu akisema, "Namdharau sana Papa na amri zake zote; na Mungu akinihifadhi maisha, baada ya miaka si mingi nita-

mfanya kijana afanyaye kazi ya ukulima ayajue Maandiko Matakatifu kuliko uyajuavyo wewe."

Kusudi aliloanza kuliweka moyoni, yaani kusudi la kuwapa watu Agano Jipya katika lugha yao wenyewe, sasa lilithibitika, na punde si punde alijitia katika kazi hiyo. Ilionekana ya kwamba alifungiwa pote katika Uingereza, naye aliona ni vema akimbilie Ugermani. Hapo akaanza kulichapa Agano Jipya katika Kiingereza. Baada ya muda si mrefu nakili elfu tatu za vitabu vya Agano Jipya vikamalizika, na katika mwaka ule ule, ikachapwa jumla ya nakili nyingine tena.

Hatimaye aliishuhudia imani yake kwa kuuawa, lakini silaha alizozitayarisha zimewawezesha askari wengine wa msalaba kupigana kwa karne nyingi mpaka siku hizi.

Shujaa aliyepatikana kwa kuitetea Injili katika nchi ya Scotland aliitwa John Knox. Mtu huyu wa haki hakumwogopa ye yote. Mioto ya mateso iliyowaka pande zake zote haikumtia hofu, bali ilizidi kumwongeza juhudi. Ingawa alikuwa katika hatari ya kuuawa alisimama imara, akijitahidi kwa uwezo wake wote apate kuiharibu ibada ya sanamu. Hivyo alishikilia kusudi lake, akipigana vita vya mwenyewe. Kila mfalme, mtawala, mwanasheria au mkuu Bwana, mpaka Scotland ikawa huru.

Katika Uingereza kulikuwa na mtu aitwaye Latimer, aliyehubiri kwenye mimbara akisema ya kwamba Biblia inapasa kusomwa katika lugha ya watu wenyewe. Alisema ya kwamba Mwenye kuanzisha Maandiko Matakatifu "ndiye Mungu mwenyewe;" na haya Maandiko Matakatifu yana nguvu na uwezo wa kuishi milele kama alivyo Mungu mwenyewe. Kila mfalme, mtawala, mwanasheria au mkuu ye yote hana budi kulitii Neno takatifu la Mungu. "Tusi-

ifuate njia yo yote nyingine, bali Neno la Mungu na lituongoze; tusifuate njia za babu zetu, wala tusiyafuate matendo yao, lakini tufuate yale ambayo yaliwapasa kuyafanya."

Barnes na Frith, waliokuwa rafiki waaminifu wa Tyndale, wao pia waliondoka wapate kuutetea ukweli. Watu walioitwa Ridley na Cranmer wakawafuata. Waongozi hawa wa Matengenezo katika Uingereza walikuwa watu walioelimika sana, na wengi wao walikuwa wakiheshimiwa sana kwa ajili ya juhudi yao na maisha ya utauwa katika Kanisa la Kirumi. Uasi wao kwa mamlaka ya Papa. Ujuzi wao juu ya siri za Babeli ulitilia uwezo zaidi kwa ushuhuda wao juu ya Babeli.

Fundisho kuu la akina Tyndale, Frith, Latimer, na Ridley ni ya kwamba maandiko yalitoka kwa Mungu, na ya kwamba ndani yake pana mafundisho yote yafaayo kwa wokovu. Mafundisho yao yalipinga kabisa ile desturi ya mapapa, baraza, makasisi na wafalme na kujitwalia nguvu za kuitawala dhamira ya watu juu ya mambo ya kiroho. Biblia ndiyo iliyokuwa kipeo cha wale watengenezaji, na mafundisho yao na madai yao yote waliyalinganisha na Biblia tu. Imani waliyokuwa nayo kwa Mungu na kwa neno lake ndiyo iliyowahifadhi watakatifu hawa walipoyatoa maisha yao kufa kama mashahidi kwa ajili ya imani ya dini.



# KUSHINDWA KUENDELEA

KAZI ya Matengenezo ya dini haikukoma baada ya kufa kwa Luther, kama wengine wanavyodhani. Kazi hiyo itaendelea mpaka mwisho wa mambo ya dunia hii. Luther alikuwa na kazi kubwa sana kushirikisha wengine nuru aliyopewa na Mungu; walakini hakupokea nuru yote iliyopasa kutolewa kwa walimwengu. Tangu siku zile mpaka sasa, Maandiko Matakatifu yamekuwa yakiangazwa zaidi na zaidi kila mara, na mambo mengine ya ukweli yamekuwa yakizidi kufunuliwa mara kwa mara.

Luther na watenda kazi wenzake walimfanyia Mungu kazi kubwa sana, lakini kwa jinsi wao wenyewe walivyotoka katika Kanisa la Kirumi, tena walikuwa wakiamini na kuyashuhudia mafundisho yake, haikuweza kutazamiwa ya kwamba wangeyatambua makosa haya yote. Ilikuwa kazi yao kuivunja minyororo ya Rumi na kutoa Biblia kwa walimwengu; walakini, kulikuwa na mambo makuu waliyoshindwa kuvumbua, tena makosa makubwa ambayo hawakuyakana. Wengi wao waliendelea kuitunza Jumapili pamoja na siku kuu zingine za Kirumi. Kwa kweli, hawakuitunza Jumapili wakifikiri ya kwamba ilikuwa siku takatifu ya Mungu, hali waliona ya kwamba inafaa kutunzwa kama siku ya kawaida ya ibada. Walakini, kulikuwa na wengine

kati yao ambao waliiheshimu Sabato ya amri ya nne. Kati ya wale watengenezaji wa dini, inatupasa kuwaheshimu wale ambao walishuhudia kweli ambayo ilikuwa imedharauliwa, hata na Maprotestanti—yaani wale walioshikilia uthabiti wa amri ya nne na sharti ya Sabato ya Biblia. Matengenezo yalipofukuza mbali giza iliyokuwa imefunika nchi zote za Kikristo, watunza Sabato walipata kubainishwa katika nchi nyingi.

Wale waliopata mibaraka mikubwa ya Matengenezo hawakuendelea mbele katika njia ile iliyofuatwa na Luther. Watu wachache waaminifu walitokea mara kwa mara kuyahubiri mambo mapya ya ukweli, na kuonyesha uongo uliokuzwa tangu zamani, lakini wingi wa watu, sawa na Wayahudi katika siku za Kristo, na wafuasi wa Papa katika siku za Luther, waliridhika wakaendelea kufuata mafundisho ya baba zao, na kuishi jinsi baba zao walivyoishi. Kwa hivyo dini ilianza kurudi nyuma kwa unafiki; makosa yalianza kukuzwa, pamoja na matendo yanayofuatana na kuamini mambo ya ushirikina, ambayo yangalitupwa mbali kama kanisa lingaliendelea kuenenda katika nuru ya Neno la Mungu. Hivi roho ile iliyoamshwa na Matengenezo ya dini, ilianza kufifia, mpaka Matengenezo makubwa yakahitajiwa katika makanisa ya Maprotestanti kama yalivyohitaji mwanzoni katika Kanisa la Kirumi katika siku za Luther. Kulikuwa na hali ya kuzimia maisha ya kiroho, na kuyakubali maoni ya wanadamu, hali ya kuipenda dunia, na kuyakubali mafundisho ya kibinadamu badala ya mafundisho ya Neno la Mungu. Kiburi na upotovu wa mali ulikuzwa kwa kuzifunika na kawaida za dini. Makanisa yaliingia katika upotovu kwa kushirikiana na dunia. Hivi mafundisho makuu yakashushwa ambayo kwa ajili

yake Luther na watenda kazi wenzake walikuwa wametaabika sana.

Shetani alipoona ya kwamba alishindwa kuivunja kabisa nguvu ya ukweli kwa njia ya mateso, alirudia tena azimio la mapatano ambalo mwanzoni lilileta uasi mkuu na kuanzishwa kwa kanisa la Kirumi. Aliwashawishi Wakristo wafanye urafiki, siyo sasa na wale washenzi, bali na wale ambao, kwa njia ya kumwabudu mungu wa dunia hii, wamejionyesha kweli ya kwamba ni waabuduo sanamu.

Shetani hakuweza kuwanyima watu Biblia:kwa kuwa Biblia iliweza kununuliwa na watu wote. Lakini aliwadanganya watu maelfu wapate kuyakubali maelezo yake yasiyo ya kweli na mafundisho ya uongo, wasipochunguza Maandiko wao wenyewe ili wapate kujifunza ukweli. Shetani alikuwa ameyachafua mafundisho ya Biblia, na mazoea yalianza kuingia ambayo yangewaharibu watu milioni nyingi. Kanisa lilikuwa likiyashika na kuyatetea mazoea haya, badala ya kuishindania imani waliyokabidhiwa watakatifu siku za kale. Na bila kujua hali yao na hatari yao, kanisa na watu wa dunia walikuwa wakikaribia wakati wa maana sana katika historia ya dunia—wakati atakapofunuliwa Mwana wa Adamu.

SURA YA SABA

# UJUMBE WA MALAIKA WA KWANZA

UNABII wa ujumbe wa malaika wa kwanza, ulioandikwa katika Ufunuo 14, ulitimizwa katika miaka ya 1840-44, watu walipokuwa wakitazamia kurejea kwa Kristo. Katika nchi za Ulaya na Amerika, watu waliojaa imani na wenye bidii kwa kuomba walivutwa moyoni walipotazamishwa mambo yaliyotabiriwa, na kwa kuyachunguza sana Maandiko Matakatifu walipata maneno yaliyowasadikisha ya kwamba mwisho wa mambo yote ulikuwa umekaribia sana. Roho wa Mungu aliwavuta watenda kazi wa Mungu walitoe onyo lile kwa wengine. Po pote duniani ujumbe huu wa injili ya milele ulienea: "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja." Ufunuo 14:7.

Po pote palipokwisha kuingiliwa na wamishenari, palitangazwa habari njema za kurudi kwa Kristo kulivyokaribia. Katoka nchi mbali mbali kulipatikana jamii za Wakristo ambao, kwa kuyachunguza sana Maandiko, walikuwa wamesadikishwa ya kwamba kurudi kwa Kristo kumekaribia. Katika nchi zingine za Ulaya, ambapo amri zilikuwa kali sana hata zikakataza kuhubiri habari za marejeo ya Yesu, watoto wadogo walitumiwa na Mungu ili waitangaze habari hiyo, na wengi wakasikiliza onyo lile.

William Miller na watenda kazi wenzake ndio walipewa kazi ya kuuhubiri ujumbe huu katika Amerika, na mwanga uliotiwa na kazi zao ulimulika mpaka nchi za mbali. Mungu alimtuma malaika wake auamshe moyo wa mkulima fulani ambaye hakuyaamini mafundisho ya Biblia, apate kuongozwa kuyachunguza maneno ya unabii. Mtu yule maalum alijiwa na malaika mara kwa mara, kumwongoza na kumfungulia maneno ya unabii ambayo tangu zamani yalikuwa mafumbo kabisa kwa watu wa Mungu. Alipewa neno la kwanza katika mfululizo wa ukweli, naye aliongozwa kuendelea kutafuta hatua kwa hatua, mpaka alipopendezwa sana na kushangazwa na Neno la Mungu. Aliona ya kwamba ndani yake kulikuwa mwandamano kamili wa ukweli. Lile Neno la Mungu, ambalo mara ya kwanza alidhani ya kwamba halikuandikwa kwa maongozi ya Mungu, sasa aliweza kuona mwenyewe uzuri na utukufu wake. Aliona ya kwamba sehemu moja ya Maandiko hueleza maana ya sehemu nyingine, na asipoweza kufahamu sehemu fulani aliweza kupata maelezo yake katika sehemu nyingine ya Biblia. Alipendezwa sana na Neno la Mungu, tena aliona ya kwamba linafaa kuheshimiwa na kuangaliwa kwa kicho.

Alipozidi kuchungulia mwandamano wa maneno ya unabii, aliona ya kwamba watu wakaao duniani wanaishi katika siku za mwisho kabisa ya mambo ya dunia hii, wala hawakujua. Aliyatazama makanisa, akaona ya kwamba yalipotoka, watu walikuwa wameacha kumpenda Yesu, wakaanza kuipenda dunia; walikuwa wakitafuta heshima na makuu ya dunia, badala ya kutaka heshima ile itokayo juu; walikuwa wanatamani mali za dunia, badala ya kuweka hazina zao mbinguni. Aliweza kuona unafiki, giza, na

kifo kila mahali. Alichomwa sana moyoni. Mungu alimwita kusudi aliache shamba lake, jinsi alivyomwita Elisha awaache ng'ombe zake na kazi yake apate kumfuata Eliya.

Kwa kicho na kutetemeka, William Miller akaanza kuwafunulia watu siri za ufalme wa Mungu, akiwafundisha wasikilizaji wake habari za unabii tangu zamani mpaka kufika wakati wa marejeo ya Kristo. Ushuhuda ulioandikwa katika Biblia uliowaongoza watu kufikiri ya kwamba Yesu atakuja katika mwaka wa 1843 uliwaamsha watu kila mahali. Wengi walisadiki ya kwamba maneno yaliyoelezwa juu ya nyakati za unabii yalikuwa sawa, na wakaacha kushika mashauri yao wenyewe, wakaupokea ukweli, kwa furaha. Wahubiri wengine waliacha fikara na maoni yao juu ya madhehebu ya dini, wakaacha mishahara yao, wakajiunga pamoja katika kutangaza habari ya kuja kwake Yesu.

Walakini kulikuwa na wahubiri wachache tu, ambao walikuwa tayari kuukubali ujumbe huu; kwa hivyo kazi kubwa iliwekwa mikononi mwa washiriki wanyenyekevu. Wakulima waliyaacha mashamba yao, mafundi wa mashine waliziacha mashine zao, wafanyi biashara waliacha bidhaa zao, wataalamu waliacha shughuli zao; walakini watenda kazi walikuwa wachache sana wakilinganishwa na kazi iliyopasa kufanywa. Hali ya kutomcha Mungu ilivyokuwa Kanisani, na dunia jinsi ilivyo katika hali ya uovu, mambo haya yalilemea roho za watu wa Mungu wenye haki, hao nao walikuwa tayari kufanya kazi kwa nguvu, wakiivumilia dhiki na taabu, kusudi wapate kuwavuta watu waongoke moyo na kupata wokovu. Ingawa kazi ilipingwa sana na Shetani, lakini iliendelea mbele kwa

nguvu, na ukweli wa marejeo ya Yesu ulikubaliwa na watu maelfu.

### *Kuamshwa kwa Mambo ya Mungu*

Po pote palisikiwa ushuhuda uliowaonya wenye dhambi, wayafuatao mambo ya kidunia pamoja na washiriki wa kanisa, wapate kuikimbia ile hasira itakayokuja. Wahubiri walilitia shoka chini ya mti, kama Yohana Mbatizaji aliyemtangulia Kristo, wakawavuta watu wapate kuyazaa matunda yapasayo toba. Mafundisho yao yaliyogusa sana mioyo yalihitilafiana kabisa na ahadi za amani na salama zilizohubiriwa katika makanisa ya kupendeza watu wengi. na po pote ujumbe huu ulipopelekwa, uliamsha mioyo ya watu.

Ushuhuda wa Biblia, uliokuwa dhahiri sana na rahisi kufahamika, na uliochoma mioyo kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, ulikuwa na uwezo mkuu wa kuwasadikisha watu, hata watu wachache tu ndio walioweza kuupinga kabisa. Walimu wakuu wa dini waliamshwa moyo wakafahamu hali yao ya kimoyo jinsi walivyo hatarini. Walifahamu maasi yao, tabia yao ya kuyapenda mambo na anasa za dunia, na kutoamini kwao, kiburi chao na hali yao ya kujipenda nafsi. Wengi walimtafuta Bwana kwa kutubu na kujidhili. Upendo wao uliokuwa umedumu sana juu ya mali za dunia hii uligeuka ukaelekea mbinguni. Roho ya Mungu aliwakalia, na kwa mioyo iliyopondeka na kutulizwa wakajiunga katika kuutangaza ujumbe huu, "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja." Ufunuo 14:7.

Wenye dhambi waliuliza sana kwa machozi wakisema, "Nifanye nini nipate kuokolewa?" Wale ambao maisha

yao hayakuwa ya uaminifu walikuwa na hamu ya kurudisha walivyonyang'anya wengine. Wote waliopokea amani katika Kristo walitaka kuwashirikisha wengine mibaraka hiyo. Mioyo ya wazazi iliwageukia watoto wao, na mioyo ya watoto iliwageukia wazazi wao. Matengano ya kiburi na unyamavu ulitokomelea mbali. Maungamo ya kweli yalitolewa, na watu wa nyumba fulani fulani walikuwa wakiwaombea wapendwa wao wengine kusudi wapate kuokolewa.

Mara nyingi sauti ya maombi ilisikika. Po pote watu walikuwa na maumivu rohoni na kumwomba Mungu. Wengi waliomba usiku kucha kwa kupata tumaini ya kwamba wanasamehewa dhambi zao wenyewe, au wakiomba kwa ajili ya jamaa zao na jirani zao wapate kuongoka. Imani ile kuu iliwafaidia sana. Watu wa Mungu wangaliendelea kuwa wenye juhudi kwa kuomba hivi, kwa kupeleka maombi yao mbele ya kiti cha neema wangekuwa na hali njema ya kiroho zaidi ya ile hali yao ya sasa. Lakini kuomba kumekuwa haba zaidi, hali ya kusadiki hatia ya dhambi huonekana mara chache sana, hali ya kutokuwa na imani huwaondolea wengi ile neema kuu iliyotolewa kwa wingi na Mwokozi wetu mwenye rehema.

Watu wa kila aina walikuja wengi kwa mikutano ya Waadventista. Matajiri na maskini, watu wenye heshima na watu duni, walikuja kwa ajili ya sababu mbali mbali, wakiwa na hamu sana kuyasikia wenyewe mafundisho ya kuja kwa Yesu mara ya pili. Wakati ule ambapo watumishi wa Mungu walikuwa wakieleza sababu ya imani yao, Bwana Mungu mwenyewe aliituliza ile nia ya kushindana. Pengine mjumbe aliweza kuwa mnyonge, lakini Roho ya Mungu alilitilia nguvu Neno lake. Kuwako kwa malaika

watakatifu kulionekana katika mikutano hii, na kila siku waaminio waliongezeka wakawa wengi. Mambo yaliyoonyesha kukaribia kwa marejeo ya Yesu yalipokaririwa, makutano makubwa ya watu walikaa kimya wakiyasikiliza maneno yale mazito. Nyakati zile ilionekana kana kwamba mbingu na dunia zilikaribiana. Uwezo wa Mungu ulionekana juu ya wazee, vijana na watu wazima. Watu walikwenda nyumbani midomo yao ikijaa sifa za Bwana, na kwa utulivu wa siku zilisikika sauti za watu zikishangilia. Hakuna hata mmoja aliyehudhuria mikutano hiyo awezaye kuyasahau maneno mazito waliyoyasikia.

*Ushindani*

Tangazo la wakati maalum wa kuja kwa Kristo lilileta ushindani mkubwa sana toka kwa watu wa kila aina, tangu wahubiri hata wenye dhambi wasiojali jambo lo lote, waliothubutu kumdharau Mungu. "Hakuna mtu ajuaye nyakati wala majira!" Maneno haya yalisikiwa yakisemwa na wahubiri wanafiki pamoja na wenye kudhihaki dini kabisa. Walikataa kuyasikia maelezo yaliyo dhahiri ya fungu hili yaliyotolewa na wale waliokuwa wakiwaonyesha jinsi mwisho wa nyakati zilizotabiriwa na manabii ulivyokaribia, pamoja na utumilizo wa ishara ambazo Kristo mwenyewe alikuwa amezitabiri ya kwamba zitaonyesha kuja kwake mara ya pili jinsi kulivyo karibu.

Wengi wao waliokuwa wakijidai ya kwamba wanampenda Mwokozi wao, walisema ya kwamba hawana neno juu ya mahubiri ya kurejea kwake; lakini hawakukubali uwekwe wakati maalum wa kuja kwake. Mungu ajuaye yote alijua fikara za mioyo yao. Hawakupendezwa na jambo la kuja kwa Kristo ili kuihukumu dunia kwa haki.

Walikuwa wametenda kama watumishi wasio waaminifu, matendo yao hayakustahili kukaguliwa na Mungu ajuaye fikara za mioyoni, hao nao waliogopa kumlaki Bwana wao. Hawakuwa tayari kumkaribisha Kristo kwa furaha, kama vile Wayahudi wasivyokuwa tayari kumpokea wakati wa kuja kwake mara ya kwanza. Shetani na malaika zake walisimanga wakamshutumu Yesu na malaika zake watakatifu, kwa kuwa watu wa Kristo walikuwa wakimpenda kidogo tu, wala hawakuwa na hamu ya kuonekana kwake.

Walinzi wasio waaminifu waliyazuilia maendeleo ya kazi ya Mungu. Watu walipoamshwa mioyoni, na wakaanza kuitafuta sana njia ya wokovu, watangulizi hawa walijiingiza kati yao na ukweli, wakitaka kuutuliza woga wao kwa kueleza vibaya maana ya Neno la Mungu. Shetani na wahubiri wasiojitoa kweli kweli waliungana katika kazi hii na kusema, Amani, amani, ambapo Mungu hakusema neno lo lote juu ya amani. Wengine walikataa kuingia katika ufalme wa Mungu wao mwenyewe, na wale waliokuwa wakitaka kuingia waliwazuia, kama Mafarisayo walivyofanya katika siku za Kristo. Damu ya watu wale waliozuiliwa ufalme wa Mungu itatakiwa juu ya wale waliowazuia.

Po pote ujumbe wa kweli ulipohubiriwa, ulikubaliwa mara ya kwanza na watu wanyenyekevu na waaminifu katika makanisa. Wale waliojisomea Biblia wenyewe, waliweza kutambua ya kwamba maelezo ya maneno ya unabii yaliyokubaliwa na wingi wa watu hayakupatana na maneno ya Biblia. Tena po pote ambapo watu hawakudanganywa na makasisi kwa vile walivyotoa maelezo ya uongo na kupotoa mambo ya dini, po pote walipokuwa wakichunguza Neno la Mungu wao wenyewe, ilitakiwa tu ili fundi-

sho lile juu ya kurejea kwa Kristo lilinganishwe na Maandiko Matakatifu, ndipo lilithibitishwa kwamba ni jambo litokalo kwa Mungu.

Watu wengi waliteswa na wenzao wasioamini. Kulikuwa na watu wengine, ambao kwa kutaka kudumu katika madarasa yao kanisani, walikubali kunyamaza wasiseme neno juu ya tumaini lao; lakini wengine waliona ya kwamba utiifu kwa Mungu ungewazuia wasiyafiche mambo ya kweli waliyokuwa wamekabidhiwa na Mungu. Watu wengi waliharimishwa kanisani kwa ajili ya sababu moja tu, yaani kuikiri imani waliyokuwa nayo juu ya kuja kwa Kristo. Maneno haya ya nabii yalikuwa na thamani kubwa kwa wale waliojaribiwa kwa imani yao: "Ndugu zenu wawachukiao ninyi waliowatupa kwa ajili ya jina langu, wamesema, na atukuzwe Bwana tupate kuiona furaha yenu; lakini watatahayarika." Isaya 66:5.

Malaika za Mungu walichungulia kwa makini sana matokeo ya onyo lile. Wakati ambapo makanisa yalikataa ujumbe, malaika wakawaacha kwa huzuni. Walakini, kulikuwako na wengi katika makanisa ambao walikuwa hawajajaribiwa bado juu ya ukweli ule wa marejeo ya Kristo. Wengi walidanganywa na waume wao, wake zao, wazazi wao au watoto wao, wakasadikishwa ya kwamba ni dhambi hata kuyasikiliza maneno yale ya uzushi yaliyofundishwa na Waadventista, yaani wale waliotazamia kurudi kwa Kristo. Malaika waliambiwa wawalinde watu hawa vizuri; kwa kuwa mwanga mwingine ulikuwa ukiwajia kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu.

### *Kujitayarisha Kumlaki Bwana*

Wale waliokuwa wameupokea ujumbe ule walikesha

kwa hamu kubwa sana wakitazamia kuja kwa Mwokozi wao. Wakati ambapo walikuwa wakitazamia kumlaki Bwana uliwadia. Waliutazamia wakati ule kwa kicho na unyofu wa moyo. Walistareheka katika kuzungumza na Mungu, wakiitazamia amani kuu waliotumaini kupata baadaye katika ufalme wake. Hakuna mtu ye yote kati ya wale walioshiriki tumaini na imani ile aliyeweza kuzisahau nyakati zile za kumngoja Bwana. Shughuli za kawaida za kidunia ziliachwa kwa majuma kadha. Waaminio walijiangalia sana fikara na nia zao kana kwamba walitaka kufa, na ya kwamba baada ya muda kitambo macho yao yatafumbwa wasiyatazame mambo ya dunia tena. Hawakuzitengeneza kanzu za kupaa mbinguni, (kama wengine wasemavyo), lakini wote walikuwa na hamu ya kuthibitisha moyoni ya kwamba walikuwa tayari kumlaki Mwokozi wao, mavazi yao meupe ndiyo usafi wa moyo, tabia iliyotakaswa na dhambi kwa damu ya upatanishi wa Kristo.

Mungu alikusudia kuwajaribu watu wake. Mkono wake ulilifunika kosa fulani katika kuzihesabu nyakati zilizotabiriwa. Wale watu waliokuwa wakimtazamia Bwana hawakulitambua lile kosa, wala adui zao walioelimika sana hawakulitambua. Adui zao walisema hivi: "Hamkukosa hata kidogo katika kuzihesabu nyakati za unabii. Kuna jambo kubwa fulani litakalotokea baada ya siku si nyingi, lakini si jambo lile ambalo William Miller analitabiri; jambo hilo ndilo kuongoka kwa walimwengu wote, wala si kuja kwa Kristo mara ya pili."

Wakati ule wa kumngoja Bwana ulipita, na Kristo hakuonekana kwa kuwaokoa watu wake. Wale ambao walimngojea Mwokozi wao kwa imani na upendo mkuu waliona uchungu mkuu sana. Walakini Bwana alikuwa

amelitimiza kusudi lake: alikuwa amejaribu mioyo ya wale waliojidai ya kwamba walitazamia marejeo yake. Miongoni mwao kulikuwa na wengine ambao walivutwa na woga tu, wala hawakuwa na moyo hasa wa kumtazamia. Ungamo la tumaini lao halikugeuza hali ya mioyo yao wala maisha yao. Tokeo lile kuu lililotazamiwa lilipokosa kutimia, ndipo watu hawa wakasema ya kwamba hawana uchungu moyoni; kwani hawakuamini ya kwamba Kristo atakuja. Wao ndio waliokuwa kati ya watu wa kwanza waliochekelea huzuni ya waaminio wa haki.

Lakini Yesu na malaika wote wa mbinguni waliwaangalia kwa upendo na rehema wale ambao, ingawa walijaribiwa na kuhuzunishwa, walidumu kuwa waaminifu. Kama kitu kinachotenga mambo yanayoonekana na yasiyoonekana kingaliweza kuondolewa ndipo malaika wangalionekana wakiwakaribia wale waliokuwa waaminifu, wakiwalinda na mishale ya madanganyifu ya Shetani.

SURA YA NANE



# UJUMBE WA MALAIKA WA PILI

MAKANISA ambayo yalikataa kuupokea ujumbe wa malaika wa kwanza yalikataa nuru iliyotoka mbinguni. Ujumbe ule ulipelekwa kwa neema kusudi uwaamshe watu ili waitambue hali yao hasa ya kupenda anasa za dunia na kuasi, wapate kujitayarisha kumlaki Bwana wao.

Ujumbe wa malaika wa kwanza ulitolewa kwa minajili ya kulitenga kanisa la Kristo na mvuto mpotovu wa dunia. Lakini kwa watu wengine, hata wale waliojidai kuwa ni Wakristo, mambo ya dunia ya kupendeza yalikuwa na mvuto wenye nguvu zaidi ya mambo ya mbinguni. Walichagua kuisikiliza sauti na mashauri ya kidunia wakauacha ujumbe huu mzito na wenye maana.

Mungu huutoa mwanga kusudi ukuzwe na kutiiwa, si kwamba udharauliwe na kukataliwa. Mwanga unaotolewa na Mungu huwa giza kwa wale wasioujali. Roho ya Mungu anapoacha kuuingiza ukweli katika mioyo ya watu, ndipo kusikia neno la Mungu huwa bure, na mahubiri yote huwa kama kitu kisicho na faida.

Makanisa yalipolidharau shauri la Mungu kwa kuukataa ujumbe juu ya marejeo ya Kristo, Bwana naye akawakataa. Malaika wa kwanza alifuatwa na wa pili ambaye alipaaza sauti akisema, "Umeanguka, umeanguka, Babeli,

mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasharati wake." Ufunuo 14:8. Watu wale waliokuwa wakiyatazamia marejeo ya Yesu walifahamu ya kwamba ujumbe huu ulitolewa kwa kutangaza kuanguka kwa makanisa kwa njia ya kiroho, kwa sababu yaliukataa ujumbe wa kwanza. Mbiu hii, "Umeanguka Babeli," ilitolewa mnamo 1844, na watu wapata elfu hamsini waliaacha makanisa yale kwa ajili ya maneno haya.

Wale watu waliouhubiri ujumbe wa kwanza hawakuwa na kusudi la kuleta utengano katika makanisa, wala hawakutazamia kufanya hivyo, tena hawakufikiri kuanzisha shirika mpya. William Miller alisema hivi, "Katika kazi zangu zote, sikuwa na hamu wala fikara yo yote kuanzisha dini nyingine zaidi ya zile zilizopo, wala kuifanikisha dini fulani kwa ajili ya hasara ya dini nyingine. Nalinuia kuwafanikisha wote. Kwa vile nilivyofikiri ya kwamba Wakristo wote wangependezwa kuyatazamia marejeo ya Kristo, ingawa wengine hawawezi kupatana nami katika maoni yangu yote sikudhani ya kwamba wangekuwa na nia mbaya juu yao wanaoshikilia fundisho hili, na kwa hiyo sikuona ya kwamba itakuwa ni lazima kutengana na kuweka mikutano mbali mbali. Kusudi langu kuu lilikuwa kuwageuza watu kwa Mungu, kuwaambia walimwengu juu ya hukumu ijayo, na kuwavuta wenzangu wapate kuitayarisha mioyo yao kwa namna itakavyowawezesha kumlaki Mungu kwa amani. Wingi wa watu walioongoka kwa ajili ya kazi yangu waliungana na makanisa mbali mbali yaliyokuwako. Watu wengine waliponijia wakiniuliza juu ya mambo yaliyowapasa kufanya, kila mara naliwajibu nikiwaambia ili waende po pote walipopendezwa kwenda; wala sikuwakatia shauri

juu ya dini yo yote kwa kusifu madhehebu fulani zaidi ya nyingine."

Kwa muda fulani makanisa mengi yalimsikiliza kwa furaha, lakini kwa jinsi walivyokataa kuisadiki habari ya marejeo ya Kristo, walikuwa na hamu ya kuyakanusha mafundisho yote yaliyohusiana na jambo lile. Wale waliokubali fundisho lile wakawa katika hali ya taabu na mahangaiko ya moyoni. Waliyapenda makanisa yao, na hawakupendezwa kutengana nayo; lakini kwa jinsi walivyochekelewa na kudhulumiwa, na kukatazwa wasiseme juu ya tumaini lao, wala kuihudhuria mikutano inapohubiriwa habari za kuja kwa Bwana, hatimaye watu wengi waliondoka wakaitupa ile nira iliyokuwa imewekwa juu yao.

Wale watu waliokuwa wakiyatazamia marejeo ya Kristo, walipoona ya kwamba makanisa yaliukataa ushuhuda wa Neno la Mungu, hawakuyahesabu tena kuwa ni kanisa la Kristo ambaye ni "nguzo na msingi wa kweli," na maneno haya, "Umeanguka Babeli," yalipoanza kutangazwa, waliona kwamba walifanya haki kwa vile walivyojitenga na ushirika wa makanisa yaliyokuwako zamani.

Tangu ujumbe ule wa kwanza ulipokataliwa, mageuzi ya kusikitisha sana yameonekana katika makanisa. Ukweli unapodharauliwa, ndipo mambo ya uongo yanapopokelewa na kukuzwa. Upendo kwa Mungu na imani kwa Neno lake zimepoa. Makanisa yamemhuzunisha Roho wa Bwana, na kwa kadiri kubwa sana Roho wa Mungu ameondolewa.

### *Muda wa Kukawia*

Mwaka wa 1843 ulipopita kabisa bila Yesu kuonekana, wale waliokuwa wakimngoja kwa imani wakawa na shaka na fadhaa kuu. Walakini ingawa waliuona uchungu mkuu

wa namna ile, wengi waliendelea kusoma Biblia kwa makini, wakiichunguza bayana ya imani yao, na pia waliyachunguza sana maneno ya unabii kusudi wapate nuru zaidi. Ushuhuda wa Biblia juu ya maoni yao ulionekana kuwa dhahiri na uliothibitika. Dalili ambazo zilionekana wazi zilionyesha ya kuwa kuja kwa Yesu mara ya pili kulikaribia sana. Wale waaminio hawakuweza kuueleza sababu ya jambo lile lililowatilia uchungu; lakini walifahamu dhahiri ya kuwa Mungu alikuwa amewaongoza katika siku zilizopita.

Imani yao iliimarishwa sana kwa kuyasoma mafungu yale ya Maandiko yaliyoonyesha ya kwamba kutakuwa muda wa kukawia. Mnamo mwaka wa 1842, Roho wa Mungu alimwongoza Charles Fitch apate kuitengeneza ramani ya wakati ule uliotabiriwa na nabii, na ramani ile lihesabiwa na wengi wa Waadventista (wale waliotazamia kuja kwa Kristo) kuwa kama utimizo wa agizo lililotolewa na nabii Habakuki kwa maneno haya, "Iandike njozi, ukaifanye iwe wazi sana katika vibao." Hakuna hata mmoja aliyeona neno la wakati ule wa kukawia jinsi ulivyotabiriwa katika unabii ule ule. Lakini baada ya uchungu ule kwa kutomwona yule waliyemtazamia, ndipo maana halisi ya maandiko yale ikatambulikana. Hivi ndivyo asemavyo nabii, "Iandike njozi, ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji. Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja haitakawia." Hab. 2:2, 3.

Wale waliokuwa wakingoja walifurahi kwa kuwa Yeye aujuaye mwisho tangu mwanzo alikuwa ametazama vizazi, akaona jinsi watakavyoona uchungu, ndipo akawapa

maneno ya kuwatia nguvu na tumaini. Kama mafungu ya namna hii yasingalikuwako katika Biblia, yanayoonyesha ya kwamba njia waliyokuwa wameifuata ilikuwa sawa, imani yao ingalipunguka katika siku zile za taabu.

Katika mfano wa wanawali kumi, tunaousoma katika Mathayo 25, mambo yaliyotokea kwa wale waliotazamia kurudi kwa Yesu yameelezwa kwa kufuata mambo yatendekayo katika arusi katika nchi za Mashariki "Ndipo ufalme wa mbinguni utakapofanana na wanawali kumi, waliotwaa taa zao, wakatoka kwenda kumlaki bwana arusi." "Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi."

Mabadili yaliyoenea sana duniani baada ya kutangazwa kwa ujumbe wa kwanza, yalilinganishwa na kuondoka kwa wale wanawali; tena kupita kwa wakati wa kumngoja Kristo, na wakati wa uchungu kwa ajili ya kutomwona, haya yote yalionyeshwa kwa kukawia kwa bwana arusi. Baada ya wakati uliotazamiwa kupita, waaminio wa kweli waliendelea kuamini ya kwamba mwisho wa mambo yote ulikuwa umekaribia lakini baadaye kidogo ilionekana ya kwamba walikuwa wakianza kupotewa na juhudi yao na kujitoa kwao kwa kadiri fulani na walikuwa wameanza tayari kuwa katika hali iliyoelezwa katika mfano wa wanawali waliokuwa wakilala usingizi wakati bwana arusi alipokawia.

Ushupavu wa dini ulianzishwa mnamo wakati ule. Wengine kati yao waliojidai kuwa waaminio wenye juhudi katika ujumbe huu walianza kulikataa Neno la Mungu kuwa ni kiongozi cha pekee kisichoweza kukosa, na kwa ajili ya kujidai ya kwamba waliongozwa na Roho wa Mungu, walianza kufuata fikara na maono yao wenyewe. Kuli-

kuwa na wengine ambao walionyesha juhudi na ushupavu pasipo kutumia akili, wakiwashutumu wote wasiokubaliana nao kwa matendo yao. Mambo yao na matendo yao ya ushupavu wa dini hayakupendelewa na wingi wa watu waliokuwa wakitazamia kurudi kwa Kristo; na pia matendo ya watu wale yalileta lawama juu ya kazi ya Mungu.

Kuhubiriwa kwa ujumbe wa kwanza katika 1843, na kuhubiriwa kwa kilio cha usiku wa manane katika mwaka wa 1844, kulisaidia kutuliza ushupavu wa dini na mafarakano. Wale waliokuwa wakishirikiana katika mashauri haya walisikilizana; mioyo yao ilijaa upendo wao kwa wao, na kwa Yesu pia, ambaye walikuwa wakimngoja. Imani ile ile, tumaini lile lile lenye baraka, liliwaweka katika hali ya kutoongozwa na mvuto wo wote wa kibinadamu, ikiwa kama ngao juu ya mashambulio ya Shetani.

SURA YA TISA



# KILIO CHA USIKU WA MANANE

HATA bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi. Lakini usiku wa manane, pakawa na kelele, "Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki. Mara wakaondoka wanawali wale wote, wakazitengeneza taa zao." Mathayo 25:5-7.

Kati kati ya mwaka wa 1844 wale waliokuwa wakitazamia kurudi kwa Kristo wakatambua kosa lao kwa namna walivyohesabu nyakati za unabii mwanzoni, wakauthibitisha wakati ulivyo halisi. Siku 2,300 zilizoandikwa katika Danieli 8:14, ambazo wote waliamini ya kwamba zitafikia kuja kwa Kristo mara ya pili, zilifikiriwa ya kwamba zitaishia mwaka wa 1844 mnamo mwezi wa Machi au Aprili; lakini ilionekana ya kwamba zinaendelea mpaka wakati wa vuli kama mwezi wa Oktoba katika mwaka ule ule, tena watu wale walitazamia siku zile kama wakati wa kuonekana kwa Bwana. Tangazo la ujumbe huu juu ya wakati lilikuwa hatua nyingine kwa utimilizo wa mfano ule wa arusi, ambao matumizi yake kwa kueleza mambo yaliyotokea yameonekana tayari katika mambo yaliyowapata wale waliokuwa wakimtazamia Yesu.

Kama ilivyoandikwa katika mfano wa wanawali, kilio kile kilitokea mnamo usiku wa manane, kikitangaza kukaribia kwa bwana arusi, vivyo hivyo katika utimizo wake,

katikati ya mwaka wa 1844, baada ya siku zile ilipofikiriwa mara ya kwanza ya kwamba siku 2,300 zitakoma, na kabla ya mwezi wa Oktoba, 1844, ambao baadaye ilionekana ya kwamba siku zile zitakoma, ndipo kilio cha namna ile kilipotokea, kwa maneno yale yale yaliyoandikwa katika Biblia: "Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki."

Habari ile ilienea pote kama maji yanavyogharikisha nchi. Ilienea katika kila nchi, kutoka mji mpaka mji mwingine, tokea kijiji mpaka kijiji kingine, hata na katika mashamba palipokuwa mbali sana na mji, mpaka watu wa Mungu wakaamshwa kabisa. Ushupavu wa dini ulitoweka kabla ya tangazo hili, kama umande utowekavyo jua lichapo. Waaminio walipata kusimama imara tena, na mioyo yao ikaanza kujaa tumaini na uthabiti.

Kazi ilikuwa haikuzuiliwa na mambo ya ushupavu wa dini ambayo kwa kawaida huonekana kila mara panapokuwa hamaniko la kibinadamu pasipo kutawaliwa na kuongozwa na Neno la Mungu na Roho Mtakatifu. Siku zile zilifanana na siku za udhilifu na kumrudia Bwana zilizoonekana katika siku za Waisraeli wa zamani, baada ya kupata ujumbe wa lawama kutoka kwa watumishi wa Bwana. Kazi ile ilionekana kuwa mamoja na kazi za Mungu katika vizazi vyote. Si kwamba ilikuwako hali ya furaha nyingi mno, bali ilikuwako hali ya kumwaza Mungu na kutafutia mioyo, kuziungama dhambi na kuacha mambo ya dunia na anasa zake. Kujitayarisha kumlaki Bwana kulikuwa jambo lililolemea roho za watu. Kulikuwa na maombi ya juhudi na kujitoa kabisa kwa Mungu.

Ujumbe wa kilio cha usiku wa manane haukuendeshwa kwa njia ya majadiliano, ingawa maneno yaliyoandikwa katika Biblia yalikuwa dhahiri na ya kuthibitisha jambo lile kwa hakika. Kilio kilikuwa na uwezo wa kuigusa mioyo ya watu. Hayakuwako mashaka wala tashwishi. Siku

ile Kristo alipoingia Yerusalemu kwa shangwe, watu waliokusanyika kutoka pande zote kwa kufanya siku kuu ya Pasaka, walikusanyika katika Mlima wa Mizeituni, na walipoungana na makutano ya watu waliofuatana na Yesu, walivutwa na jambo lile lililofanywa kwa maongozi ya Roho, wakapaaza sauti pamoja wakisema, "Ndiye mbarikiwa, Yeye ajaye kwa jina la Bwana." Mathayo 21:9. Hivyo ndivyo ilivyokuwa na watu wasioamini walikusanyika katika mikutano ya wale waliokuwa wakimtazamia Yesu—wengine walikuja kwa ajili ya upekuzi tu na wengine kwa minajili ya kuwachekelea—hao nao walivutwa na kusadikishwa na uwezo ule ulioutia nguvu ujumbe ukisema hivi, "Haya, Bwana arusi anakuja!"

Wakati ule kulikuwa na imani iliyoyafanya maombi kujibiwa—imani iliyotazamia hayo malipo ya mwisho. (Ebr. 11:26). Roho wa neema aliwashukia wale waombaji kama manyunyu ya mvua yaangukayo juu ya ardhi iliyokauka. Wale wliokuwa wakitazamia kumwona Mwokozi uso kwa uso karibuni walikuwa na furaha isiyokadirika. Uwezo mkuu wa Roho Mtakatifu, unaolainisha na kuutiisha moyo, uliingia katika mioyo ya watu, kwa jinsi utukufu wa Mungu ulivyoongezeka juu ya wale waaminifu wenye imani.

Kwa kicho na utulivu wale walioupokea ujumbe waliufikia wakati ambao walikuwa wakitumaini kumwona Bwana wao. Kila asubuhi waliona ya kwamba ilikuwa wajibu wao wa kwanza kuhakikisha ya kwamba wamekubaliwa na Mungu. Walikuwa na umoja na upendano wa moyo, na waliombeana sana wao kwa wao. Walizoea kukusanyika mahali pa faragha wapate kuzungumza na Mungu, na sauti zao za maombezi zilipanda hata mbinguni kutoka mashambani na vichakani walipokusanyika. Walikuwa na hamu ya kuhakikisha ya kwamba walikubaliwa na Mwokozi, zaidi

ya jinsi walivyotaka chakula chao cha kila siku, na mioyo yao ilipoingiliwa na shaka fulani, hawakuweza kutulia mpaka shaka ile iondolewe. Waliposikia moyoni ushuhuda wa kusamehewa dhambi kwa neema ya Mungu, walitumaini zaidi kumwona Yeye ambaye walikuwa wanampenda.

*Waliona Uchungu Lakini Hawakuachwa*

Lakini walikuwa wameelekea kutiwa uchungu mara ya pili kwa ajili ya kutopata yaliyotazamiwa. Wakati ule waliokuwa wakimtazamia Mwokozi ulipita, naye hakuonekana. Walikuwa wamemngoja wakiwa na tumaini kuu lililo thabiti, lakini wakati ule wakawa kama Mariamu, alipofika kwenye kaburi la Yesu na kulikuta li wazi, akapaaza sauti akilia, "Wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka." Yohana 20:13.

Hali ya kicho, na woga ya kwamba labda ujumbe ule uliweza kuwa wa kweli, kwa muda fulani ilikuwa imewazuia walimwengu wasioamini. Lakini hali hii haikutoweka mara moja baada ya kupita kwa wakati ule watu wale walioona uchungu, lakini kwa jinsi ambavyo hawakuona dalili yo yote iliyoonyesha ghadhabu ya Mungu, waliacha woga wakaanza tena kuwafanyizia mzaha na lawama. Watu wengi waliokuwa wakijidai ya kwamba waliamini ya kuwa marejeo ya Bwana yalikaribia, walikanusha imani yao. Wengine ambao walikuwa na hakika zaidi, waliona uchungu sana kwa jinsi walivyoona wameferheheshwa, hata wakataka kupotea usoni pa dunia. Walimnung'unikia Mungu kama Yona alivyofanya, waliona afadhali kufa kuliko kuishi. Wale waliokuwa wameijenga imani yao juu ya maoni ya wenzao badala ya Neno la Mungu, sasa walikuwa tayari tena kuyageuza maoni yao. Wenye kudhihaki walivavuta wanyonge na waoga wakawafuata, na wote wa-

kaungama kwa kutangaza ya kwamba haiwapasi kuogopa wala kumngoja Bwana tena. Wakati ulikuwa umepita, wala Bwana hakuja, na walifikiri ya kwamba dunia ingedumu kuwa katika hali ile kwa miaka elfu nyingi.

Waaminio wenye bidii walikuwa wameacha vyote kwa ajili ya Kristo, na walikuwa wamefahamu kuwapo kwake kati yao zaidi ya zamani. Walidhani ya kwamba wamelitoa onyo la mwisho kwa dunia yote, na walikuwa wakitazamia kupokewa na Bwana wao karibuni na kukaa pamoja naye na malaika za mbinguni; na kwa kadiri kubwa walikuwa wametengana na lile kundi la watu wasioamini. Walikuwa wameomba kwa makini, "Uje Bwana Yesu, uje upesi." Lakini hakuja. Waliona ya kwamba kuanza tena kuuchukua mzigo wa masumbufu ya dunia hii na mashaka, na kuvumilia dhihaka, dharau, na matusi ya watu wa dunia, kweli kulikuwa majaribu ya imani na uvumilivu.

Walakini uchungu huo haukuwa mkuu kama ule uliowapata wanafunzi wa Kristo wakati wa kuja kwake mara ya kwanza. Yesu alipoingia Yerusalemu kwa shangwe akimpanda punda, wafuasi wake walidhani ya kwamba alikuwa karibu kuketi katika kiti cha enzi cha Daudi na kuwaokoa Waisraeli mikononi mwa watesi wao. Kwa furaha kuu na matumaini, walishindana wao kwa wao kwa kumheshimu Mfalme wao. Watu wengi waliyatandaza mavazi yao njiani yapate kuwa kama zulia atakapopitia, na wengine wakakata matawi ya miti wakayatandaza njiani. Kwa furaha kuu walipaaza sauti wakisema, "Hosana, mwana wa Daudi!"

Mafarisayo, waliposhtushwa na kukasirishwa na kelele hii ya shangwe, wakamwomba Yesu awakaripie wanafunzi wake, na Yesu akawajibu akisema, "Wakinyamaza hawa,

mawe yatapiga kelele." Luka 19:40. Unabii ni lazima utimizwe. Wanafunzi walikuwa wakilitimiza kusudi la Mungu; lakini walikuwa wanaelekea kuona uchungu mkuu ajabu. Zilipita siku chache tu ndipo walimwona Mwokozi akifa kifo cha maumivu makuu, wakamzika kaburini. Mambo waliyoyatazamia yalikuwa hayajatimizwa hata kidogo, na matumaini yao yalikufa pamoja na Yesu. Bwana wao alipofufuka akiwa mshindi, kutoka katika wafu, ndipo walipofahamu ya kwamba yale yote yalikuwa yametabiriwa na manabii ya kwamba "ilimpasa Kristo kuteswa, na kufufuka katika wafu." Matendo 17:3. Vivyo hivyo maneno ya unabii yalitimizwa katika ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili. Ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili ulitolewa kwa wakati uliopangwa, na habari hizo zilitimiliza kazi ambayo Mungu alikusudia kutimiza.

Watu wa dunia walikuwa wakitazama, wakingoja waone jambo litakalotendeka, na wakiona ya kwamba wakati umepita, wala Kristo hakuonekana, ndipo mambo hayo yote na mafundisho hayo yote juu ya kumtazamia Kristo yangeachwa kabisa. Ingawa wengi walipojaribiwa vikali waliacha imani yao, lakini kulikuwa na wengine waliosimama imara. Hawakulivumbua kosa lo lote kwa vile walivyohesabu miaka iliyoandikwa katika unabii. Adui zao wenye akili kabisa hawakuweza kupindua maneno hayo jinsi walivyohesabu wakati. Kwa kweli, kulikuwa na kosa kwa jambo lililotazamiwa hasa, lakini neno hilo halikuweza kuipunguza imani yao juu ya Neno la Mungu.

Mungu hakuwaacha watu wake; Roho wake alidumu kuwa na wale ambao hawakuikataa kwa haraka ile nuru waliyokwisha kuipokea, na kuinenea habari ya marejeo ya Kristo. Mtume Paulo, alipokuwa akivitazama vizazi vya

mbele, aliandika maneno ya kuwaonya na kuwatia nguvu wanaojaribiwa, maneno yaliyofaa kwa wale waliomngojea Bwana katika siku zile za taabu: "Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu. Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi. Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia. Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; naye akisitasita, roho yangu haina furaha naye. Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu." Ebr. 10:35-39.

Njia yao ya pekee ya usalama ilikuwa tu kuikuza ile nuru ambayo walikuwa wamepewa na Mungu, kuzishikilia ahadi zake, kudumu kuyachungua Maandiko, na kumngoja kwa saburi wakitazamia kuipokea nuru zaidi.



SURA YA KUMI

# PATAKATIFU

FUNGU la Biblia ambalo limekuwa kama msingi wa nguzo ya imani juu ya kuja kwa Yesu zaidi ya mafungu yote, lilikuwa fungu lile linalosema: "Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa." Dan. 8:14. Maneno haya yote yalijulikana na wote walioamini ya kuwa kuja kwa Bwana kulikuwa kumekaribia. Maneno haya ya unabii yalikaririwa kwa furaha na watu maelfu, tena yalikuwa kama kanuni ya imani yao. Wote walidhani ya kwamba matumaini yao yote yaliyategemea mambo yaliyoonyeshwa katika fungu hili. Siku hizi za unabii zilizotajwa hapo, zilionyeshwa ya kwamba zingeishia mnamo 1844 katika siku za masika, kama mwezi wa Oktoba. Wale waliokuwa wakimngoja Yesu walikuwa wakifikiri mamoja na Wakristo wengine wote duniani, wakidhani ya kwamba dunia hii, au sehemu yake fulani, ndiyo iliyokuwa patakatifu, na ya kwamba kutakaswa kwa patakatifu ndiko kutakaswa kwa dunia na moto wa siku kuu ya mwisho. Walifahamu ya kwamba jambo hili litafanywa Kristo atakapokuja mara ya pili. Kwa hivyo wakakata neno ya kwamba Kristo atakuja duniani katika mwaka wa 1844.

Lakini siku iliyowekwa iliwadia, wala Bwana hakuonekana. Waaminio walijua ya kwamba Neno la Mungu hali-

wezi kukosa; na bila shaka ni maelezo yao ya maneno ya unabii yasiyokuwa sawa; lakini kosa lilikuwa wapi? Wengi wao walikata shauri kwa haraka kwa kukanusha ya kwamba siku 2,300 ziliishia mnamo 1844. Hawakuweza kutoa sababu yo yote kwa kusema vile, isipokuwa walisema ya kwamba Kristo hakuja katika siku ile aliyotazamiwa. Walijadiliana wakisema ya kwamba kama siku zile za unabii zilitimia mnamo 1844, basi Kristo angalikuja kupatakasa patakatifu kwa kuitakasa dunia kwa moto; na ya kwamba kwa jinsi ambavyo hakuja, siku zile zilikuwa hazijatimia bado.

Ingawa wingi wa wale waliomngoja Yesu waliacha njia yao ya zamani ya kuzihesabu nyakati za unabii, na baadaye waliukana usahihi wa mambo na mafundisho yaliyoegemezwa na unabii ule, kulikuwa na wachache kati yao waliokataa kuyakanusha mafundisho ya imani yao na mambo yaliyothibitishwa na neno la Biblia na shahidi maalum wa Roho wa Mungu. Waliamini ya kwamba katika kuchunguza maneno ya Biblia, walikuwa wamefuata njia za kweli kwa kueleza maneno yake, na ya kwamba ilikuwa wajibu wao kuyashikilia mafundisho ya kweli waliyokwisha kujifunza, na ya kwamba iliwapasa kudumu katika njia ile ile kwa kuchunguza maneno ya Biblia. Kwa maombi na juhudi waliyarudia mambo waliyokwisha kuyasoma, wakachunguza Biblia kwa uangalifu zaidi ili wapate kulivumbua kosa lao. Wasipoweza kuliona kosa katika maelezo yaliyotolewa juu ya nyakati za unabii, waliongozwa kuchunguza kwa makini sana yale mafundisho yanayohusiana na patakatifu.

### *Patakatifu pa Duniani na pa Mbinguni*

Katika uchunguzi wao waliona ya kwamba patakatifu

pa duniani, palipojengwa na Musa kwa amri ya Mungu, kwa kuufuata mfano aliopewa mlimani, palikuwa kama "mfano wa wakati huu uliopo sasa; wakati huo sadaka na dhabihu zinatolewa," yaani patakatifu pake pawili palikuwa "nakala za mambo yaliyo mbinguni;" na ya kwamba Kristo Kuhani wetu Mkuu, ndiye "mhudumu wa patakatifu, na wa ile hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu;" na ya kwamba "Kristo hakuingia patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa-Mungu kwa ajili yetu." Ebr. 9:9, 23; 8:2; 9:24.

Patakatifu pa mbinguni, ambapo Yesu anahudumu kwa ajili yetu, ndipo patakatifu pa kwanza, na palipo pakuu, ambapo palipojengwa na Musa palikuwa mfano wake. Kwa jinsi ambavyo patakatifu pa duniani palikuwa na sehemu mbili, yaani patakatifu na patakatifu pa patakatifu (au patakatifu mno), vivyo na patakatifu pa mbinguni pana patakatifu pawili. Sanduku la agano ambamo kuna sheria ya Mungu, na madhabahu ya uvumba, na vifaa vingine vilivyopatikana katika patakatifu pa duniani, vilikuwa mifano ya vile vilivyomo katika patakatifu pa mbinguni. Mtume Yohana alipokuwa katika njozi yake takatifu, aliruhusiwa aingie mbinguni, na pale alipata kuziona taa saba za moto na madhahabu ya uvumba, na "Hekalu ya Mungu ilipofunguliwa," ndipo akaona "sanduku la Agano." Ufunuo 4:5; 8:3; 11:19.

Wale waliokuwa wakiitafuta kweli waliyapata mambo yaliyowathibitishia kabisa ya kwamba pana patakatifu mbinguni. Musa alipajenga patakatifu pa duniani kwa mfano alioonyeshwa. Paulo aliarifu ya kwamba mfano ule ndio uliokuwa patakatifu pa asili palipo mbinguni. Ebr.

8:2, 5.) Yohana pia alishuhudia ya kwamba alipaona mbinguni.

Mnamo mwisho wa siku 2,300 katika 1844, hakuna patakatifu palipokwisha kuwako duniani kwa karne nyingi; kwa hiyo yamkini patakatifu pa mbinguni ndipo palipoonyeshwa kwa maneno haya, "Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa." Lakini patakatifu pa mbinguni pangewezaje kuwa na haja ya kutakaswa? Wale watu waliokuwa wakiyachunguza maneno ya unabii walianza kurudia Maandiko tena, wakaona ya kwamba kutakaswa kwa patakatifu hakukuwa kuondoa uchafu wo wote unaoonekana, kwa kuwa utakaso ulipasa kufanywa na damu, na kwa hiyo lazima kuwe kutakaswa dhambi. Hivi ndivyo asemavyo mtume: "Basi ilikuwa sharti nakala za mambo yaliyo mbinguni zisafishwe kwa hizo (yaani damu ya wanyama), lakini mambo ya mbinguni yenyewe yasafishwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo (yaani damu yenye thamani ya Kristo)." Ebr. 9:23.

Kwa kusudi la kupata ujuzi kamili wa utakaso uliotajwa katika maneno ya unabii, iliwapasa kufahamu namna ya huduma inayofanyika katika patakatifu pa mbinguni. Huduma hii ya mbinguni iliweza kufahamiwa tu kwa kujifunza juu ya huduma ya patakatifu pa duniani; kwa sababu Paulo asema ya kwamba makuhani waliohudumu katika patakatifu pa duniani walihudumu "kwa mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni." Ebr. 8:5.

### *Kutakaswa kwa Patakatifu*

Kwa jinsi dhambi za watu zilivyopitishwa, kwa mfano, mpaka patakatifu pa duniani kwa damu ya dhabihu ya

dhambi, vivyo hivyo na dhambi zetu zinapitishwa mpaka patakatifu pa mbinguni kwa damu ya Kristo. Na kwa jinsi ambavyo kutakaswa kwa mfano kwa patakatifu pa duniani kulifanywa kwa kuondolewa kwa dhambi ambazo zilipachafua, vivyo hivyo na kutakaswa kuliko halisi kwa patakatifu pa mbinguni kutafanywa kwa kuondolewa, au kufutwa, kwa dhambi zilizoandikwa humo. Kufutiwa huku kwa dhambi kunataka ukaguzi wa vitabu, ili ionekane ya kwamba ni kina nani ambao, kwa kuzitubia dhambi na kumwamini Kristo, wanastahili kufadhiliwa na upatanisho wake. Kwa hivyo kazi ya kupatakasa patakatifu inafanya hukumu ya upelelezi kuwa ni lazima. Kazi hii ni lazima ifanywe kabla ya kuja kwa Kristo kuwaokoa watu wake, kwa kuwa atakapokuja, atakuja na ujira wake "kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo." (Ufunuo 22:12.)

Kwa hivi wale waliofuata nuru iliyowatangulia katika maneno ya unabii, waliona ya kwamba, badala ya kuja duniani mnamo mwisho wa siku 2,300 katika mwaka wa 1844, Kristo aliingia katika patakatifu mbinguni, usoni pa Mungu hasa, ili kuifanya kazi ya mwisho ya upatanisho, akiyafanya mambo tayari kwa kuja kwake.



SURA YA KUMI NA MOJA

# UJUMBE WA MALAIKA WA TATU

KRISTO alipoingia katika patakatifu mno mbinguni ili kuifanya kazi ya mwisho ya upatanisho, aliwapa watumishi wake ujumbe wa mwisho wa neema, upate kutangazwa kwa watu wote wakaao duniani. Hilo ndilo onyo la malaika wa tatu lililoandikwa katika Ufunuo 14. Baada ya tangazo lile, mara nabii alimwona Mwana wa Adamu akija pamoja na utukufu wake apate kuyavuna mavuno ya dunia.

Jinsi ilivyotabiriwa katika Maandiko, huduma ya Kristo katika patakatifu pa patakatifu ilianzishwa mnamo mwisho wa siku zilizotabiriwa, mwaka wa 1844. Maneno haya ya mwandishi wa Ufunuo yanahusika na wakati ule, "Kisha hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa, na sanduku la agano lake likaonekana ndani ya hekalu lake." Ufunuo 11:19. Sanduku la agano la Mungu liko katika sehemu ya pili ya patakatifu. Kristo alipoingia pale, kusudi kuhudumu kwa ajili ya mwenye dhambi, hekalu la ndani lilifunguliwa, na sanduku la Mungu likaonekana. Utukufu na uwezo wa Mungu ulifunuliwa kwa wale ambao kwa imani walimwona Mwokozi akifanya kazi yake ya kuwaombea.

Utukufu wake ulipolijaza hekalu, mwanga uliotoka katika patakatifu mno uliwaangazia watu waliokuwa wakimngoja duniani.

Kwa imani, walikwisha kumfuata Kuhani wao Mkuu kutoka katika patakatifu mpaka patakatifu mno, na walimwona akiidai damu yake mbele ya sanduku la Mungu. Katika sanduku lile takatifu kuna sheria ya Baba, sheria ile iliyotolewa na Mungu mwenyewe kati ya ngurumo kule mlimani pa Sinai, na iliyoandikwa kwa mkono wake mwenyewe juu ya vibao vya mawe. Hakuna hata amri moja ambayo imetanguka; hakuna yodi wala nukta ambayo imegeuzwa. Mungu alipomtolea Musa nakala ya sheria yake, aliiweka sheria ya asili katika patakatifu mbinguni. Kwa kuzitazama amri zote moja moja, wale waliokuwa wakiitafuta kweli, katikati ya amri kumi waliiona amri ya nne ikiandikwa jinsi ilivyotangazwa mara ya kwanza: "Ikumbuke siku ya Sabato, uitakase. Siku sita utafanya kazi, utatenda mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako; siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako: maana kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba: kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato, akaitakasa." Kutoka 20:8-11.

Roho ya Mungu aliwavuta moyo wanafunzi hawa juu ya Neno lake. Walisadikishwa ya kwamba kwa kutojua kwao walikuwa wamekosea amri ya nne kwa ajili ya kutojali siku ya mapumziko ya Muumba. Walianza kuzichungua sababu za kuitunza siku ya kwanza ya juma badala ya siku ambayo Mungu aliitakasa. Hawakupata neno lo lote katika Maandiko Matakatifu lililowaonyesha ya kwamba amri ya nne ilikuwa imetanguka, wala hawakupata habari

yo yote juu ya kugeuzwa kwa Sabato; baraka ile ya kuitakasa siku ya saba mwanzoni, ilikuwa haijaondolewa. Walikuwa wakitafuta kwa uaminifu sana ili wapate kujua na kuyafanya mapenzi ya Mungu, na walipofahamu ya kwamba walikuwa wamekosea sheria yake, mioyo yao ikajaa huzuni kuu. Mara wakaanza kuonyesha uaminifu wao kwa Mungu kwa kutunza Sabato yake takatifu.

Watu wengi walijaribu sana kuipindua imani yao. Hakuna mtu ye yote aliyeshindwa kuona ya kwamba, kama patakatifu pa duniani palikuwa mfano wa patakatifu pa mbinguni, sheria iliyowekwa katika sanduku duniani ilikuwa nakili ya sheria iliyoko katika sanduku la mbinguni, na ya kwamba ikiwa mtu aliukubali ukweli juu ya patakatifu pa mbinguni, ilipasa kukubali na kuyatimiza madai ya sheria ya Mungu, pamoja na sharti ya amri ya nne juu ya Sabato.

Wale ambao waliikubali fundisho juu ya kazi ya Kristo ya upatanishi, na umilele wa amri za Mungu, waliona ya kwamba mambo haya ndiyo mafundisho yaliyodhihirishwa katika ujumbe wa malaika wa tatu. Malaika wa tatu asema, "Hapo ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Ufunuo 14:12. Maneno haya yametanguliwa na onyo lililo zito na la kutisha: "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake." Ufunuo 14:9,10. Maelezo yalitakiwa ili kudhihirisha wazi maana ya mifano iliyotumiwa hapa, kusudi kuufahamu ujumbe huu. Majina haya yalifananisha nini: mnyama,

sanamu, na alama? Wale waliokuwa wakiutafuta ukweli wakarudia tena kujifunza maneno ya unabii.

*Mnyama na Sanamu (Mfano) Yake*

Mnyama huyu wa kwanza anasimama badala ya Kanisa la Kirumi, ambalo ni shirika la kanisa lililofunikwa na nguvu ya serikali, kanisa lenye mamlaka ya kuwahukumu watu wakataao kulitii. Sanamu ya mnyama inasimama badala ya dini nyingine inayojivika na uwezo wa namna ile. Kutengeneza sanamu hii ni kazi ya mnyama yule ambaye kuondoka kwake kwa amani, na mafundisho ya upole yanamfanya kuwa mfano wa ajabu wa nchi ya Amerika (U. S. A.).. Katika Amerika ndipo tunapoweza kuipata sanamu au mfano wa mamlaka ya Papa. Makanisa ya nchi hiyo, yatakapoungana pamoja katika mafundisho ya dini yanapofuatwa nao kwa kawaida, na pia kuivuta Serikali ya nchi ya Amerika ipate kuzitilia nguvu amri zao, na kuzihifadhi kawaida zao, ndipo Waprotestanti wa Amerika watakapokuwa wameifanya sanamu ya mamlaka ya Kanisa la Kirumi. Ndipo kanisa la kweli litashambuliwa na kuteswa, kama watu wa Mungu wa zamani walivyotendwa.

Mnyama mwenye pembe kama za mwana kondoo awaamuru "wote wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao: tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake." Ufunuo 13:16,17. Alama au chapa hii ndiyo ambayo malaika wa tatu alitoa onyo juu yake. Ni alama ya yule mnyama wa kwanza, au ma-

mlaka ya Papa, na kwa hiyo alama hii inaweza kupatikana katika tabia kuu za mamlaka ya Papa. Nabii Danieli alisema ya kwamba Kanisa la Kirumi, lililofananishwa na pembe ndogo, ndilo litakatakalotumaini kubadili majira na sheria (Dan. 7:25), na Paulo amelitaja kanisa lile kuwa ni mtu wa dhambi (2 The. 2:3, 4), ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu. Mamlaka ya Papa haikuweza kujiinua juu ya Mungu isipokuwa kwa njia ya kubadili sheria ya Mungu; na mtu ye yote ambaye kwa makusudi aishika sheria jinsi ilivyogeuzwa na kujua hivyo, anamheshimu kamili yule aliyegeuza sheria hivi.

Amri ya nne, ambayo Kanisa la Kirumi limejitahidi sana kuibadili, ndiyo amri ya pekee kati ya amri zote kumi inayomtaja Mungu kuwa Muumba wa mbingu na dunia, na hivi humdhirisha Mungu wa kweli kati ya miungu ya uongo. Sabato iliwekwa kuwa ukumbusho wa kazi ya uumbaji, na hivi kuelekeza fikara za wanadamu kwa Mungu wa kweli aliye hai. Ukweli wa uwezo wake wa kuumba umeonyeshwa pote katika Maandiko kwa kuthibitishwa ya kwamba Mungu wa Israeli ndiye aliye mkuu zaidi ya miungu ya ushenzi. Kama Sabato ingalitunzwa daima, ndipo fikara za wanadamu na upendo wake zingaliongozwa kwa Muumba wao kama mmoja tu anayestahili kuheshimiwa na kuabudiwa; na asingalikuwako mwabudu sanamu, wala asiyeamini ya kwamba Mungu yuko, wala mtu asiye na dini yo yote.

Amri ile inayomtaja Mungu kama Muumbaji ndiyo dalili ya haki aliyo nayo ya kuwa na mamlaka juu ya viumbe vyake vyote. Tena kugeuzwa kwa Sabato ni dalili au alama ya mamlaka ya Kanisa la Kirumi. Wale ambao, ingawa wanafahamu matakwa va amri ya nne, huchagua

kuitunza Sabato iliyofanyizwa badala ya ile ya asili, kwa hiyo humheshimu yule aliyetoa agizo hilo.

*Ujumbe wa Kutisha*

Onyo la kutisha zaidi na la kuogofya ambalo limetolewa kwa wanadamu ni lile lililoandikwa katika ujumbe wa malaika wa tatu. Dhambi ambayo inaleta ghadhabu ya Mungu isiyochanganyika na rehema, bila shaka ni dhambi mbaya sana. Wanadamu hawawezi kuachwa gizani bila kuonywa juu ya jambo hili kuu; onyo juu ya dhambi hii halina budi kutolewa kwa walimwengu kabla ya wakati wa hukumu za Mungu, kusudi wote wajue kwa nini hukumu zinatolewa, na wapate kuwa na nafasi ya kuepukana na adhabu hizo.

Katika mwisho wa shindano hili kuu, inabainika aina mbili za watu walio mbali mbali kabisa. Aina ya kwanza ndio wanaomsujudu "huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea alama katika kipaji cha uso," na hivi kujiletea hukumu mbaya iliyotangazwa na malaika wa tatu. Aina ya pili ndio "wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Ufunuo 14:9, 12.

Haya ndiyo mafundisho makuu yaliyofunuliwa kwa wale walioupokea ujumbe wa malaika wa tatu. Walipotazama nyuma na kufikiri mambo yaliyotendeka kwao tangu walipoanza kutangaza habari za kuja kwa Kristo mara ya pili mpaka kupita kwa wakati ule katika mwaka wa 1844, waliona ya kwamba uchungu wao ulikuwa umeelezwa na mioyo yao ilianza tena kujaa tumaini na furaha. Nuru iliyotoka katika patakatifu iliyaangaza mambo yaliyopita, mambo yaliyopo, na mambo yajayo, hao nao wakafahamu ya kwamba Mungu alikuwa amewaongoza kwa njia

yake iliyo ya haki. Sasa kwa ushujaa na imani thabiti, waliungana kwa kuyatoa maonyo ya malaika wa tatu. Tangu mwaka wa 1844, kwa kuutimiza unabii wa ujumbe wa malaika wa tatu, watu wa dunia wameelekezwa habari ya Sabato ya kweli, na watu wengi huongezeka daima wa kirudi wapate kuitunza siku ya Mungu iliyo takatifu.

SURA YA KUMI NA MBILI



# JUKWAA LILILO IMARA

NALIONA kundi la watu waliolindwa vizuri na kusimama imara, waliokataa kukubaliana na wale waliotaka kutaharakisha imani ya kundi. Mungu alipendezwa na wale waliosimama imara. Nalionyeshwa hatua tatu—ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Malaika aliyekuwa akifuatana nami aliniambia, "Ole wake atakayeondoa au kubadili hata sehemu moja ya maneno ya wajumbe hawa watatu. Ni jambo la muhimu sana kuyafahamu maneno ya ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Maisha ya wanadamu yanategemea sana jinsi wanavyoyapokea maneno haya."

Nalionyeshwa tena mambo ya habari hizi nikaona mambo yaliyowatokea watu wa Mungu katika maisha yao, jinsi yalivyo ya thamani sana. Waliyapata kwa shida nyingi na mateso makali. Mungu alikuwa amewaongoza hatua kwa hatua, mpaka mwishowe akawaweka juu ya jukwaa lisilotikisika. Naliwaona watu wengine wakija mmoja mmoja na kulikaribia lile jukwaa kusudi wautazame msingi wake. Wengine kwa furaha wakapanda mara juu ya jukwaa lile. Wengine walianza kutafuta kasoro fulani katika msingi ule. Walitaka ili itengenezwe sehemu nyingine, ndipo jukwaa lingekuwa kamili, na watu wangefurahi zaidi.

Wengine walishuka chini kutoka kwa jukwaa kusudi

walitazame, na wakasema ya kwamba lilijengwa vibaya. Lakini naliona ya kwamba karibu wote walisimama imara juu ya jukwaa lile wakiwasihi wale walioshuka ili wayaache manung'uniko yao; kwa kuwa Mungu ndiye aliyekuwa Mjenzi Mkuu, tena walikuwa wakishindana naye. Waliisimulia kazi ya ajabu ya Mungu, iliyowaongoza hata jukwaa lile lililo imara, na wote wakainua macho yao mbinguni, wakaanza kumtukuza Mungu kwa sauti kuu. Jambo hili liligeuza nia za wale waliokuwa wamenung'unika na kushuka chini, na kwa unyenyekevu wakapanda tena juu ya jukwaa.

*Habari ya Maisha ya Wayahudi Yarudiwa*

Nalielekezwa kwa mambo yaliyotokea zamani katika siku ambazo kuja kwa Kristo mara ya kwanza kulitangazwa. Yohana alitumwa katika roho na nguvu za Eliya ili aitengeneze njia ya Yesu. Wale waliokataa ushuhuda wa Yohana hawakufaidiwa hata kidogo na mafundisho ya Yesu. Kukataa kwao kwa ujumbe uliotabiri kuja kwake kulifanya wasiweze kukubali hata ushuhuda ulio thabiti ya kwamba Yeye ndiye Masiya. Shetani alizidi kuwaongoza wale walioukataa ujumbe wa Yohana wapate kuasi zaidi, hata wamkatae na kumsulibisha Kristo. Kwa kufanya hivyo, walijiweka katika hali ambayo kwayo hawakuweza kupata mbaraka ule siku ya Pentekote, ambao ungaliwafundisha njia iendayo hata patakatifu pa mbinguni.

Kupasuliwa kwa pazia la hekalu kulionyesha ya kwamba dhabihu na sadaka zao zisingekubaliwa tena. Dhabihu kuu ilikwisha kutolewa na kukubaliwa, na Roho Mtakatifu aliyeshuka siku ya Pentekote alielekeza nia za wanafunzi kwa patakatifu pa mbinguni badala ya patakatifu pa du-

niani. Yesu alikuwa ameingia katika patakatifu pa mbinguni kwa ajili ya damu yake, kuwamiminia wanafunzi wake mibaraka ya upatanishi wake. Lakini Wayahudi waliachwa katika giza nene. Walipotewa na nuru yote ambayo wangaliweza kupokea juu ya azimio la wokovu, wakadumu kuziamini dhabihu na sadaka zao zisizo na faida yo yote. Patakatifu pa mbinguni palikuwa pamechukua nafasi ya patakatifu pa duniani, walakini hawakulifahamu geuzo hilo. Kwa sababu hiyo hawakuweza kufaidiwa na kazi ya Yesu ya kuwaombea watu katika patakatifu.

Kuna watu wengi wanaochukizwa mno kwa jinsi Wayahudi walivyomkataa Kristo na kumsulibisha; na wanaposoma jinsi alivyotendewa vibaya na kuaibishwa, wanafikiri ya kwamba wanampenda Yesu, na ya kwamba wenyewe wasingalimkana kama Petro alivyofanya, wala kumsulibisha kama walivyofanya Wayahudi. Lakini Mungu, asomaye fikira za mioyo ya watu wote, amekuwa akijaribu upendo wao wanaojidai ya kwamba wanampenda Yesu.

Wote wa mbinguni walishughulika sana katika kutazama jinsi watu walivyoupokea ujumbe wa malaika wa kwanza. Lakini wengi waliojidai ya kwamba walimpenda Yesu, na ambao walitoka machozi waliposoma habari za msalaba, waliidharau habari njema ya kuja kwake. Badala ya kuupokea ujumbe huu kwa furaha; walitangaza ya kwamba ni udanganyifu mtupu. Waliwachukia wale waliopenda kufunuliwa kwake, wakawazuia wasiingie katika makanisa. Wale waliokanusha ujumbe wa kwanza hawakuweza kufaidiwa na ujumbe wa pili; wala hawakufaidiwa na kilio cha usiku wa manane, ambacho kilikuwa kimekusudiwa kuwatayarisha kwa kuingia na Yesu kwa imani

katika patakatifu mno palipo mbinguni. Na kwa kuukataa ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili, wamezitia giza akili zao, hata wasiweze kuiona nuru katika ujumbe wa malaika wa tatu, ambao unaongoza hata patakatifu pa patakatifu.

SURA YA KUMI NA TATU



# MADANGANYIFU YA SHETANI

SHETANI alianzisha udanganyifu wake katika Edeni. Alimwambia Hawa, "Kufa hamtakufa." Hapo ndipo Shetani alipoanza kufundisha ya kuwa mwanadamu ana hali ya kutokufa, na ameuendeleza udanganyifu huu tangu siku ile mpaka leo, tena atauendeleza mpaka siku ile Mungu atakaporejeza mafungo ya wateule wake. Nalionyeshwa Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni. Walitwaa tunda la mti ule uliokatazwa, ndipo upanga wa moto ukawekwa kuzunguka mti wa uzima, wakafukuzwa kutoka katika bustani, wasije wakalitwaa tena la mti wa uzima na kuwa wenye dhambi watakaoishi milele. Matunda ya mti huu yalikuwa na nguvu ya kudumisha hali ya kutokufa. Nalimsikia malaika fulani akiuliza hivi "Ni nani kati ya jamaa ya Adamu ambaye ameupita upanga wa moto akalitwaa tunda la mti wa uzima?" Nilisikia malaika mwingine akijibu: "Hakuna hata mmoja wa jamaa ya Adamu ambaye ameupita ule upanga wa moto na kutwaa la mti wa uzima; hivyo hakuna mwenye dhambi aliye na hali ya kutokufa." Roho ifanyayo dhambi itakufa milele—mauti ile ya mwisho ambayo baadaye hakuna kufufuka tena; ndipo ghadhabu ya Mungu itakwisha.

Mungu amesema, Roho ile ifanyayo dhambi, itakufa." (Ezek. 18:4). Nalishangaa kuona jinsi Shetani alivyoweza

kuwadanganya wanadamu hata waamini ya kwamba maana ya maneno haya ni kama kusema ya kwamba rohc ifanyayo dhambi haitakufa, bali itaishi milele katika maumivu makali. Malaika alisema, "Uzima ni uzima, ingawa ni kwa maumivu au furaha. Katika mauti hakuna maumivu, furaha, wala chuki."

Shetani aliwaambia malaika zake wafanye bidii kuueneza ule uongo ambao kwao alimdanganya Hawa katika Edeni, akisema, "Kufa hamtakufa." Na udanganyifu huu ulipokubaliwa na watu, wakiongozwa kuamini ya kwamba mwanadamu ana hali ya kutokufa, ndipo Shetani aliendelea kuwafanya kuamini ya kwamba mwenye dhambi ataishi katika maumivu ya milele. Ndipo njia ilipofunguliwa kwa Shetani na wajumbe wake kuwaonyesha watu ya kwamba Mungu ni mdhalimu mwenye kulipa kisasi, naye huwatupa katika Jehanum wale wasiompendeza na ya kwamba daima huwafanya waione ghadhabu yake; na wanapopata maumivu makali hivi, wakigaagaa katika moto wa milele, inasemwa ya kwamba Mungu huridhika moyoni akiwaona wakitaabika hivi. Shetani alijua ya kwamba kama watu wangekubali habari hii ya uongo, ndipo Mungu angechukiwa na wengi, badala ya kupendwa na kusujudiwa; tena wengine wengi wangefanywa kuamini ya kwamba maonyo ya Neno la Mungu yasingetimia kweli, kwani Mungu ni mkarimu mwenye upendo, na kuwapasha maumivu ya milele wale wanadamu aliokwisha kuwaumba kungekuwa tendo lililo mbali kabisa na tabia yake.

Jambo jingine la ajabu ni jinsi ambavyo Shetani amewafanya wanadamu waisahau kabisa haki ya Mungu na maonyo ya Neno lake na kusema ya kwamba Mungu ni mwenye neema, hata hakuna ye yote atakayepotea, bali

wote, watakatifu na wenye dhambi, mwisho wataokolewa katika ufalme wake.

Kwa ajili ya mafundisho ya uongo juu ya hali ya wanadamu ya kutokufa, na juu ya maumivu yasiyo na mwisho, ambayo yanakubaliwa na wingi wa watu, Shetani aweza kuongoza watu wengine kusema ya kwamba Biblia haikutoka katika pumzi ya Mungu. Watu hawa huona ya kwamba Biblia inafundisha mambo mengi yaliyo mema, lakini hawawezi kuyasadiki maneno yake, kwa kuwa wamefundishwa ya kwamba Biblia hutangaza mafundisho ya maumivu ya milele.

Kuna watu wengine tena ambao Shetani huwapotosha zaidi, hata kuwafanya kusema ya kwamba Mungu hayuko. Hawaoni unyofu wa tabia zake zilivyoelezwa katika Biblia, kama anaweza kuwaletea watu wengine maumivu makali milele hata milele. Kwa hivyo watu hawa huikana Biblia na Mwandishi wake, na kusema ya kwamba kifo ni usingizi wa milele.

Tena kuna watu wengine ambao ni waoga, wepesi kutishwa. Shetani anawashawishi wapate kutenda dhambi, na wakisha kufanya dhambi, ndipo Shetani huwafanya kufikiri ya kwamba mshahara wa dhambi si mauti, bali ni kuishi katika maumivu makali ambayo hawana budi kuyavumilia milele na milele. Kwa kuwatangazia watu habari hii ya vitisho juu ya mahali zinapoadhibiwa roho za watu milele na milele, ndivyo Shetani anavyowapotosha watu, hata na kuwafanya wapotewe na akili zao. Hapo ndipo Shetani na malaika zake husimanga, tena makafiri na watu wasioamini ya kwamba Mungu yuko, wanashirikiana pamoja katika kulaumu dini ya Ukristo. Hudai ya kwamba mabaya haya ni matokeo ya kuiamini Biblia na Mwandishi

wake, lakini kwa kweli yanatokea kwa ajili ya kusadiki mafundisho ya uongo yanayokubaliwa na wingi wa watu duniani.

### *Maandiko Matakatifu Ndiyo Kinga Yetu*

Naliona ya kwamba jeshi la mbinguni walighadhabika sana kwa ajili ya huu ukavu wa macho wa Shetani. Nalitaka kujua kwa sababu gani madanganyifu haya yaliruhusiwa kuwa na nguvu katika fikara za wanadamu hali malaika za Mungu ni wenye nguvu, na wakitumwa, wangeweza kumshinda adui kwa urahisi. Ndipo nikaona ya kwamba Mungu alijua ya kwamba Shetani angeitumia kila njia ambayo kwayo angeweza kumharibu mwanadamu; ndiyo maana Mungu aliamuru Neno lake liandikwe, na kuyafanya makusudi yake juu ya wanadamu kuwa dhahiri, hata mtu mdhaifu wa namna gani asikose kwa ajili ya kutojua. Mungu alipokwisha kumpa mwanadamu Neno lake, alililinda kwa uangalifu lisije likaharibiwe na Shetani na malaika zake, wala na ye yote katika wajumbe wake. Ingawa vitabu vingine vitaharibika, Biblia ilikusudiwa kudumu milele. Na katika siku za mwisho, madanganyifu ya Shetani yanapoongezeka, nakili za Biblia zingezidishwa kuwa nyingi hata mtu ye yote angeweza kupata nakili yake mwenyewe; na hivyo wangeweza kujivika silaha za Neno la Mungu wakajilinda na madanganyifu na ajabu za uongo wa Shetani.

Naliona ya kwamba Mungu alihifadhi Biblia kwa namna ya ajabu; na pengine nakili za Biblia zilipokuwa chache, watu wengine waliokuwa wameelimika waliyageuza maneno yaliyoandikwa humo, wakidhani ya kuwa waliidhihirisha maana yake zaidi, lakini kwa kweli wakayafumba

mambo yaliyokuwa dhahiri tayari, kwa sababu waliyafanya maneno yale yafuatane na maoni yao wenyewe ambayo yaliongozwa na mapokeo ya kibinadamu. Lakini naliona ya kwamba Neno la Mungu ni kama mnyororo uliokamilika, kiungo kimoja kikiungana na kiungo kingine na kuieleza maana yake. Watu wanaotafuta ukweli kwa makini hawana haja ya kukisia, kwa kuwa Neno la Mungu ni dhahiri na wazi kwa kumwonyesha mtu njia ya uzima, pia Roho Mtakatifu ametumwa kama mwongozi kwa kuwasaidia watu wapate kuifahamu njia ya uzima inayofunuliwa katika Biblia.

Naliona ya kwamba malaika za Mungu hawana ruhusa kutawala fikara za watu. Mungu ameweka mbele za mwanadamu uzima na kifo. Mwanadamu aweza kuchagua njia yake. Watu wengi wana hamu ya kuupata uzima, lakini wangali wakiendelea kuifuata njia iliyo pana. Wanachagua kuiasi mamlaka ya Mungu, ijapokuwa alionyesha upendo na rehema kuu kwa vile alivyomtoa Mwana wake wa pekee apate kufa kwa ajili yao. Wale wasiokubali kuuchagua wokovu ulionunuliwa na damu yenye thamani kuu, ni lazima wahukumiwe. Lakini naliona ya kwamba Mungu hatafunga mahali pa kutaabika milele, wala hatawachukua mbinguni; kwa kuwa kama wangepelekwa huko kuwa pamoja na watakatifu, wangetaabika zaidi. Lakini atawaharibu kabisa, na kuwafanya wawe kana kwamba hawakuwako; ndipo haki ya Mungu itatimizwa. Alimwumba mwanadamu kwa mavumbi ya nchi, na wakaidi na watu wasio safi wataateketezwa kwa moto na kurudi mavumbini tena. Naliona ya kwamba kwa ajili ya ukarimu na huruma ya Mungu katika jambo hili, inawapasa wote kumpenda na kulitukuza jina lake takatifu.

Baada ya kuharibiwa kwa waovu duniani, ndipo jeshi zima la mbinguni watasema, "Amina!"

Shetani hupendezwa kabisa na wale wanaojiita na jina la Kristo, na huku wanashikamana na madanganyifu yaliyoanzishwa naye Shetani. Kazi yake ingali ya kuyavumbua madanganyifu mapya, na uwezo wake na akili yake kwa kufanya hivi huongezeka kila mara. Aliwatilia mapapa na makasisi fikara ya kujivuna wakawataharakisha watu ili wawatese na kuwaangamiza wale waliokataa kuyafuata madanganyifu yake. Lo! maumivu na huzuni ya ajabu ambayo wafuasi wateule wa Kristo walilazimishwa kuyavumilia! Malaika wameyaandika mambo hayo yote yaliyotendeka. Shetani na malaika zake waovu wakasimanga wakiwaambia malaika wa Mungu waliowahudumia watu wale wa Mungu walioteswa ya kwamba watauawa wote, asipatikane Mkristo wa kweli hata mmoja duniani. Naliona ya kwamba kanisa la Mungu lilikuwa safi kabisa katika siku zile. Hakukuwako na hatari ya watu wenye mioyo michafu kuingia katika kanisa, kwa kuwa Mkristo wa kweli aliyethubutu kuisimamia imani yake alikuwa katika hatari ya kuteswa vikali, kuteketezwa moto, na kuadhibiwa kwa namna yo yote ambayo Shetani na malaika zake waliweza kutia katika fikara za wanadamu.

SURA YA KUMI NA NNE



# IMANI JUU YA KUONGEA NA MIZIMU

IMANI ya kwamba mwanadamu ana roho isiyoweza kufa imefanya njia tayari kwa dini ya siku hizi ya kuongea na mizimu. Ikiwa ni kweli ya kuwa wafu hukubaliwa kwenda mbele za Mungu na malaika watakatifu, na kupewa maarifa yanayozidi yale walivyokuwa nayo zamani, je, wasingeweza kurudi duniani kuwafundisha walio hai? Wale wanaoamini ya kama wanadamu wanaendelea kuishi peponi baada ya kufa, wanawezaje kukataa mafundisho ya uongo yanayokuja kwao kama ni nuru ya Mungu inayoletwa na pepo zilizotukuzwa? Hapa kuna njia ambayo watu hudhani ya kwamba ni takatifu lakini hutumiwa na Shetani ili ayatimize makusudi yake. Malaika waovu wanaofanya mapenzi ya Shetani huonekana kuwa ni wajumbe watokao kuzimuni. Hapo Shetani anapojidai ya kwamba anawawezesha walio hai kuzungumza na wafu, ndipo anapotumia uwezo wake wa giza kwa kuwadanganya katika fikara zao.

Shetani ana uwezo hata kufanya watu watokewe na mifano ya rafiki zao waliokwisha fariki. Mfano huu ni kamili; maneno na sauti huigizwa sawasawa. Wengi hufarijiwa kwa kuamini ya kwamba wapenzi wao wamo katika hali ya heri mbinguni, na bila kutambua ya kwamba wamo hatarini kusikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani.

Watu wanapokwisha kuongozwa kuamini ya kwamba wafu hurudi kweli na kuongea nao, Shetani huwafanya watokelewe na wale walioshuka kaburini pasipo kuwa tayari kumlaki Mungu. Hao nao huanza kujidai ya kwamba wako katika hali ya heri mbinguni, na ya kwamba wana madaraka ya heshima huko, na hivi fundisho la uongo huenezwa ya kwamba hakuna tofauti baina ya wenye haki na waovu. Wadanganyifu hawa wanaojidai kwamba hutoka kuzimuni pengine huleta maonyo na mashauri yaonekanayo kuwa ni ya kweli. Ndipo wakisha kuwavuta watu wawasadiki, huanza kuleta mafundisho yanayoharibu imani ya watu katika Maandiko Matakatifu. Kwa kuonekana ya kwamba hujishughulisha sana kwa mambo mema ya wenzao hapa duniani, hueneza mafundisho mabaya sana. Kwa jinsi ambavyo mara nyingine husema yaliyo kweli, na mara nyingine wanaweza kuyabashiri mambo yajayo maneno yao huonekana kuwa ya maana na mafundisho yao ya uongo hukubaliwa na watu wengi mara moja na kuaminiwa kabisa kana kwamba ni kweli ya Mungu sawa na mambo makubwa matakatifu ya Biblia. Sheria ya Mungu haifuatwi, roho ya neema hudharauliwa, na damu ya agano huhesabiwa kuwa kitu kisicho kitakatifu. Pepo hukana kabisa ya kwamba Kristo si Mungu, hata humhesabu Muumbaji kuwa sawa nao. Hivi kwa hila nyingine, mwasi mkuu huendelea kufanya vita vile na Mungu alivyoanzisha mbinguni na kufanya duniani tangu miaka elfu sita.

Watu wengi hujaribu kueleza sababu ya maonyesho ya uwezo wa pepo wakisema ya kwamba hufanyika kwa hila au kwa matendo ya kiinimacho yanayofanywa na yule kijumbe wa pepo. Ingawa ni kweli ya kama mara nyingine watu wapata kudanganywa ya kuwa matendo ya kiini-

macho ndiyo maonyesho hakika ya pepo, lakini kumekuwa na matendo mengine ambayo yameonekana dhahiri kwamba yametendeka kwa uwezo usio wa kibinadamu. Mabisho ya ajabu iliyokuwa mwanzo wa dini ya siku hizi ya kuamini juu ya kuongea na mizimu haikufanywa na werevu na hila ya kibinadamu, lakini ni matendo halisi ya malaika waovu, na kwa tendo lile walianzisha fundisho ambalo limewadanganya watu wengi na kuwaharibu. Wengi watashikwa kwa ajili ya kuamini ya kama nguvu za pepo ni ujanja wa wanadamu tu; na kama wakiona maonyesho na matendo ya pepo, mambo ambayo hawana budi kukubali ya kwamba yametendeka na nguvu isiyo ya kibinadamu, watadanganywa na kuamini ya kwamba mambo hayo yalifanywa na uwezo mkuu wa Mungu.

Watu hawa hawafikiri jinsi Maandiko Matakatifu yasemavyo juu ya maajabu yafanywayo na Shetani na wafanyi kazi wake. Waganga wa Farao waliyaigiza matendo ya Mungu kwa usaidizi wa Shetani. Mtume Yohana, akieleza uwezo wa kuifanya miujiza katika siku za mwisho, asema hivi: "Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya." Ufunuo 13:13,14. Hapa hatuambiwi juu ya ujanja tu. Wanadamu wanadanganywa kwa miujiza ambayo wafanyi kazi wa Shetani wanawezeshwa kuifanya, si mambo tu ambayo wanajisingizia ya kuwa wanaweza kuyafanya.

### *Uchawi wa Namna ya Kisasa*

Jina hasa la uchawi linadharauliwa siku hizi. Habari inayosema ya kwamba wanadamu wanaweza kuongea

na pepo wachafu inafikiriwa kuwa hadithi ya Zama za Giza. Lakini imani hii juu ya kuongea na mizimu (yaani Spiritualism), inayofuatwa na watu maelfu, naam, watu milioni nyingi, na ambayo imepata nafasi ya kupenya katika mambo ya elimu, na ambayo imeingia hata katika makanisa, tena inapendelewa na watu wa baraza kuu na katika majumba ya wafalme—udanganyifu mkubwa huu wa siku hizi sio jambo la kigeni hasa, lakini ni kuamsha kwa namna nyingine uchawi ule ule uliolaumiwa na kukatazwa katika siku za kale.

Shetani huwadanganya watu siku hizi kama vile alivyomdanganya Hawa katika bustani ya Edeni, kwa kuichochea tamaa ya kupata ujuzi isiyo halali yake. Shetani asema "Mtafumbuliwa macho nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya." Mwanzo 3:5. Lakini ujuzi unaoletwa na ile dini ya kuamini pepo ndiyo ile iliyosimuliwa na mtume Yakobo: "Hekima hiyo siyo ile ishukayo kutoka juu, bali ni ya dunia, na ya tabia ya kibinadamu, na Shetani." Yakobo 3:15.

Mkuu wa giza yu mwenye akili nyingi, naye huleta majaribu ya hila akigeuza majaribu na kuyafanyiza kufaa kwa kuwashika watu wa kila namna, wenye daraja na hali na uwezo mbali mbali. Hutumia "madanganyo yote ya udhalimu" ili kuwatawala wanadamu, lakini hawezi kuyatimiza mapenzi yake kwao ila tu kama wakikubali kushindwa na majaribu yake. Wale wanaojitia chini ya utawala wake kwa kuyaendeleza matendo yao mabaya na kukuza tabia zao zilizo mbaya, hawawezi kuufahamu mwisho wa mwenendo wao. Yule mwovu huwaharibu kabisa, ndipo huanza kuwatumia kwa kuwaharibu watu wengine pia.

Lakini hakuna ambaye hana budi kudanganywa na madai ya udanganyifu ya imani ya kuongea na mizimu (Spiritualism). Mungu ameutoa mwanga kwa walimwengu kutosha kuwadhihirishia madanganyo haya. Hata kama ushuhuda mwingine usingekuwako, kuna neno moja ambalo lingetosha Wakristo, ndilo linalosemwa ya kwamba pepo hawaweki tofauti yo yote kati ya wema na uovu, hata ya wanafunzi wanyofu wa Kristo na watumishi wabaya mno wa Shetani. Kwa Kuonyesha ya kwamba mtu aliye mwovu kabisa yuko mbinguni, na ya kwamba ameadhimishwa huko, kwa kweli ni kama Shetani huwatangazia walimwengu neno hivi: Haidhuru ukiwa mwovu wa namna gani; haidhuru kama unamwamini Mungu na Biblia au sivyo. Waweza kuishi maisha kama upendavyo; mbinguni makao yako.

Hata mitume, kama wakiigizwa na pepo hawa wa uongo, wanaonyeshwa kana kwamba wanayakanusha maneno waliyoyaandika kwa maongozi ya Roho Mtakatifu walipokuwa hapa duniani. Hukana ya kwamba Biblia ni Neno Takatifu la Mungu, na hivi huuondoa msingi wa tumaini la Wakristo na huizimisha taa inayoangaza njia iendayo mbinguni.

Shetani anawafanya walimwengu waamini ya kwamba Biblia ni kitabu cha hadithi zilizobuniwa tu, au ya kwamba ni kitabu kilichofaa kusomwa na mataifa ya zamani, lakini kwa sasa inafaa kuheshimiwa kidogo tu, ama kufikiriwa kuwa kitu cha zamani kisichotumika siku hizi. Na badala ya Neno la Mungu Shetani huleta maonyesho ya mizimu. Hapa ndipo njia inayokuwa chini ya utawala wake kabisa; kwa namna hii anaweza kuwafanya watu waamini juu ya mambo yo yote apendavyo. Kile Kitabu kitakacho-

mhukumu Shetani na wafuasi wake hukiweka gizani, kipate kudharauliwa jinsi atakavyo; na humfanya Mwokozi wa wanadamu asiwe na tofauti na mtu ye yote duniani. Na kama vile askari wa Kirumi waliolinda kaburi la Yesu walivyoeneza habari za uongo kama walivyoambiwa na makuhani na wakuu ili kuikanusha habari ya ufufuo wa Yesu, hivyo ndivyo ambavyo wale wanaoamini juu ya maonyesho ya mizimu wanavyowadanganya watu ya kwamba hakuna mambo ya ajabu wala mwujiza katika maisha ya Mwokozi wetu. Baada ya kumdharau Yesu hivi, huanza kuwatazamisha watu miujiza yao wenyewe wakisema ya kwamba miujiza hii huishinda ile iliyofanywa na Kristo.

Nabii Isaya asema hivi: "Na wakati watakapokuambia, Tafuta habari kwa watu wenye pepo na kwa wachawi; waliao kama ndege na kunong'ona; je! haiwapasi watu kutafuta habari kwa Mungu wao? waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai? Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi" Isaya 8:19, 20. Kama wanadamu wangekubali kuupokea ukweli unaoelezwa dhahiri katika Biblia, ya kwamba wafu hawajui kitu, ndipo wangeweza kuyaona maneno na maonyesho ya pepo kwamba ni kutenda kwake Shetani kwa uwezo na ishara na ajabu za uongo. Lakini kwa kuwa ni vigumu kwao kuacha kufuata mapenzi yao ya nia ya mwili, wasitake kujitenga na dhambi ambazo wanapenda kuzifanya, wingi wa watu wameyafumba macho yao wasione nuru; tena wanaendelea mbele bila kujali maonyo, wakati Shetani anapoweka tanzi lake la kuwategea, hao nao hushikwa naye. "Kwa sababu hawakubali kuipenda ile kweli, wapate ku-

okolewa," kwa hiyo "Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo." 2 The. 2:10, 11.

Wale wanaoyakataa mafundisho juu ya kuongea na mizimu (Spiritualism), si kwamba wanashindana na wanadamu tu, bali wanashindana na Shetani mwenyewe na malaika zake. Wameingia katika vita juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza la ulimwengu huu, na juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Shetani hataacha nafasi hata kidogo asipofukuzwa na uwezo wa wajumbe watokao mbinguni. Inawapasa watu wa Mungu kuwa tayari kumkabili kama Mwokozi wetu alivyomkabili na maneno haya, "Imeandikwa." Hata sasa Shetani anaweza kuyataja mafungu ya Biblia kama alivyofanya katika siku za Kristo, naye atayageuza vibaya mafundisho ya Biblia ili yapate kulingana na madanganyifu yake. Lakini maneno yaliyoandikwa dhahiri katika Biblia yanakuwa silaha za kutosha kushinda katika kila shindano.

Wale ambao watasimama imara katika siku za taabu, inawapasa kufahamu ushuhuda wa Maandiko juu ya hali ya wanadamu na hali ya wafu jinsi ilivyo, kwa kuwa baada ya siku si nyingi watu wengi watafikiwa na pepo za mashetani wanaojifanya kuwa ni jamaa zao au rafiki zao waliokufa, wakiwatangazia mafundisho mabaya ya uzushi. Roho hizi za mashetani watatuvuta roho kwa kutuonyesha na kutuambia mambo ambayo tunajishughulisha nayo, na watafanya miujiza ili kuyathibitisha madanganyifu yao. Inatupasa kuwa tayari kuwashinda kwa ukweli wa Neno la Mungu ya kwamba wafu hawajui kitu, na ya kwamba wale wanaojitokeza hivyo ni roho za mashetani.

Kwa muda mrefu sana Shetani amekuwa akijitayarisha kwa jitihada yake ya mwisho kwa kuwadanganya walimwe-

ngu. Msingi wa udanganyifu wake uliwekwa na maneno hayo aliyomwambia Hawa: "Hakika hamtakufa. . . . siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya." Mwanzo 3:4, 5. Punde kwa punde ameitayarisha njia yake kwa kazi hii kuu kwa kuaminisha watu juu ya kuongea na mizimu. Hajayatimiza maazimio yake yote bado; lakini atayatimiza katika siku za mwisho kabisa, na wanadamu watatumbukizwa katika mambo haya ya udanganyifu. Kwa upesi sana watu wanatulizwa roho ya kwamba wa salama, na huku wako hatarini; lakini hawataamshwa ila na mmiminiko wa ghadhabu ya Mungu.



SURA YA KUMI NA TANO

# SAUTI KUU

NILIWAONA malaika wakiruka huko na huko mbinguni, wakishuka duniani, na tena wakipanda mbinguni, wakifanya mambo tayari kwa utimizo wa tokeo fulani lililo kuu. Tena nikamwona malaika mwingine mwenye mamlaka kuu aliyetumwa ashuke duniani, kusudi aiunganishe sauti yake na ya malaika wa tatu, akatie nguvu na uwezo kwa ujumbe wake. Malaika yule alipewa uwezo mkuu na utukufu, aliposhuka, dunia iliangazwa na utukufu wake. Mwanga uliomfunika malaika huyu ulipenyeza pote alipolia kwa nguvu kwa sauti kuu, "Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza." Ufunuo 18:2

Ujumbe huu juu ya kuanguka kwa Babeli, jinsi ulivyotolewa na malaika wa pili, umerudiwa hapa, na pia yametajwa mabaya ambayo yamekuwa yakiingia makanisani tangu 1844. Kazi ya malaika huyu imeanzishwa kwa wakati uliofaa na kuungana na kazi kuu ya ujumbe wa malaika wa tatu unapotolewa kwa sauti kuu. Na hivi watu wa Mungu wanatayarishwa wapate kusimama wakati wa majaribu, ambayo yatawapata baada ya siku si nyingi. Naliiona nuru kuu ikiwakalia, wakaungana pamoja kwa kuutangaza ujumbe wa malaika wa tatu kwa ushujaa.

Malaika wengine walitumwa wapate kumsaidia malaika yule mwenye mamlaka kuu, aliyetoka mbinguni, tena

nalisikia sauti iliyokuwa ikienea pote ikisema hivi: "Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake." Ufunuo 18:4, 5. Ujumbe huu ulionekana ya kwamba uliongezwa juu ya ujumbe wa tatu, ukiungana nao kama vile kilio cha usiku wa manane kilivyoungana na ujumbe wa malaika wa pili katika mwaka wa 1844. Utukufu wa Mungu uliwakalia watakatifu waliovumilia wakingoja, nao wakalitoa onyo la mwisho kwa ushujaa, wakilitangaza anguko la Babeli, na kuwaita watu wa Mungu watoke kwake, kusudi waepukane na hukumu yake ya kutisha.

Mwanga ule uliowakalia wale waliokuwa wakimngoja Bwana ulipenyeza na kumulika pote, na wale waliokuwa katika makanisa yaliyopata nuru yo yote, na ambao hawakusikia na kuzikataa habari zilizoletwa na malaika watatu, watu kama hao waliuitikia wito, wakatoka katika makanisa yale yaliyoanguka. Wengi walikuwa wamepata umri wa watu wazima na kupata kufahamu mambo zaidi tangu malaika wa kwanza, wa pili na wa tatu walipoanza kutoa habari zao, nao sasa walipewa nuru, na walikuwa na nafasi ya kuchagua uzima au kifo. Wengine walichagua uzima, wakasimama pamoja na wale waliokuwa wakimtazamia Bwana wao na kuzishika amri zake zote. Ujumbe wa tatu ulipaswa kuitimiza kazi yake; na wote walijaribiwa na maneno ya ujumbe ule, na waliokuwa wenye haki walitoka katika dini mbali mbali.

Uwezo uliotoka juu uliwabidisha waaminifu, na huku maonyesho ya uwezo wa Mungu uliwatia hofu jamaa na rafiki zao wasioamini, na kuwashika wasithubutu kuwazuia wale ambao waliona ya kwamba walishurutishwa na Roho

wa Mungu waifanye kazi yake. Wito wa mwisho ulipelekwa hata kwa watumwa maskini; na wale waliokuwa wakimcha Mungu kati yao waliimba kwa furaha na shangwe kuu wakitazamia kuokolewa kwao.* Matajiri hawakuweza kuwazuia; walishikwa na woga na mshangao. Miujiza ya ajabu ilifanywa, wagonjwa waliponywa, na waaminio walifanya ishara na maajabu mengi. Mkono wa Mungu ulikuwa kazini, na bila kuwa na hofu ya matokeo yake watakatifu wote waliyafuata maoni ya dhamiri zao, wakaungana na wale waliokuwa wakizishika amri zote za Mungu; na kwa uwezo mkuu waliueneza ujumbe wa malaika wa tatu. Naliona ya kwamba ujumbe huu utakoma kwa nguvu na uwezo unaozidi ule wa kilio cha usiku wa manane.

Watumishi wa Mungu, wakijaa uwezo uliotoka juu na nyuso zao ziking'aa, wakajitoa kabisa kwa Mungu, waliondoka wautangaze ule ujumbe uliotoka mbinguni. Watu waliokuwa wametawanyika katika dini mbali mbali, waliuitikia wito ule, na wateule wa Mungu walitoka mara katika makanisa yale yaliyohukumiwa, kama Luti alivyoondoshwa hima kutoka katika Sodoma kabla ya kuharibiwa kwake. Watu wa Mungu waliongezewa nguvu, na utukufu mkuu uliowafunika kwa wingi ukawatayarisha wapate kuvumilia katika wakati wa majaribu. Kila mahali nalisikia sauti za watu wengi wakisema hivi: "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu; hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Ufunuo 14:12.

* Twajua ya kwamba itakuwako hali ya utumwa wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili, kwa vile Yohana alivyosema katika kitabu cha Ufunuo 6:15, 16, akisimulia ya kwamba "kila mtumwa, na mwungwana" wataiambia milima na miamba iwaangukie na kuwasitiri "mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi."



SURA YA KUMI NA SITA

# MWISHO WA REHEMA

NALIONYESHWA wakati wa mwisho wa ujumbe wa malaika wa tatu. Uwezo wa Mungu uliwakalia watu wake; walikuwa wameimaliza kazi yao, na walikuwa tayari kwa wakati wa taabu uliokuwa ukiwajia. Walikuwa wameisha pata mvua ya masika, yaani kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana, na ushuhuda wa milele ulikuwa umeamshwa. Onyo kuu la mwisho lilikuwa limetangazwa kila mahali, nalo lilikuwa likiwashtusha na kuwakasirisha wakaao duniani ambao hawakuukubali ujumbe huo.

Naliwaona malaika wakiruka kwa haraka wakienda huko na huko mbinguni. Malaika mmoja mwenye kidau cha mwandishi kiunoni alirudi toka duniani akamwambia Yesu ya kwamba kazi yake ilikuwa imekwisha, na watakatifu wamehesabiwa wakatiwa muhuri. Ndipo nikamwona Yesu, ambaye alikuwa akihudumu mbele ya sanduku zilimokuwamo amri za Mungu, akitupa chini chetezo cha uvumba. Aliinua mikono yake, na kwa sauti kuu alisema, "Imetimia." Na jeshi la malaika waliziondoa taji zao walipoyasikia maneno haya mazito yakitoka kinywani mwa Yesu: "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki

na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa." Ufunuo 22:11.

Kesi ya kila mtu ilikuwa imeisha katwa, kwa uzima au kwa kufa. Yesu alipokuwa akihudumu katika patakatifu, hukumu ya wenye haki waliokufa ndiyo iliyokuwa ikifanyika, na ndipo baadaye ikafuata ya wenye haki walio hai. Kristo alikuwa ameupokea ufalme wake, baada ya kuufanya upatanisho kwa watu wake na kuzifuta dhambi zao. Hesabu ya raia za ufalme ule ilitimizwa. Arusi ya Mwana-Kondoo ilifungwa. Na ufalme ule na ukuu wa ufalme chini ya mbingu walipewa Yesu na warithi wa wokovu; na Yesu akaanza kumiliki kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

Yesu alipokuwa akitoka katika patakatifu mno, nalisikia mlio wa njuga katika joho lake; na alipoondoka, watu wakaao duniani wakafunikwa na wingu la giza. Ndipo hapakuwa na mpatanishi kati ya mwanadamu mwenye dhambi na Mungu aliyekosewa. Yesu alipokuwa akisimama kati ya Mungu na mwanadamu mwenye dhambi, wanadamu walikuwa wakizuiliwa wasifanye maovu wapendavyo; lakini Yesu alipoondoka kati ya wanadamu na Baba yake, hapakuwa na kizuizi tena, na Shetani akawa na mamlaka kabisa juu ya wale ambao mwishoni walikataa kutubu.

Haikuwezekana kuyamimina mapigo wakati Yesu alipokuwa akihudumu katika patakatifu; lakini kazi yake ikisha pale, naye aache kuwaombea wanadamu, hakuna jambo lo lote linaloweza kuizuia ghadhabu ya Mungu, nayo huanguka kwa ukali juu yao wenye dhambi wasio na mahali pa kukimbilia, ambao waliudharau wokovu na kuchukia kukaripiwa. Wakati ule wa kuogofya, kazi ya Yesu ikisha kukoma kama mwombezi wetu, watakatifu

wataishi mbele za Mungu mtakatifu bila mwombezi. Hukumu zote zitakuwa zimekatwa, na hesabu zote za wateule wa Mungu zitakuwa zimetimizwa. Nalimwona Yesu akikawia kidogo katika chumba cha nje cha patakatifu pa mbinguni, na dhambi zote zilizoungamwa alipokuwa katika patakatifu mno ziliwekwa juu ya Shetani, mwanzishaji wa dhambi, ambaye alipaswa kuhukumiwa kwa ajili ya dhambi.*

### *Kukawia! Kukawia!*

Ndipo nikamwona Yesu akiyavua mavazi yake ya ukuhani, akajivika mavazi ya kifalme kabisa. Kichwani mwake zilikuwako taji nyingi, taji moja juu ya taji nyingine. Alitoka mbinguni akizungukwa na jeshi la malaika. Mapigo yalikuwa yakiwaangukia watu duniani. Wengine walikuwa wakimkana Mungu na kumlaani. Wengine walienda upesi kwa watu wa Mungu, wakiwasihi wawaonyeshe jinsi wanavyoweza kuziepuka hukumu zake. Lakini watakatifu hawakuwa na msaada wo wote wa kuwapa. Hakuna machozi tena kwa ajili ya wenye dhambi, walikuwa wameombewa

* Maumivu haya ya Shetani si kwamba kufanya upatanisho kwa ajili ya wanadamu. Tukisoma katika sura fulani iliyopita, twaona ya kwamba "Kristo alikuwa badala ya wanadamu, ndiye mdhamini wa wanadamu, na dhambi zote za wanadamu zikawekwa juu ya Kristo." Lakini baada ya kuokolewa wale wanaokubali ile dhabihu ya Kristo, ni jambo la haki ili Shetani, mwanzishaji wa dhambi, na ataabike kwa hukumu ya mwisho. Jinsi Bibi White asemavyo mahali pengine, "Kazi ya upatanishi imalizikapo katika patakatifu pa mbinguni, ndipo dhambi za watu wa Mungu zitawekwa juu ya Shetani mbele za Mungu na malaika za mbinguni, na mbele ya kundi la waliookolewa; naye Shetani atatajwa kuwa ni mwenye hatia ya maovu yote ambayo aliwaongoza kuyafanya." —*The Great Controversy*, p. 658.

mara ya mwisho, mzigo wa mwisho ulikuwa umechukuliwa kwa ajili yao, na onyo la mwisho lilikuwa limekwisha kutolewa. Hakuna sauti ya rehema iliyoweza kuwaita tena, wakati ambapo watakatifu na jeshi zima la mbinguni walikuwa wakijishughulisha na wokovu wao, wao wenyewe hawakujishughulisha kamwe ili wapate kuokoka. Uzima na mauti yalikuwa yamewekwa mbele yao kusudi wachague. Wengine walikuwa na hamu ya kuupata uzima, lakini hawakujitahidi kuupata. Hawakuchagua uzima, na sasa damu haikupatikana ya kuwatakasa wenye hatia hakuna tena Mwokozi mwenye rehema atakayewaombea akisema, "Waachie, waachie wenye dhambi muda kitambo tena." Jeshi zima la mbinguni liliungana na Yesu walipoyasikia maneno haya, "Imetimia. Imekwisha." Azimio la wokovu lilikuwa limetimia, lakini wachache tu waliochagua kuupokea wokovu ule. Na sauti nzuri ya rehema ilipofifia, waovu wakashikwa na woga na hofu kuu. Walisikia maneno haya yakisemwa kwa udhahiri sana, "Mmekawia! mmekawia ajabu!"

Wale ambao hawakulithamini Neno la Mungu walikuwa wakienda hima huko na huko, wakizungukazunguka toka nchi fulani mpaka nchi nyingine, na kutoka magharibi mpaka mashariki, wakilitafuta Neno la Mungu. Malaika akasema, "Hawatalipata Neno la Mungu wanalotafuta. Kuna njaa kuu duniani; wala si njaa ya chakula, wala kiu ya maji, bali ni njaa na kiu ya kuyasikia maneno ya Mungu. Wangekubali kutoa cho chote ili wapate kusikia neno lo lote la sifa kutoka kwa Mungu! lakini hapana; ni lazima waendelee kuisikia njaa na kiu. Siku kwa siku walikuwa wakidharau wokovu, wakihesabu mali na anasa za dunia kuwa ya thamani kuu zaidi ya hazina

na vitu vya kutamanisha vilivyo mbinguni. Wamemkataa Yesu na kuwadharau watakatifu wake. Inawapasa wachafu kuendelea kuwa wachafu milele."

Wingi wa waovu walikasirika sana walipoyasikia maumivu ya yale mapigo. Ulikuwa wakati wa maumivu makuu. Wazazi walikuwa wakiwalaumu watoto wao kwa ukali, na watoto kadhalika wakiwalaumu wazazi wao, tena ndugu na dada wakawa wakilaumiana. Vilio vya maombolezo vilisikika kila upande, wakisema, "wewe ndiwe uliyenizuia nisipate ukweli huu ambao ungeniokoa katika wakati huu wa hatari." Watu waliwageukia wahubiri wao wakiwachukia na kuwalaumu wakisema, "Ninyi hamkutuonya. Mlituambia ya kwamba watu wote wataongoka, mkapaaza sauti zenu mkisema, Amani, amani, kusudi mwitulize hofu yote tuliyokuwa nayo. Hamkutuambia juu ya wakati huu; na wale waliokuwa wakituonya juu ya wakati huu, mliwaita wazushi na waovu waletao dini za uongo, zilizoweza kutuangamiza." Lakini naliona ya kwamba wahubiri hawakuepukana na ghadhabu ya Mungu. Maumivu yao yalizidishwa mara kumi ya yale ya watu wao.



SURA YA KUMI NA SABA

# WAKATI WA TAABU YA YAKOBO

NALIWAONA watakatifu wakitoka katika miji na vijiji, wakiungana pamoja kwa makundi, wakienda kukaa katika hali ya upweke. Malaika waliwapa chakula na maji, lakini waovu waliumwa na njaa na kiu. Ndipo nikawaona wakuu wa dunia wakishauriana pamoja, na Shetani na malaika zake wakishughulika karibu nao. Naliiona barua fulani, ambayo nakili zake zilitawanywa katika nchi mbali mbali, ikitoa amri ya kwamba watakatifu wasipoacha imani yao iliyo maalum, kuacha kuishika Sabato na kuitunza siku ya kwanza ya juma, baada ya muda fulani watu watakuwa na ruhusa ya kuwaua. Lakini katika wakati huu wa taabu watakatifu walitulia na kuwa na amani rohoni, wakimwamini Mungu na kütegemea ahadi yake ya kwamba watapata njia ya kuokoka.

Katika nchi nyingine, waovu waliwarukia watakatifu ili kuwaua kabla ya siku ile iliyoagizwa; lakini malaika waliochukua mfano wa wanadamu waliwapigania watakatifu. Shetani alikuwa na hamu ya kuwa na uwezo wa kuwaharibu watakatifu wake Aliye Juu, lakini Yesu aliwaambia malaika zake wawalinde. Mungu angeheshimiwa mbele za washenzi waliowazunguka, kwa kulifanya agano na wale waliozishika amri zake; na Yesu angeheshimiwa

kwa kuwahamisha wale waaminifu waliokuwa wakimngoja kwa muda mrefu, wasione mauti.

Baada ya muda kitambo niliwaona watakatifu wakiona maumivu makuu mioyoni mwao. Walionekana wakizungukwa na waovu wa dunia. Kwa kadiri ilivyoonekana, walikuwa katika hali mbaya sana. Wengine walianza kuogopa ya kwamba labda Mungu amewaacha wapate kutaabishwa na waovu. Lakini kama macho yao yangalifunguliwa, wangaliona ya kwamba walizungukwa na malaika za Mungu. Ndipo kundi la waovu wakaja wamekasirika, na nyuma yao kundi la malaika watakatifu, wenye nguvu. Jambo hili halikuwezekana. Malaika za Mungu waliwafanya waovu warudi nyuma, hata na malaika waovu waliokuwa wakisongana karibu nao waliwafanya warudi nyuma.

*Kilio kwa Kupata Kuokolewa*

Wakati ule ulikuwa wakati wa maumivu makuu ya rohoni kwa watakatifu. Walimlilia Mungu mchana na usiku apate kuwaokoa. Kwa kadiri ilivyoonekana, haikuwezekana kwao kuokolewa. Waovu walikuwa wameanza kushangilia tayari, wakisema kwa sauti kuu, "Mbona Mungu wenu hawaokoi ninyi katika mikono yetu? Kwa nini hampandi juu mkayaokoe maisha yenu?" Lakini watakatifu hawakuwasikiliza. Walijitahidi katika kumwomba Mungu kama Yakobo alivyofanya. Malaika walikuwa na hamu ya kuwasaidia, lakini iliwapasa kungoja kidogo; ni lazima watu wa Mungu wanywe katika kikombe kile, na kubatizwa na ubatizo ule. Malaika, kwa jinsi walivyokuwa waaminifu kwa kazi yao, waliendelea kungoja. Mungu asingeacha jina lake lilaumiwe na washenzi. Wakati ulikuwa umewadia ambapo ilimpasa kuuonyesha uwezo wake na

kuwaokoa watakatifu wake kwa utukufu. Kwa ajili ya utukufu wa jina lake angewaokoa wote ambao walingoja wakimtazamia, na ambao majina yao yameandikwa katika kitabu. Nalionyeshwa mzee Nuhu aliyekuwa mwaminifu. Mvua iliponyesha na Gharika ilipokuja, Nuhu na jamaa zake walikuwa wameingia katika safina, na Mungu alikuwa amewaonya watu walioishi kabla ya gharika lakini walimdharau na kumcheka tu. Tena maji yaliposhuka duniani, na watu wakaanza kuzama mmoja mmoja, waliiona safina ile, waliyoichezea na kuifanyia mzaha, ikielea salama juu ya maji, ikiwaokoa Nuhu mwaminifu na watu wa nyumba yake. Kadhalika naliona ya kwamba watu wa Mungu, ambao kwa uaminifu waliwaonya watu wa dunia juu ya ghadhabu ya Mungu ijayo, wataokolewa. Mungu hatawaacha waovu wawaharibu wale wanaotazamia kuhamishwa duniani, na ambao walikataa kumsujudu mnyama na kuipokea alama yake. Naliona ya kwamba kama waovu wangeruhusiwa kuwaua watakatifu, ndipo Shetani na jeshi lake pamoja na wote wanaomchukia Mungu wangependezwa. Shetani angeshangilia ajabu kama katika vita vya mwisho angeweza kushinda wale ambao kwa muda mrefu wamemngoja Yule wanayempenda! Wale ambao wameidharau hali ya kupanda kwa watakatifu wa mbinguni, wataona utunzaji wa Mungu kwa watu wake, na wataona wokovu wao wa ajabu.

Watakatifu walipotoka katika miji na vijiji walikimbizwa na waovu, wakitaka kuwaua. Lakini panga zilizoinuliwa kwa kuwaua watu wa Mungu zilivunjika zikawa hazina nguvu kama nyasi. Malaika za Mungu waliwalinda watakatifu. Walipomlilia Mungu mchana na usiku, kilio chao kilifika mbele za Mungu.



SURA YA KUMI NA NANE

# KUOKOLEWA KWA WATAKATIFU

USIKU wa manane ndio wakati ambao Mungu aliuchagua kwa kuwaokoa watu wake. Waovu walipokuwa wakidhihaki, mara jua likaonekana, liking'aa kwa nguvu nyingi, na mwezi ulitulia. Waovu walishangaa walipokiona kioja kile, lakini watakatifu walifurahi walipoona dalili za kuokolewa kwao. Ishara na maajabu yakafuatana kwa upesi. Kila kitu kilionekana ya kwamba kimegeuzwa hali yake ya kawaida. Mito ilikoma. Mbingu zikatanda mawingu mazito na meusi yaliyogongana. Lakini kulikuwapo na mahali pamoja palipokuwa na utukufu na utulivu, mahali sauti ya Mungu ilipotokea kama sauti ya maji mengi, ikitikisa mbingu na nchi. Kulikuwako na tetemeko kuu la nchi. Makaburi yalifunguliwa, na wale waliokufa katika imani ya ujumbe wa malaika wa tatu, wakiitunza Sabato, waliondoka mavumbini wakiwa na utukufu, wapate kulisikia agano la amani ambalo Mungu alitaka kufanya na wale waliozishika amri zake.

Mbingu ilifunguliwa na kufungwa, na kulikuwako msukosuko. Milima ilitikisika kama mainzi inavyopeperushwa na upepo, na ikatupatupa miamba huko na huko. Bahari ilichemka kama mtungi, na ikayatupa mawe juu ya nchi kavu. Mungu alipokuwa akiitangaza siku na saa ya kuja kwa Yesu, na kutoa agano lake la milele kwa watu wake,

aliyatamka maneno machache, akanyamaza kidogo maneno yake yalipokuwa yakienea duniani pote. Watu wa Mungu walisimama na macho yao wameyakaza juu, wakiyasikiliza maneno yaliyokuwa yakitoka kinywani mwa Mungu, yakisikika duniani kama sauti kuu ya ngurumo. Ulikuwa wakati wa kutisha kabisa. Baada ya kila fungu la maneno ya Mungu, watakatifu walipaaza sauti zao wakisema, "Utukufu!" Halleluya!" nyuso zao ziliangazwa na utukufu wa Mungu, ziking'aa na utukufu kama uso wa Musa ulivyong'aa aliposhuka kutoka katika mlima wa Sinai. Waovu hawakuweza kuwatazama kwa ajili ya utukufu ule. Na wale waliomheshimu Mungu kwa kuitunza Sabato yake takatifu walipobarikiwa na mbaraka usio na mwisho, kukawa na shangwe kuu ya ushindi juu ya mnyama na sanamu yake.

Ndipo miaka ya furaha ikaanza, yaani miaka ya kupumzika kwa nchi.

Naliwaona watumwa waliomcha Mungu wakiondoka katika ushindi wakishangilia, wakiiondoa minyororo iliyowashika, na huku mabwana wao waovu walitatanishwa wasijue la kufanya, kwa maana waovu hawakuweza kuyafahamu maneno yaliyotoka kinywani mwa Mungu.

*Marejeo ya Yesu*

Mara likaonekana wingu kuu lililo jeupe, na juu yake aliketi Mwana wa Adamu. Wingu hili lilipoonekana kwa mbali, lilikuwa dogo sana. Malaika alisema ya kwamba lilikuwa ishara ya Mwana wa Adamu. Liliposhuka na kuzidi kukaribia dunia, tuliweza kuuona uzuri na utukufu kamili wa Yesu alipoondoka apate kushinda. Jeshi la malaika watakatifu wenye taji zing'aazo vichwani, wakafuatana naye.

Hakuna lugha yo yote inayoweza kusimulia fahari na utukufu wa mambo hayo jinsi yalivyo. Wingu lile la utukufu wa ajabu, ambalo lilikuwa jeshi la malaika watukufu, liliendelea kuikaribia dunia hata tuliweza kumwona Yesu mwenyewe dhahiri na uzuri wake. Hakuvaa taji ya miiba, bali taji ya utukufu ilikuwa kichwani mwake. Katika vazi lake na katika paja lake liliandikwa jina, Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana. Uso wake uling'aa kama mwangaza wa jua wakati wa adhuhuri, macho yake yalikuwa kama mwako wa moto, na miguu yake ilionekana kama shaba iliyo safi sana. Sauti yake ilisikika kama sauti za vinanda vingi. Dunia ilitetemeka mbele yake, mbingu zikaondolewa kama ukurasa ulivyokunjwa, na kila mlima na kisiwa kikahamishwa kutoka mahali pake. "Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na mwungwana, wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima, wakiiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yao, imekuja; naye ni nani awezaye kusimama?" Ufunuo 6:15-17.

Wale ambao muda kitambo kabla ya wakati ule walikuwa tayari kuwaharibu waaminifu wa Mungu duniani, sasa waliona wenyewe utukufu wa Mungu uliowakalia. Hao nao walipokuwa wanashikwa na hofu nyingi sana, walisikia sauti za watakatifu wakisema kwa furaha, "Huyu ndiye Mungu wetu, ndiye tuliyemngojea, atusaidie." Isaya 25:9.

### *Ufufuo wa Kwanza*

Sauti ya Mwana wa Mungu ilipowaita watakatifu wa-

liokuwa wamelala, dunia ilitetemeka kwa nguvu sana. Waliitikia wito wake, wakaondoka wamevikwa utukufu na hali ya kutokufa, wakashangilia wakisema, "Ushindi, ushindi, juu ya mauti na kuzimu! Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako? (Soma 1 Kor. 15:55). Ndipo watakatifu walio hai, pamoja nao waliofufuliwa wakapaaza sauti zao kwa namna ya shangwe na furaha kuu. Miili yote iliyozikwa makaburini ikiwa na alama ya maradhi na kifo sasa ilitoka makaburini ikiwa na afya njema na hali ya kutokufa. Watakatifu walio hai hugeuzwa mara, kufumba na kufumbua, na kuungana na wale waliofufuka, nao watamlaki Bwana wao pamoja angani. Kutakuwa kukutana kwa ajabu sana! Rafiki ambao walikuwa wametengwa kwa ajili ya kifo, sasa wataungana wasitengane tena.

Katika kila upande wa gari lile la wingu kulikuwa na mabawa, na chini yake kulikuwa na magurudumu yaliyo hai; na gari lilipopanda juu, magurudmu yale yalipaaza sauti na kusema, "Mtakatifu" na mabawa yalipokuwa yakienda, yalipaaza sauti yakisema, "Mtakatifu," na mafuatano ya malaika watakatifu waliozunguka lile wingu walipaaza sauti wakisema, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu wa Majeshi!" Na watakatifu waliokuwa katika lile wingu walipaaza sauti zao wakisema, "Utukufu, Alleluya!" Ndipo gari likapanda juu kwenye Mji Mtakatifu. Kabla ya kuingia mjini, watakatifu walipangwa katika mraba ulio kamili, na Yesu akisimama katikati. Naye akawapita wote kwa urefu, watakatifu hata na malaika, tangu mabega na kwenda juu. Umbo lake la utukufu na uso wake wa kupendeza uliweza kuonwa na wote waliokuwa katika mraba ule.





# UJIRA WA WATAKATIFU

HALAFU niliona jeshi la malaika wengi sana wakizileta taji za utukufu kutoka katika mji mtakatifu —taji moja kwa kila mtakatifu, na jina lake limeandikwa juu yake. Yesu alipoziagiza taji, malaika walizileta kwake, naye kwa mkono wake wa kulia aliziweka vichwani mwa watakatifu. Vile vile malaika walivileta vinanda na Yesu alivigawa kwa kila mtakatifu. Malaika wenye cheo cha juu waliongoza kwa kupiga vinanda, ndipo sauti zote zikainuliwa kwa sifa na shukrani, na kila mkono ukaanza kuzinyakua nyuzi za vinanda, kama wajuzi kamili wa muziki, vikatoa sauti tamu na za kupendeza.

Ndipo nikamwona Yesu akiwaongoza wale waliookolewa kwenye mlango wa mji. Aliushika mlango akaujongeza nyuma kwa pata zake zilizokuwa zikíng'aa, akawaambia mataifa yote yaliyozishika amri zake waingie ndani. Kila kitu kilichokuwa mjini kilikuwa cha kupendeza macho. Utukufu mwingi ulionekana kila mahali. Ndipo Yesu akawaangalia watakatifu wake waliookolewa; nyuso zao ziling'aa kwa utukufu; naye alipokaza macho ya upendo juu yao akasema kwa sauti yake iliyo tamu: "Nayaona masumbufu ya moyo wangu, na nimeridhika. Utukufu huu wa ajabu ni wenu, nanyi mtaufurahia milele. Huzuni zenu zimekoma. Haitakuwako mauti tena, wala maombolezo,

wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena" Naliwaona waliokolewa wakiinama wakizitupa taji zao miguuni pa Yesu, na alipowainua kwa mkono wake wa upendo, wakavichukua vinanda vyao vya dhahabu wakazijaza mbingu na sauti tamu ya muziki wakimwimbia Mwana-Kondoo.

Baadaye nikamwona Yesu akiwaongoza watu wake kwenye mti wa uzima, na tukasikia tena sauti yake ya kupendeza, sauti nzuri zaidi ya sauti yo yote ambayo wanadamu wamepata kuisikia, akisema, "Majani ya mti huu yatakuwa kwa kuwaponya mataifa. Mnaruhusiwa kuyala yote." Mti wa uzima ulizaa matunda mazuri ajabu, ambayo watakatifu waliruhusiwa wayale kwa wingi, katika mji kulikuwa na kiti cha enzi cha Mungu, ulipotoka mto wa maji ya uzima, yaliyokuwa safi kama kioo. Kila upande wa mto huu kulikuwa na mti wa uzima, na katika kingo za mto huu kulikuwa na miti mingine mizuri iliyokuwa na matunda ambayo pia yalikuwa matamu kwa chakula.

Lugha za kibinadamu hazitoshi hata kujaribu kusimulia jinsi mbingu ilivyo. Kama nikiwaza mambo haya jinsi nilivyoonyeshwa, nashangaa kabisa. Nikivutwa moyoni kwa ajili ya utukufu ule na fahari ya ajabu, naiweka kalamu chini, nikisema, "Lo, si upendo huu! wa ajabu kabisa!" Lugha iliyo bora zaidi duniani haiwezi kuusimulia utukufu wa mbinguni na upendo usiokadirika wa Mwokozi wetu.



# MIAKA ELFU

NALIONYESHWA dunia tena. Waovu walikuwa wameharibiwa, na maiti zao zilikuwa zikitapakaa usoni pa dunia. Ghadhabu ya Mungu ilikuwa imeminwa juu ya watu wakaao duniani kwa mapigo saba ya mwisho, nao wakalazimishwa kuzitafuna ndimi zao kwa ajili ya maumivu, na walikuwa wakimtukana Mungu. Wachungaji wa uongo ndio ambao ghadhabu ya Mungu ilikuwa kali zaidi juu yao. Macho yao yalikuwa yamedhoofika katika vitundu vyao, vivyo hivyo na ndimi zao midomoni mwao wakati walipokuwa wanasimama kwa miguu yao. Watakatifu walipokwisha kuokolewa kwa sauti ya Mungu, ndipo umati wa waovu wakaanza kufanyiana ukali wao kwa wao. Dunia ilionekana kwamba imegharikishwa na damu, na maiti ilionekana kutoka upande mmoja wa dunia mpaka upande mwingine.

Dunia ilionekana kuwa jangwa la ukiwa kabisa. Miji na vijiji, kwa vile vilivyobomolewa na tetemeko la nchi, vikawa mafungu mafungu. Milima ilikuwa imehamishwa kutoka mahali pake, ikiacha mapango makubwa mahali ilipotoka. Miamba iliyopasuka, iliyotupwa kutoka baharini, au iliyobomoka yenyewe kutoka usoni pa dunia, ilitapakaa huko na huko usoni pa nchi. Miti mikubwa ilikuwa imeng'olewa na kutawanywa juu ya nchi. Hapa ndipo pata-

kapokuwa makao ya Shetani na malaika zake kwa miaka elfu. Hapa ndipo atakapokuwa kama mfungwa, akitembea huku na huko juu ya uso wa dunia iliyobomoka apate kuyaona matokeo ya uasi wake kwa Mungu na sheria yake. Kwa miaka elfu atayaona mazao ya laana ambayo aliileta duniani.

Kwa jinsi atakavyokuwa akifungwa duniani yeye peke yake, hatakuwa na ruhusa ya kwenda katika sayari nyingine apate kuwajaribu na kuwasumbua wale ambao hawakuanguka dhambini. Wakati huu Shetani atataabika vibaya sana. Tangu kuanguka kwake, tabia zake za uovu zimezoezwa juu ya wanadamu. Lakini wakati ule atanyang'anywa uwezo wake naye ataachwa peke yake apate kuyawaza mambo ambayo alikuwa ameyatenda tangu kuanguka kwake, na apate kutazamia kwa hofu na kutetemeka mambo ya kuogofya yatakayompata mbeleni, atakapoadhibiwa kwa ajili ya maovu yote aliyokwisha kuyatenda, na kwa ajili ya dhambi ambazo aliwashawishi wengine wakazitenda.

Nalisikia sauti za shangwe za malaika na za watakatifu waliookolewa, sauti zilizofanana na vilio vya vinanda elfu kumi, kwa kuwa haitawezekana kwao kujaribiwa wala kuudhiwa tena na Shetani, na kwa kuwa wenyeji wa sayari nyingine walilindwa asiwaendee na kuwajaribu.

Ndipo nikaona viti vya enzi, na Yesu na watakatifu waliookolewa waliketi juu ya viti vile; na watakatifu walimiliki kama wafalme na makuhani kwa Mungu. Kristo, pamoja na watu wake, aliwahukumu waovu waliokuwa wamekufa, akiyalinganisha matendo yao na Kitabu cha Sheria, yaani Neno la Mungu, na akikata kila hukumu kwa jinsi matendo ya kimwili yalivyo. Halafu wakawa-

pimia waovu hukumu iliyowapasa kupata kwa namna ya matendo yao, na hukumu zote ziliandikwa juu ya majina yao katika kitabu cha mauti. Shetani pia, pamoja na malaika zake walihukumiwa na Yesu na watakatifu. Shetani alipaswa kupata adhabu kali zaidi ya watu ambao aliwadanganya. Adhabu yake haina budi kuwa kali zaidi hata isiweze kulinganishwa na adhabu ya wengine. Baada ya kufa kwa wale aliokwisha kuwadanganya, Shetani aliachwa apate kuishi akiendelea kuyasikia maumivu kwa muda mrefu zaidi.

Hukumu ya waovu ilipokwisha, mnamo mwisho wa miaka elfu, Yesu alitoka katika mji, na watakatifu pamoja na mwandamano wa malaika walimfuata. Yesu alishuka kwenye mlima mkubwa, na mara ile miguu yake ilipougusa mlima ule, mlima ulipasuka vipande viwili ukawa uwanja mkuu. Ndipo tukaangalia juu tukauona mji mzuri ule ulio mkuu, uliojengwa juu ya misingi kumi na miwili, na milango kumi na miwili, milango mitatu kila upande, na malaika mmoja katika kila mlango. Tulipaaza sauti zetu tukisema, "Mji ule! mji mkuu! Unashuka chini kutoka kwa Mungu mbinguni!" Mji ule ukashuka chini kwa fahari yake ya utukufu unaoshangaza, ukatua juu ya uwanja ule mkubwa uliokuwa umetayarishwa na Yesu.



SURA YA ISHIRINI NA MOJA

# UFUFUO WA PILI

BAADAYE Yesu na mafuatano ya malaika watakatifu, na watakatifu wote waliookolewa, waliondoka katika mji. Malaika walimzunguka Amiri Mkuu wao, wakamwandama alikokwenda, na mafuatano ya watakatifu waliookolewa nyuma. Ndipo kwa utukufu wa ajabu na wa kuogofya, Yesu aliwaita waovu waliokufa; waliondoka katika makaburi wakiwa na miili yenye hali ile ya unyonge na ugonjwa jinsi walivyokwenda makaburini. Jambo la kutisha! Jambo la ajabu kweli! Katika ufufuo wa kwanza wote waliondoka katika hali ya kutokufa, lakini katika ufufuo wa pili alama za laana zinaonekana kwa wote. Wafalme na wakuu wa dunia, wanyonge na watu duni, watu walioelimika na wasioelimika, wote huondoka pamoja. Wote humwona Mwana wa Adamu; na wale hasa ambao walimdharau na kumdhihaki, waliomwekea taji ya miiba kichwani na kumpiga na mwanzi, wote humwona katika utukufu wake wa kifalme. Wale waliomtemea mate wakati wa hukumu yake sasa hugeuka wasione macho yake na utukufu wa uso wake ambao unawapenyeza moyo. Wale waliomchoma mikono na miguu kwa misumari sasa huzitazama alama za kusulibishwa kwake. Wale waliomchoma ubavu kwa mkuki huona alama za ukali wao mwilini mwake. Watajua ya kwamba yeye ndiye yule ambaye

walimsulibisha na kumdhihaki katika maumivu yake ya kukata roho. Hapo ndipo kutakuwa kilio cha huzuni kuu, wakikimbia na kujificha kutoka mbele za Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

Wote wanataka kujificha chini ya miamba, hutaka kujificha wasiuone utukufu wa kuogofya wa Yeye ambaye zamani walimdharau. Na wakishindwa na kuchomwa moyo na utukufu wake mkuu walipaaza sauti zao kwa moyo mmoja, na kwa sauti inayosikika wazi wakisema, "Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana."

Ndipo Yesu na malaika watakatifu, wakifuatana na watakatifu wote, wakaingia tena mjini, na maombolezo makuu na vilio vya waovu vikasikiwa pote. Ndipo nikamwona Shetani akianzisha kazi yake tena. Alipita huko na huko kati ya watu wake, akawafanya walegevu na wanyonge wawe na nguvu, akawaambia ya kwamba yeye na malaika zake ndio wana uwezo. Aliwaonyesha watu milioni nyingi sana waliofufuliwa. Palikuwa na askari waliokuwa hodari na wafalme wenye akili katika kufanya vita, na ambao walikuwa wamezishinda falme kuu za dunia. Palikuwa na majitu hodari na mashujaa ambao tangu awali walikuwa hawajashindwa katika vita vyo vyote. Nalimwona Napoleon, yule jemadari hodari na mwenye kiburi, ambaye mashambulio yake yaliwatetemesha wafalme wa dunia. Naliwaona watu warefu na wenye kuadhimishwa, ambao walishindwa katika vita wakiwa na hamu ya kushinda

Walipoondoka katika makaburi yao, walianza kuwaza mambo jinsi walivyokuwa wakiwaza wakati wa kufa kwao. Walikuwa na hamu ile ile ya kushinda waliyokuwa nayo moyoni walipokufa. Shetani alishauriana na malaika zake, halafu akashauriana na wafalme na majemadari wakuu na

watu walio hodari. Ndipo akalitazama lile jeshi kubwa, akawaambia ya kwamba kundi la watu walioko pale mjini ni wachache tena ni wanyonge, tena wanaweza kupanda na kuuteka mji, na kuwafukuza watu wakaao ndani yake, na kuzitwaa mali zote zilizomo ndani na kuupata ule utukufu.

Shetani hufaulu kwa kuwadanganya, na ndipo wote wakajikusanya mara wajitayarishe kwenda vitani. Katika jeshi lile kubwa wako watu wengi walio stadi na wenye akili kwa vita, hao nao wakaunda aina zote za vifaa vya vita. Ndipo jeshi lile likaanza mwendo wao na Shetani akawaongoza, Wafalme na askari za vita vya zamani walitembea karibu na Shetani, na makutano walifuata nyuma makundi makundi. Kila kundi lilikuwa na mtangulizi, na walitembea kwa utaratibu juu ya nchi iliyobomoka wakielekea ule Mji Mtakatifu. Yesu akaifunga milango ya mji, na jeshi hili kubwa likazunguka mji, wakajipanga safu safu, wakiyatazamia mapigano makali.



SURA YA ISHIRINI NA MBILI

# KUMTAWAZA KRISTO

KRISTO alionekana tena mbele ya adui zake. Juu sana, kuelekea ule mji, juu ya msingi wa dhahabu inayong'aa sana, kulikuwa na kiti cha enzi, kilichoinuliwa juu sana. Mwana wa Mungu aliketi juu ya kiti kile, akizungukwa na raia za ufalme wake. Hakuna lugha inayoweza kuusimulia uwezo na utukufu wa Kristo, wala hakuna kalamu inayoweza kuuchora kadiri ya utukufu ule. Utukufu wa Baba wa Milele humfunika Mwana wake. Mwanga wa kuwapo kwake unajaza mji wa Mungu, hata ikaipita milango, ukiifunika dunia yote na kung'aa kwake.

Karibu na kiti cha enzi wanakaa wale ambao zamani walikuwa watenda kazi hodari wa Shetani, lakini walikuwa kama kinga kilichopokonywa motoni, wakamfuata Mwokozi wao kwa moyo wa upendo na bidii. Nyuma yao kuna watu wale waliotakasa tabia zao za Kikristo kati ya unafiki, wale walioiheshimu sheria ya Mungu, wakati ambao Wakristo wengine wengi walisema ya kwamba sheria ya Mungu imetanguka, na pamoja nao watu mamilioni katika vizazi vyote, waliouawa kwa ajili ya imani yao. Baada ya hayo nikaona "mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kiti kile cha enzi, na mbele za Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe,

wana matawi ya mitende mikononi mwao." Ufunuo 7:9. Vita vyao vimekoma, ushindi wameupata. Shindano lao limekwisha, nao wamelipokea tuzo. Matawi ya mitende mikononi mwao ni dalili ya shangwe yao kuu, na mavazi meupe ni dalili ya utakatifu wa Kristo usio na mawaa, ambao umekuwa wao.

Waliookolewa huimba wimbo wa sifa ambao unasikika kama mwangwi unaosikika katika pande zote za mbinguni, wakisema, "Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo." Malaika na maserafi huungana kwa sauti wakimsujudu Mungu. Waliookolewa walipokwisha kuuona uwezo na uovu wa Shetani, wakafahamu kuliko walivyojua mara ya kwanza, ya kwamba hakuna uwezo wo wote, isipokuwa ule wa Kristo mwenyewe, ulioweza kuwafanya wawe washindi. Katika kundi lile kubwa lenye kumetameta, hakuna hata mmoja mwenye kujidai ya kwamba uwezo wake ndio uliomwezesha kuupata wokovu, kana kwamba walishinda kwa ajili ya uwezo na wema wao wenyewe. Hakuna neno lo lote lisemwalo juu ya jambo lo lote walilotenda, wala maumivu yo yote waliyoyavumilia, lakini habari yote ya wimbo wao ndiyo hii: "Wokovu una Mungu wetu . . . na Mwana-Kondoo." Ufunuo 7:10.

Mwana wa Mungu atatawazwa mbele ya makutano ya wakaao mbinguni na duniani. Naye akipewa enzi kuu na mamlaka, Mfalme wa wafalme atawahukumu wale waliomwasi, tena atawahukumu kwa haki wale walioharibu amri zake na kuwatesa watu wake. Nabii wa Mungu asema hivi: "Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake, ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona

wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao." Ufunuo 20:11, 12.

Vitabu vya majina vitakapofunguliwa, na macho ya Yesu yatakapowatazama waovu, watayafahamu maovu yote ambayo walikuwa wameyatenda. Wataona dhahiri mahali ambapo miguu yao iliteleza ikiacha njia ya usafi na utakatifu, jinsi kiburi na uasi ulivyowaongoza hata wakaziharibu amri za Mungu. Madanganyifu na majaribu ambayo waliyakuza kwa ajili ya kuishikilia dhambi, mibaraka waliyoitumia vibaya, habari za rehema zilizowajia ambazo walizikataa kwa ajili ya mioyo migumu isiyoweza kugeuka—haya yote yataonekana kana kwamba yaliandikwa kwa nukta za moto.

### *Jinsi Shindano Kuu Lionekanavyo*

Juu ya kiti cha enzi ulionekana msalaba; na kama picha inayopitishwa, yalionekana mambo ya jaribu la Adamu na kuanguka kwake dhambini, na hatua zote zilizofuatana katika azimio la wokovu. Kuzaliwa kwa Mwokozi kwa namna ya unyenyekevu; maisha ya udogo wake ya unyofu na utiifu; ubatizo wake katika Yordani; kufungwa kwake na majaribu yake jangwani; kazi yake miongoni mwa watu, akiwafunulia wanadamu mibaraka ilivyo bora ya mbinguni; siku zake zilizojaa matendo ya upendo na rehema; kujitenga kwake nyakati za usiku akienda mlimani ili kuomba na kukesha; jinsi watu walivyomlipa fadhili zake wakimvizia kwa ajili ya wivu, chuki na kijicho; maumivu makuu aliyoyapata katika Gethsemane, akilemewa na uzito

wa dhambi za walimwengu wote; kusalitiwa kwake na kuwekwa mikononi mwa kundi la wauaji; mambo ya kuogofya yaliyotendeka usiku ule; mfungwa asiyejitetea aliyeachwa na wanafunzi wake wapendwa, akitembezwa hima kwa ufidhuli katika barabara za Yerusalemu; Mwana wa Mungu akipelekwa na kudhihakiwa mbele ya Anna, akishitakiwa katika pumba la kuhani mkuu, katika jumba al hukumu la Pilato, mbele ya Herode mkali, akitukanwa na kushambuliwa, akiumizwa vibaya, akihukumiwa kufa—haya yote yatafafanuliwa dhahiri kabisa.

Na hapo mbele ya makutano ya watu yatafunuliwa mambo ya mwisho katika maisha ya Kristo: Mshitakiwa mvumilivu asiye na hatia akienda kusulibishwa; Mfalme wa mbinguni akitundikwa msalabani; makuhani wenye kiburi na ghasia ya watu wakimcheka wakati wa maumivu ya kufa kwake; giza isiyo ya kawaida; dunia iliyopanda na kushuka kama mawimbi, miamba iliyopasuka, makaburi yaliyofunuka, yakionyesha wakati Mwokozi wa dunia alipofariki.

Mambo yale yote ya kushtusha yataonekana jinsi yalivyotokea hapa duniani. Shetani, malaika zake, na watu wake hawatakuwa na uwezo wa kugeuka wasitazame ufafanuzi wa matendo yao. Kila mmoja atakumbuka kazi yake aliyoifanya. Herode, aliyewaua watoto wadogo wa Bethlehemu kusudi amwue Mfalme wa Israeli; Herode mwovu, ambaye kwa ajili ya ubaya wa moyo wake Yohana Mbatizaji aliuawa; Pilato mnyonge, aliyetaka kuwapendeza wakuu; askari waliokuwa wakimdhihaki Yesu; makuhani na wakuu na makutano ya watu waliokasirika na kusema, "Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu."—Hawa wote wataona ubaya wa uovu wao jinsi unavyopita

kiasi. Watajaribu kujificha mbele ya utukufu wa uso wake ambao unang'aa sana kushinda mwanga wa jua, nao watakatifu wataziweka taji zao miguuni pa Mwokozi wakisema, "Alikufa kwa ajili yangu!"

Kati ya wale waliookolewa watakuwako mitume wa Kristo, shujaa Paulo, Petro mwenye juhudi, mpendwa Yohana mwenye upendo, na ndugu zao waliokuwa wanyofu mioyoni, na pamoja nao wataonekana kundi la mashahidi waliomfilia Kristo; na nje ya mji kitaonekana kila kitu kilicho kichafu, pamoja na wale watu waliowatesa mashahidi, wakiwatupa gerezani na kuwaua. Mfalme Nero, yule mkatili na mfisadi wa ajabu, atakuwapo akiwaona watu ambao aliwatesa kama sasa wameshangilia na kuheshimiwa; naye zamani alipokuwa akiwataabisha na kuwaumiza alipendezwa vibaya. Mama yake Nero pia atakuwa hapo, akiyashuhudia matokeo ya kazi yake mwenyewe kuziona tabia mbaya alizomfundisha mwana wake, na tamaa mbaya alizozikuza katika maisha ya mwana wake kwa mvuto wa matendo yake mwenyewe aone jinsi ambavyo mabaya yale yamezaa matendo ya uhalifu yaliyowashtusha walimwengu wote.

Pale watakuwapo maaskofu na mapadre wa Kanisa la Kirumi ambao walijidai kwamba ni wajumbe wa Kristo, na huku waliyaleta mateso makali, wakiwatupa watu gerezani na kuwachoma moto kusudi wapate kuwatuliza watu wa Mungu. Pale patakuwako na mapapa wenye kiburi ambao walijiinua juu ya Mungu na kuthubutu kuibadili sheria yake Aliye Juu. Wale waliojiita kuwa ni kama baba za kanisa, hawana budi kutoa hesabu kwa Mungu, jambo ambalo wangetamani waachiliwe. Watafahamishwa ya kwamba Yeye Ajuaye Yote huona wivu kwa ajili

ya sheria yake, na ya kwamba hatamwachilia ye yote aliye na hatia. Lakini watafahamu kwamba siku ya rehema imepita; wamekuwa wakichelewa kabisa. Watafahamu ya kwamba Kristo hujishughulisha na mambo ya watu wake wanaopotezwa; nao watayasikia maneno yake mazito, "Kadiri mlivyomtendea mmojowapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi." Mathayo 25:40.

*Katika Baraza ya Hukumu*

Walimwengu waovu wote watasimama mbele ya hukumu ya Mungu, wakihukumiwa kwa ajili ya kuihalifu amri ya mamlaka ya mbinguni. Hawana mwombezi ye yote awezaye kuwatetea; hawana udhuru wo wote; nao watahukumiwa kufa kwa milele.

Siku ile, itaonekana dhahiri ya kwamba mshahara wa dhambi siyo hali ya kujiwezea mwenyewe na kupata uzima wa milele, bali ni utumwa, uharibifu na mauti. Waovu wataona malipo ya maisha yao ya uasi. Walipopewa utukufu wa milele wakaudharau; lakini wakati ule wataona kwamba unafaa sana. Kila mtu aliyepotea atalia hivi, "Haya yote yangekuwa yangu, lakini nalichagua kuyazuia yasiingie katika maisha yangu. Loo, nilipumbazika ajabu! Nalikubali kuchagua maumivu, aibu na kushindwa, badala ya amani, furaha na heshima." Wote wataona ya kwamba wamekatazwa mbinguni kwa haki kabisa. Katika maisha yao walisema, Hatumtaki huyu Yesu atutawale.

Kana kwamba wamepumbazwa, naliwaona waovu wakilitazama tamasha la kutawazwa kwa Mwana wa Mungu. Mikononi mwake kuna mbau mbili za amri za Mungu, amri zile ambazo waovu walikuwa wakizidharau na kuziharibu. Watawaona waliookolewa wakiwa na furaha na

shangwe wakimsujudu Mungu; na sauti ya wimbo itakaposikiwa na makutano yale ya watu wasimamao nje ya mji, wote watapaaza sauti zao pamoja wakisema, "Ni makuu, na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; ni za haki, na za kweli, njia zako, Ee mfalme wa mataifa," (Ufunuo 15:3), hao nao wataanguka kifudifudi, wakimwabudu Mfalme wa uzima.



SURA YA ISHIRINI NA TATU

# MAUTI YA PILI

SHETANI atashangazwa sana akiiona fahari na utukufu wa Kristo. Yeye ambaye mara ya kwanza alikuwa kerubi mwenye kusitiri, atakumbuka siku ya kuanguka kwake. Yule ambaye alikuwa serafi anayeng'aa, "mwana wa asubuhi," amebadilika, naye ameshushwa ajabu!

Shetani ataona ya kwamba uasi wake aliouanzisha mwenyewe umemfanya asiwe na haki ya kuingia mbinguni. Daima amekuwa akizoeza nguvu zake kwa kushindana na Mungu, na kwa hivyo utakatifu, amani na usikilizano wa mbinguni ungekuwa kwake kama maumivu makali sana. Mashtaka yake yote juu ya rehema na haki za Mungu yatakomeshwa. Lawama zote alizokuwa akiweka juu ya Mungu, zitawekwa juu yake mwenyewe. Ndipo Shetani atainama na kuungama haki ya adhabu yake.

Mambo yote ya ukweli na ya uongo katika shindano ambalo limeendelea tangu miaka mingi yatadhihirishwa. Haki na uadilifu wa Mungu vitadhihirishwa na kuthibitishwa kabisa. Walimwengu wote wataona jinsi Baba na Mwana walivyokuwa wamejinyima ajabu kwa ajili ya wanadamu. Wakati utakuwa umefika kwa Kristo kuketi juu ya kiti cha enzi kwa kuwa anastahili, naye atatukuzwa

zaidi ya falme na mamlaka zote, na jina lake litatukuzwa zaidi ya majina yote.

Ingawa Shetani atashurutishwa kukiri ya kwamba hukumu zaMungu ni za haki, na kufanywa kujiinamisha mbele ya mamlaka na utukufu wa Kristo, lakini tabia zake zitadumu kuwa zile zile za zamani, wala hazitageuzwa. Moyo wa uasi utaonekana kwake ukiamshwa tena kwa nguvu kama nguvu ya tufani. Kwa moyo wa ghadhabu ataikaza nia yake asije kushindwa katika lile shindano kuu. Wakati wake utafika wa kufanya mashindano makali zaidi juu ya Mfalme wa mbinguni. Ndipo ataingia kati ya watu wake, atajaribu kuwafanya wawe na ghadhabu kama yake, na kuwachochea waanze kupiga vita mara. Lakini kati ya watu mamilioni ambao amewadanganya ili wamwasi Mungu, hakuna hata mmoja atakayekubali mamlaka yake. Uwezo wake wote utakoma. Waovu watajaa ile chuki inayomshika Shetani; lakini wataona ya kwamba hawawezi kitu, kwa kuwa hawawezi kumshinda Mungu. Ghadhabu yao itaanza kuwaka juu ya Shetani na wale waliomsaidia katika kazi ya udanganyifu. Watawarukia kwa uwezo mkuu kama wa mashetani, ndipo vita vitakuwa ulimwenguni pote.

### *Moto Kutoka Mbinguni*

Ndipo maneno haya ya unabii yatakapotimia: "Maana Bwana ana ghadhabu juu ya mataifa yote, na hasira kali juu ya jeshi lao lote: amewaangamiza kabisa, amewatoa waende kuchinjwa." Isaya 34:2. "Awanyeshee wasio haki mitego; moto na kiberiti, upepo wa hari, na viwe fungu la kikombe chao." Zaburi 11:6. Moto utashuka kutoka kwa Mungu mbinguni. Dunia itavunjika kabisa. Silaha ambazo

zimefichika chini ya ardhi zitaondolewa. Moto uteketezao utatoka katika kila shimo. Hata miamba itawaka moto. Siku itakuwa imekuja ambayo "inawaka kama tanuru." Malaki 4:1. "Viumbe vya asili vitaunguzwa na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea." (2 Petro 3:10). Moto wa Tofeth umewekwa kwa mfalme wa uasi, ameifanya kubwa, inakwenda chini sana; tanuru yake ni moto na kuni nyingi: na "pumzi ya Bwana, kama moto wa kiberiti, huiwasha." Isaya 30:33. Uso wa dunia utaonekana kama kitu kilichoyeyushwa—kama ziwa kuu la moto. Hii ndiyo siku ya hukumu na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu—"siku ya kisasi cha Bwana, mwaka wa malipo, ili kushindania Sayuni." Isaya 34:8.

Waovu watapata ijara yao duniani. "Watakuwa makapi: na siku ile inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa majeshi." Malaki 4:1. Wengine wataharibiwa mara moja lakini wengine wataendelea kupata maumivu kwa siku nyingi. Wote wataadhibiwa kwa namna ya matendo yao. Dhambi zote za watakatifu zitawekwa juu ya Shetani, mwanzishaji wa uovu, yeye ndiye atakayechukua adhabu yao. Hivyo ataadhibiwa, si kwa ajili ya uasi wake peke yake, lakini pia kwa ajili ya dhambi zote ambazo aliwafanya watu wa Mungu kuzitenda. Adhabu yake itakuwa kali mno zaidi ya wale ambao aliwadanganya. Baada ya wote waliodanganywa naye kufa wote, yeye ataendelea kuishi akiumizwa kwa muda fulani. Katika moto wa mwisho wa kuitakasa dunia, waovu wote wataharibiwa, shina na tawi —Shetani ndiye shina, na wafuasi wake ndio matawi. Haki ya Mungu itaridhika, na watakatifu na jeshi lote la malaika watasema kwa sauti kuu, Amina!

Dunia itakapokuwa ikiteketea kwa ghadhabu ya Mu-

ngu, watakatifu watakaa salama katika Mji Mtakatifu. Mauti ya pili haitakuwa na nguvu juu yao walio na sehemu katika ufufuo wa kwanza. (Ufunuo 20:6). Kwao waovu Mungu atakuwa moto ulao, lakini kwa watakatifu wake atakuwa jua na ngao. (Zaburi 85:11).



SURA YA ISHIRINI NA NNE

# ULIMWENGU MPYA

KISHA nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita." Ufunuo 21:1. Moto utakaoteketeza waovu ndio utakaoitakasa dunia. Dalili zote za laana zitafutiliwa mbali. Hakuna jehanum yo yote ambapo moto utawaka milele na kudumu kuwakumbusha waliookolewa matokeo na adhabu ya dhambi. Kutabaki ukumbusho mmoja tu: yaani, Mwokozi wetu atadumu kuwa na alama zile za kusulibishwa kwake. Kichwani mwake, mikononi na miguuni mwake, hapo tu ndipo zitakapoonekana alama za matendo ya ukali ambayo yaliletwa na dhambi.

"Na wewe, Ee mnara wa kundi, kilima cha binti Sayuni, utajiliwa; naam, mamlaka ya kwanza yatakuja." Mika 4:8. Ufalme ule uliokuwa umepotezwa kwa ajili ya dhambi, ulikombolewa na Kristo, na waliookolewa wataurithi pamoja naye. "Wenye haki watairithi nchi, nao watakaa humo milele." Zaburi 37:29. Kwa ajili ya kuogopa ili wasifanye makao ya watakatifu ya mbinguni kuwa kitu cha hakika hasa, wengi wameongozwa wayabatilishe mafundisho ya kweli yanayotuonyesha ya kwamba dunia mpya itakuwa makao yetu, nao wanasema ya kwamba maneno hayo hayaelezi juu ya makao halisi. Yesu aliwaahidia wanafunzi wake ya kwamba alikwenda kuwa-

andalia makao. Wale ambao wanayakubali mafundisho ya Neno la Mungu hawatakosa kujua habari ya makao ya mbinguni. Lakini mtume Paulo asema hivi, "Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (wala hayakuingia katika moyo wa wanadamu), mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao." 1 Kor. 2:9. Lugha za kibinadamu haziwezi kuusimulia ujira wa watakatifu. Ujira ule utafahamiwa na wale tu watakaoupokea. Hakuna fikara ya kibinadamu inayoweza kuufahamu utukufu wa pale anapokaa Mungu.

Katika Biblia, urithi wa watakatifu umeitwa nchi. (Ebr. 11:14-16). Hapo Mchungaji mkuu atawaongoza watu wake kwenye maji ya uzima. Mti wa uzima utatoa matunda yake kila mwezi, na majani ya mti ule ni ya kuwaponya mataifa. Kutakuwako na vijito vinavyotiririka daima, vyenye maji yaliyo safi kama kioo, na kando ya mito hiyo imepandwa miti ambayo itatupa vivuli vyake juu ya barabara itakayotembelewa na waliokombolewa na Bwana. Katika nchi ile, mabonde yatainuka na kuwa vilima vya kupendeza, na milima ya Mungu itainua vilele vyake. Katika nyanda zile za amani, kando ya mito hiyo ya maji ya uzima, watu wa Mungu, ambao tangu miaka mingi wamekuwa wageni na wasafiri, watayapata makao ya milele.

*Yerusalemu Mpya*

Yerusalemu Mpya ni hapo, "wenye utukufu wa Mungu, na mwangaza wake ulikuwa mfano wa kito chenye thamani nyingi kama kito cha yaspi, safi kama bilauri." Ufunuo 21:11. Bwana asema, "Nami nitaufurahia Yerusalemu, nitawaonea shangwe watu wangu." Isaya 65:19. "Maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya

maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita." Ufunuo 21:3, 4.

Katika mji wa Mungu "hamna usiku." Hakuna atakayetaka kupumzika. Hakuna ye yote atakayechoka kwa kuyatenda mapenzi ya Mungu na kulisifu jina lake. Tutadumu katika hali njema, wenye afya. "Wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru." Ufunuo 22:5. Badala ya mwanga wa jua utakuwako mwanga utakaong'aa bila kuyatia macho kiwi, ingawa utaangaza kwa nguvu zaidi ya mwanga wa adhuhuri yetu ya sasa. Utukufu wa Mungu na wa Mwana Kondoo utaufunika mji mtakatifu na mwanga usiofifia. Waliookolewa watatembea katika nuru mchana wa daima usio na haja ya mwangaza wa jua.

"Nami sikuona hekalu ndani yake; kwa maana Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-Kondoo, ndio hekalu lake." Ufunuo 21:22. Watu wa Mungu watakuwa na haki ya kuzungumza na Baba bila kizuizi. "Wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo." 1 Kor. 13:12. Tunauona mfano wa Mungu, kama kitu kionekanacho kwa kioo, tukimwona katika kazi zake za uumbaji, na kwa mambo anayowatendea wanadamu; lakini baadaye tutamwona uso kwa uso, bila kizuizi cho chote. Tutasimama mbele zake na kuutazama utukufu wa uso wake.

Katika nchi ile watu walio na hali ya kutokufa watajifunza kwa furaha isiyo na mwisho, wakiyachunguza maajabu ya uwezo wa uumbaji, na siri ya upendo ule uliowa-

komboa. Yule adui mkali hatakuwako, hakuna atakayewadanganya watu wamsahau Mungu. Uwezo wa akili za kila namna utaongezeka. Uwezo wa kufahamu utazidishwa. Fikara za watu hazitachoka kwa kujifunza mambo mapya, wala uchovu wo wote hautakuwako. Katika nchi ile, kazi zilizo bora kabisa zitaendeshwa, na mambo makuu yatafanywa, haja kuu zitatimizwa, na siku zote kutakuwako na mambo makuu zaidi ambayo itawapasa watu kujifunza, maajabu mapya ya kustaajabia, mafundisho mapya ya kufahamiwa, mambo mapya yatakayohitaji kufanywa kwa uwezo wa mikono, kwa fikara na moyo.

Na miaka ikizidi kupita, watu wataendelea kuyavumbua mambo makuu zaidi juu ya Mungu na juu ya Kristo. Kwa jinsi ujuzi utakavyoongezeka, ndivyo kutakavyokuwa na upendo, heshima na furaha pia. Kwa kadiri watu watakavyozidi kujifunza juu ya Mungu, ndivyo watakavyozidi kupendezwa na tabia yake. Yesu atakapowafunulia mambo makuu ya wokovu, na ushindi wa ajabu katika mashindano yake na Shetani, mioyo ya watakatifu itajaa furaha na heshima, na watazinyakua nyuzi za vinanda vya dhahabu kwa nguvu zaidi; na sauti elfu kumi na mara elfu kumi, na sauti maelfu maelfu zitaungana kwa kuuimba wimbo wa kumsifu Mungu.

"Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi na juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele." Ufunuo 5:13.

Dhambi na watenda dhambi hawataonekana tena, ulimwengu wote wa Mungu utakuwa safi, na shindano kuu litakuwa limekoma kabisa.